

**ATHARI ZA KIKURYA KATIKA UJIFUNZAJI WA KISWAHILI SANIFU
MIONGONI MWA WAKURYA**

JANETH MAHERI GEKONDO

**TASNIFU ILIYOWASILISHWA KWA AJILI YA KUKAMILISHA SEHEMU
YA MASHARTI YA SHAHADA YA UZAMILI (M.A KISWAHILI)
CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA**

2019

UTHIBITISHO

Aliyetia sahihi hapa chini anaithibitisha kazi kuwa ameisoma na hapa anapendekeza kuwa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kuikubali na kupokea tasnifu hii iliyoandikwa juu ya “Athari za Kikurya katika ujifunzaji wa Kiswahili Sanifu miongoni mwa Wakurya” katika kukamilisha baadhi ya matakwa ya shahada ya uzamili katika Kiswahili Isimu (M.A Kiswahili) ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.



Dkt Dunlop Ochieng

(Msimamizi)

.....
Tarehe

HAKIMILIKI

Hairuhusiwi kuiga au kunakili sehemu yoyote ile iliyomo ndani ya tasnifu hii bila idhini ya mwandishi ama Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa niaba ya mwandishi wa tasnifu hii.

TAMKO

Mimi **Janeth Maheri Gekondo** nathibitisha kwamba tasnifu hii ni kazi yangu halisi tena halali na haijawahi kuwasilishwa na haitawasilishwa katika chuo kingine kwa ajili ya kutunikiwa Digrii nyingine yoyote.

.....
Sahihi

.....
Tarehe

TABARUKU

Naitabaruku kazi hii kwa wadogo zangu wapendwa Francis Gekondo, Beatus Gekondo na Deogratius Gekondo ili iweze kuwa chachu kwa ajili ya kuendelea kutaka kujifunza zaidi na kwa bidii.

SHUKRANI

Awali ya yote namshukuru mwenyezi Mungu kwa fadhili zake na rehema zake kwa kunijalia uhai na afya njema, kadhalika amenisidia kufanikisha kazi yangu hii. Kazi hii imefanikiwa kutokana na utayari wa watu mbalimbali ambao walionyesha ushirikiano kwa mtafiti alipohitaji msaada na maelekezo kutoka kwao. Hata hivyo si rahisi kuwataja watu wote kwa majina ila nawashukuru wote nitakaowataja na ambao sitawataja kwa moyo wa dhati kwa namna mlivyojitoa na kuacha shughuli zenu ili kukamilisha kazi hii.

Kwa kipekee sana, napenda kumshukuru msimamizi wangu Dkt. Dunlop Ochieng. Amekuwa kiungo muhimu kuhakikisha kuwa nafanikiwa katika adhima ya utafiti wangu kwani alikuwa kiongozi, mshauri, na mwalimu mwema aliyenielekeza kwa unyofu na kunikosa kwa busara na hekima kubwa. Uvumilivu, umahiri na uchapakazi wake kwangu umezaa matunda ya mafanikio. Mwenyezi Mungu akubariki sana.

Aidha nawashukuru wahadhiri wote wa idara ya Kiswahili walionifunza masomo kwa kina na kwa weledi mkubwa. Umahiri wao na ujuzi wao umenifanya kupata mwanga na ufahamu zaidi katika taaluma hii ya Isimu. Kadhalika natoa shukrani zangu za dhati kwa wanafunzi wote tuliosirikiana wakati wote wa masomo ya uzamili. Mwenyezi Mungu awabariki sana.

Shukrani zangu maalum ziwaendee wazazi wangu wapendwa; baba yangu Mr. Marwa. W. Gekondo na mamaangu Maria Wegesa Nyakisegere, kwa namna

walivyoonyesha mapenzi yao yote kwangu ili nifanikiwe katika shahada ya uzamili. Kadhalika kaka zangu Francis Gekondo, Beatus Gekondo pamoja na Deogratius Gekondo kwa michango yao ya mawazo na ushauri mzuri uliniwezrsha kuwa na moyo wa kuendelea na utafiti huu pasipo kukata tamaa. Mwenyezi Mungu azidi kuwabarikia katika lililojema mnalolihitaji.

IKISIRI

Utafiti huu ulihusu athari za Kikurya katika ujifunzaji wa Kiswahili Sanifu miongoni mwa Wakurya. Uliongozwa na malengo makuu mawili. Lengo la kwanza lilikuwa ni kuonesha jinsi gani maneno ya lugha ya Kikurya yanaathiri ujifunzaji wa Kiswahili Sanifu. Na, lengo la pili lilihusiana na kubainisha sababu zinazohangia athari za Kikurya katika kujifunza Kiswahili Sanifu. Ili kukamilisha azma ya utafiti kama ilivyokusudiwa, mbinu za hojaji na mahojiano zilitumika katika kukusanya data. Kadhalika utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Fonolojia Zalishi Asilia ambayo huchunguza bayana athari hizo za lugha ya kwanza (Kikurya) katika kujifunza lugha ya pili yaani Kiswahili. Data za utafiti huu zilikusanywa katika wilaya ya Tarime ambayo ilichukuliwa sampuli kati ya wilaya za Butiama na Serengeti zenye wakazi wengi ambao wanatumia lugha ya Kikurya kama lugha yao ya kwanza mkoani Mara. Katika uchanganuzi wa data matokeo yalionesha kwa kina jinsi ambavyo lugha ya Kikurya imeathiri lugha ya Kiswahili sanifu hususani katika vipengele vya matamshi (fonolojia), morfolojia pamoja na tahajia (uandishi) ambavyo mtafiti alivichunguza. Pia matokeo ya uchanganuzi wa data yalionesha kuwa; athari za lugha ya kwanza, mitazamo finyu katika jamii na kukosekana kwa baadhi ya sauti katika lugha ya Kikurya ni sababu zilizochangia lugha ya Kiswahili kuathiriwa. Aidha, baada ya kubaini changamoto zinazohangia athari hizo kuwepo, utafiti huu umetoa mapendekezo ya kuweza kusaidia kuzuia athari hizo katika jamii hasa kwa wakazi wanaoishi maeneo ya vijini. Jamii inapaswa kuelimishwa thamani ya lugha ya Kiswahili ili iweze kuondokana na mitazamo potofu juu ya lugha ya Kiswahili. Kwa kufanya hivi tutakuwa tumesaidia wanajamii kuipenda lugha ya Kiswahili na hivyo itawasababisha wajifunze lugha ya Kiswahili kwa ufasaha na pia kuizungumza kwa ufasaha.

YALIYOMO

| | |
|---------------------------------------|------|
| UTHIBITISHO | ii |
| HAKIMILIKI | iii |
| TAMKO | iv |
| TABARUKU | v |
| HUKRANI | vi |
| IKISIRI | viii |
| ORODHA YA MAJEDWALI | xiii |
| SURA YA KWANZA | 1 |
| 1.0 UTANGULIZI | 1 |
| 1.1 Utangulizi | 1 |
| 1.1.1 Lugha ya Kikurya..... | 1 |
| 1.1.2 Lugha ya Kiswahili | 2 |
| 1.2 Usuli wa Tatizo | 3 |
| 1.3 Tamko la Tatizo la Utafiti | 5 |
| 1.4 Malengo ya Utafiti | 6 |
| 1.4.1 Lengo Kuu la Utafiti | 6 |
| 1.4.2 Malengo Mahsusi ya Utafiti..... | 6 |
| 1.5 Maswali ya Utafiti..... | 7 |
| 1.6 1.6 Umuhimu wa Utafiti..... | 7 |
| 1.7 Mipaka ya Utafiti | 8 |
| 1.8 Mpangilio wa Tasnifu | 8 |
| 1.9 Hitimisho..... | 8 |

| | |
|--|----|
| SURA YA PILI | 10 |
| MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA KINADHARIA | 10 |
| 2.1 Utangulizi | 10 |
| 2.2 Mapitio ya Kazi Tangulizi..... | 10 |
| 2.3 Mapitio Mbalimbali Kuhusiana na Lugha za Asili Zinayoathiri Lugha ya Pili (Kiswahili)..... | 10 |
| 2.3.1 Tafiti Mahususi Zilizofanywa Tanzania Kuhusiana na Lugha za Asili Zinayoathiri Lugha ya pili (Kiswahili)..... | 16 |
| 2.4 Mkabala wa Kinadharia | 18 |
| 2.5 Hitimisho..... | 22 |
| SEHEMU YA TATU | 23 |
| 3.0 MBINU ZA UTAFITI | 23 |
| 3.1 Utangulizi | 23 |
| 3.2 Eneo la Utafiti | 23 |
| 3.3 Usanifu wa Utafiti | 23 |
| 3.4 Kundi Lengwa | 24 |
| 3.5 Sampuli na Usamplishaji..... | 24 |
| 3.5.1 Sampuli..... | 24 |
| 3.5.2 Usamplishaji..... | 25 |
| 3.6 Data Zitakazokusanywa | 27 |
| 3.6.1 Data za Msingi | 27 |
| 3.6.2 Data za Upili..... | 28 |
| 3.7 Mbinu za Kukusanyia Data | 28 |
| 3.7.1 Hojaji..... | 29 |

| | | |
|------------|---|------------|
| 3.7.2 | Mahojiano..... | 30 |
| 3.7.3 | Usomaji wa Nyaraka Maktabani | 30 |
| 3.8 | Uchambuzi wa Data | 30 |
| 3.9 | Hitimisho | 31 |
| | SURA YA NNE..... | 32 |
| 4.0 | UWASILISHAJI, UCHAMBUZI NA MJADALA WA DATA | 32 |
| 4.1 | Utangulizi | 32 |
| 4.2 | Jinsi Maneno ya Lugha ya Kikurya Yanavyoathiri Ujifunzaji wa Kiswahili Sanifu | 32 |
| 4.2.1 | Athari katika Matamshi (Fonolojia)..... | 33 |
| 4.2.2 | Athari katika Mofolojia | 46 |
| 4.2.3 | Athari katika Tahajia | 73 |
| 4.3 | Sababu Zinazochangia Lugha ya Kikurya Kuathiri Ujifunzaji wa Lugha ya Kiswahili Sanifu | 89 |
| 4.3.1 | Athari za Lugha ya Kwanza | 89 |
| 4.3.2 | Mitazamo Finyu Katika Jamii | 92 |
| 4.3.3 | Athari za Sarufi Matamshi katika Lugha ya Kikurya..... | 95 |
| 4.4 | Hitimisho | 99 |
| | SURA YA TANO | 100 |
| 5.0 | HITIMISHO, MUHTASARI NA MAPENDEKEZO | 100 |
| 5.1 | Utangulizi | 100 |
| 5.2 | Muhtasari wa Utafiti..... | 100 |
| 5.3 | Mapendekezo ya Utafiti | 102 |
| 5.4 | Hitimisho | 103 |

| | |
|--------------------------|------------|
| MAREJEO | 105 |
| VIAMBATISHO | 115 |

ORODHA YA MAJEDWALI

| | |
|--|----|
| Jedwali 4.1: Kundi la Wazee (Watu Saba) Maneno Yaliyotolewa Kutamkwa | 34 |
| Jedwali 4.2: Kundi la Watu wa Kati (watu 7) Maneno Yaliyotolewa Kutamkwa . | 35 |
| Jedwali 4.3: Kundi la Vijana (Watu 7) Maneno Yaliyotolewa Kutamkwa | 36 |
| Jedwali 4.4: Sentensi Zilivyoandikwa Na Mtafitiwa Namba Mbili | 48 |
| Jedwali 4.5: Sentensi Zilivyoandikwa Na Mtafitiwa Namba Tatu..... | 49 |
| Jedwali 4.6: Sentensi Zilivyoandikwa Na Mtafitiwa Namba Nne..... | 50 |
| Jedwali 4. 7: Sentensi Zilivyoandikwa Na Mtafitiwa Namba Tano | 51 |
| Jedwali 4.8: Sentensi Zilivyoandikwa na Mtafitiwa Namba Sita..... | 52 |
| Jedwali 4.9: Sentensi Zilivyoandikwa na Mtafitiwa Namba Saba | 53 |
| Jedwali 4. 10: Sentensi Zilivyoandikwa Na Mtafitiwa Namba Nane..... | 54 |
| Jedwali 4.11: Sentensi Zilivyoandikwa Na Mtafitiwa Namba Tisa | 55 |
| Jedwali 4.12: Sentensi Zilivyoandikwa Na Mtafitiwa Namba Kumi | 56 |
| Jedwali 4.13: Sentensi Zilivyoandikwa Na Mtafitiwa Namba Kumi Na Moja | 57 |
| Jedwali 4.14: Sentensi Zilivyoandikwa Na Mtafitiwa Namba Kumi Na Mbili..... | 58 |
| Jedwali 4.15: Sentensi Zilivyoandikwa Na Mtafitiwa Namba Kumi Na Tatu | 59 |
| Jedwali 4.16: Sentensi Zilivyoandikwa Na Mtafitiwa Namba Kumi Na Nne..... | 60 |
| Jedwali 4.17: Sentensi Zilivyoandikwa Na Mtafitiwa Namba Kumi Na Tano | 61 |
| Jedwali 4.18: Matokeo ya Jumla ya Watafitiwa | 62 |
| Jedwali 4.19: Tahajia Sahihi na Tahajia Iliyokosewa Na Mtafitiwa Namba 1..... | 76 |
| Jedwali 4.20: Tahajia Sahihi Na Tahajia Iliyokosewa Na Mtafitiwa Namba 2 | 77 |
| Jedwali 4.21: Tahajia Sahihi Na Tahajia Iliyokosewa Na Mtafitiwa Namba 3 | 78 |
| Jedwali 4.22: Tahajia Sahihi Na Tahajia Iliyokosewa Na Mtafitiwa Namba 4 | 79 |
| Jedwali 4.23: Tahajia Sahihi Na Tahajia Iliyokosewa Na Tafiwa Namba 5 | 79 |

| | |
|--|----|
| Jedwali 4.24: Tahajia Sahihi Na Tahajia Iliyokosewa Na Mtafitiwa Namba 6..... | 80 |
| Jedwali 4.25: Tahajia Sahihi Na Tahajia Iliyokosewa Na Mtafitiwa Namba 7..... | 81 |
| Jedwali 4.26: Tahajia Sahihi Na Tahajia Iliyokosewa Na Mtafitiwa Namba 8..... | 82 |
| Jedwali 4. 27: Tahajia Sahihi Na Tahajia Iliyokosewa Na Mtafitiwa Namba Tisa... | 82 |
| Jedwali 4.28: Linaonesha Matokeo ya Jumla ya Watafitiwa..... | 83 |
| Jedwali 4.29: Sababu Zilizochangia Lugha Ya Kikurya Kuathiri Ujifunzaji wa Kiswahili Sanifu | 99 |

SURA YA KWANZA

1.0 UTANGULIZI

1.1 Utangulizi

Bara la Afrika linaundwa na nchi mbalimbali ambazo zina makabila tofauti tofauti. Tanzania ni miongoni mwa nchi hizo za bara la Afrika inayopatikana upande wa Mashariki. Wakazi wake hutumia lugha ya Kiswahili kama lugha rasmi ya Taifa pamoja na lugha zao za asili katika kuwasiliana. Lugha za asili za makabila haya zina athiri sana katika kujifunza lugha ya Kiswahili. Wakurya ni miongoni mwa makabila hayo. Hivyo, sura hii ya utangulizi inahusiana na mada ya utafiti ambayo inaangalia athari za Kikurya katika ujifunzaji wa Kiswahili Sanifu miongoni mwa Wakurya. Kwa undani, utafiti huu ulijikita zaidi katika kubainisha na kueleza dhana ya lugha ya Kikurya, historia ya lugha ya Kikurya pamoja na chimbuko la Wakurya. Iliangalia vilevile lugha ya Kiswahili, usuli wa tatizo, tamko la tatizo la utafiti, alengo ya utafiti, Maswali ya utafiti ambayo kimsingi utafiti umekusudia kuyajibu. Aidha, sura hii pia iliangalia mipaka ya utafiti na matatizo ya utafiti.

1.1.1 Lugha ya Kikurya

Wakurya ni moja ya makabila ya Tanzania ambayo yanaishi katika kanda ya ziwa Victoria upande wa mashariki katika mkoa wa Mara wilaya za Butiama, Tarime na Serengeti. Lugha kuu inayozungumzwa na Wakurya ni Kikurya. Tafiti mbalimbali ikiwemo ya Guthrie (1948) zinaonyesha wazi kwamba Kikurya ni miongoni mwa lugha zinazozungumzwa na Wabantu. Nurse na Hinnebusch (1993) wanaunga mkono hoja ya Guthrie (ameshatajwa) wanaposema kuwa wazungumzaji wa lugha

ya Kibantu wako katika makundi matano. Baadhi ya makundi hayo kama wanavyoonyesha yanatambulika kwa kuitwa Sabaki, Pamoko, Mijikenda pamoja na Nazija. Wanaendelea kusema kuwa ushahidi wa kiakiolojia na kiisimu unaonyesha kwamba “Mame – Swahili” ndilo kundi chimbuko la Kiswahili na kwamba kundi hili limetokana na kundi la Sabaki ambalo linahisiwa kujitenga kutoka katika makundi mengine mnamo karne ya kumi. Kwa hiyo, mahusiano ya kihistoria ya lugha ya Kiswahili kama yanavyoelezwa na Masebo na Nyangwine (2008) yanaonesha kuwa na mahusiano ya karibu na lugha nyingine za kibantu katika vipengele mbalimbali kama uambishaji, unyambulishaji, ngeli za majina na dhana zinazoandamana nazo. Lugha ya kikurya haiko tofauti katika mahusiano haya ya kibantu kama inavyoainishwa na Guthrie (ameshatajwa).

1.1.2 Lugha ya Kiswahili

Lugha ya Kiswahili ni lugha ambayo imepenya sehemu nyingi za bara la Afrika na Dunia kwa ujumla. Freeman Grenville (1959) kama alivyonukuliwa na Masebo na Nyangwine (2008) anasema kuwa lugha hiyo iliinukia katika sehemu mbalimbali za Upwa wa Afrika Mashariki miaka mingi iliyopita hasa katika maeneo ya Zanzibari, Pwani ya Tanzania pamoja na Kenya. Maelezo ya Freeman (ameshatajwa) yanaonesha kwamba lugha ya Kiswahili haikuanza sehemu moja maalumu. Hii ilidhihirishwa na baadhi ya maneno, majina ya watawala na maafisa wa serikali yalivyojitokeza katika fasili mbalimbali. Kwa mfano, katika historia ya Pate.

Shihabuddin Chiraghadin na Mathias Mnyapala (1988) wanaeleza kuwa asili ya lugha ya Kiswahili ni Kibantu ambacho kinazungumzwa zaidi katika Upwa wa Afrika

Mashariki, hasa maneno ya Pate, Unguja, Lamu, Comoro, Pemba, Mombasa, Kilwa pamoja na Tanga. Lugha ya Kiswahili ina tabia ya kusemwa, kuzungumzwa na kuandikwa kwa nia ya kukamilisha mawasiliano miongoni mwa wanajamii wa lugha ya Kiswahili. Ni lugha rasmi na lugha ya taifa kwa upande wa Tanzania ingawa kwa Watanzania wengi ni lugha ya pili. Kiswahili kina watumiaji wanaokadiliwa kuwa zaidi ya milioni 55 kwa Watanzania. Duniani kinakadiliwa kuwa na wazungumzaji zaidi ya milioni 150 kwa mujibu wa Iribemwangi (2010).

Hii inadhihirishwa kutokana na kuwepo kwa vituo mbalimbali vya redio na luninga vinavyotangaza kwa Kiswahili ndani na nje ya bara la Afrika kama vile sauti ya Amerika, BBC London, Sauti ya Uajemi, KBC na vingine vingi tu. Kiswahili pia kinafundishwa katika shule za msingi, sekondari na vya juu. Ghanen (2005) kama alivyonyukiwa na Nyanda (2015) pamoja na Njogu (2008) wanasema lugha ya Kiswahili ni miongoni mwa lugha kubwa barani Afrika. Kwa ukubwa huo kimekubalika kwa kupewa baraka zote na kuteuliwa kuwa lugha ya umoja wa Afrika. Inasemekana kwa sasa Kiswahili kina hadhi ya nafasi ya sita kimataifa kikitanguliwa na Kingereza, Kifaransa, Kihispania, Kiarabu na Kireno.

1.2 Usuli wa Tatizo

Watalamu mbalimbali kupitia maandiko yao wanakubaliana kuwa lugha ina tabia ya kuathiriwa na lugha nyingine. Masebo na Nyangwine (2007) kwa mfano wanasema kuwa lugha ina tabia ya kuathiriwa na lugha nyingine au kuathiri lugha zingine. Wanaonesha kuwa lugha ya Kiswahili imeathiriwa sana na lugha ya Kiarabu kwa kiwango cha asilimia thelathini na moja (31%) pamoja na lugha za Kibantu kwa

kiwango cha asilimia sitini na nne (64%). Anaendelea kusema maathiriano ya lugha katika jamii hutokana na athari za kimazingira au kijografia. Mbaabu (2007) akiunga mkono, alisema kuathiriana kwa lugha ni jambo la kawaida hasa pale watumiaji wanapoingiliana katika mazingira fulani. Anatoa mfano, Waarabu waliishi na Waswahili kwa muda mrefu sana. Katika mahusiano yao ya kuingiliana kwa shughuli mbalimbali iliwalazimu wajifunze lugha ya Kiswahili kwa ajili ya kuboresha mawasiliano.

Matinde (2012) anasema kwa upande wake kuwa muktadha wa matumizi ya lugha hutambulisha jamii husika kupitia kwa maneno na miundo yake. Alionyesha kuwa msemaji wa lugha yoyote ile anakuwa katika mazingira yanayo mtawala kimaisha, ambayo kimsingi ndiyo yanayomwamlia kuhusu vitendo na hata mazungumzo yake. Anatolea mfano mazungumzo ya ofisini, kanisani, hospitali, sokoni na mtaani.

Lugha ya Kiswahili nayo imeathiriwa na lugha za Kibantu kwa kutohoa maneno kutoka katika lugha za asili ambayo yamesanifishwa katika Kiswahili Sanifu na yanatumika kama msamiati sahihi hadi hivi leo. Kwa mfano, katika Kiswahili tuna msamiati wa neno /*Ikulu*/ ambao etimolojia yake ni kutoka lugha ya Kinyamwezi. Halikadhalika, neno /*Ngeli*/ limetokana na lugha ya Kihaya. Mekacha (2011) naye anaeleza kuwa lugha moja huathiriwa kutokana na muktadha wa matumizi yake. Watu mbalimbali wameathiriwa na lugha za kikabila wanapozungumuza Kiswahili Sanifu na kushindwa kutofautisha baadhi ya matamshi. Kwa mfano matamshi kati ya /*n*/ na /*m*/, katika kabila la Wamakonde badala ya kusema *mtu* wao wanasema

ntu. Hivyo basi, kutokana na sababu hii ya watu kuathiriwa na lugha za makabila wanapozungumza Kiwahili inamlazimu mtafiti kuchunguza kwa undani athari ya lugha ya Kikurya katika Kiswahili Sanifu.

1.3 Tamko la Tatizo la Utafiti

Changamoto zinazojitokeza mtu ajifunzapo lugha ya pili ni jambo la kawaida kutokea. Hii ni kwa sababu watumiaji wa lugha bado hawajaelewa vizuri kanuni za lugha ya pili. Changamoto mojawapo ni lugha ya mama kuathiri lugha nyingine kifonolojia, kimofolojia na pia kisintakisia. Watalamu mbalimbali wamejaribu kujadili tatizo hili kwa umakini wa hali ya juu. Masebo na Nyangwine (2007) wanasema Kiswahili kimeathiriwa kwa kiasi kikubwa na lugha za Kibantu. Alionyesha kuwa asilimia sitini nanne (64%) ya maneno katika lugha ya Kiswahili yana mfanano sana na lugha za asili za Kibantu.

Otiende (2013) alifanya utafiti wa athari za kimofonolojia za Kisoluba katika matumizi ya Kiswahili Sanifu kama lugha ya pili. Alibainisha kuwa matamshi ya lugha ya Kisoluba yana athari kubwa katika Kiswahili hususani katika wanafunzi wanaotumia Kiswahili kama lugha yao ya pili. Wenceslaus (2015) alifanya utafiti kuhusu athari ya lugha ya Kijita katika kujifunza Kiswahili. Alijikita kuangalia athari ya lugha ya Kijita zinazowafanya wanafunzi wasimudu kujifunza vyema wanapojifunza lugha ya Kiswahili. Tunaona watalam wote hawa, Masebo na Nyangwine (2007), Otiende (2013), Wenceslaus (2015) na Nyanda (2015) katika tasnifu zao, wameeleza kwa ujumla wao namna mbalimbali ambavyo lugha za makabila ya Kibantu zinavyoathiri lugha ya Kiswahili katika nyanja tofauti tofauti.

Hii ni kutokana na vile walivyoguswa kila mmoja kwa nafasi yake pale alipoona pengo la utafiti. Katika tafti zote hizi, hakuna mtaalam hata mmoja aliyeshughulikia athari za kabila la Kikurya katika ujifunzaji wa Kiswahili sanifu miongoni mwa Wakurya. Hali hii inatengeneza pengo linalotakiwa kufanyiwa utafiti kwa kusudi la kuelimisha jamii ya Wakurya ili waweze kuepuka makosa ya kisarufi watakapokuwa wakijifunza ama kuzungumuza lugha ya Kiswahili. Hii itasaidia kulinda hadhi ya lugha ya Kiswahili. kwa mfano, kutofuata sarufi sahihi ya lugha ya Kiswahili imekuwa ni tatizo kwa makabila mengi ya asili, idadi kubwa ya Wakurya hawawezi kutofautisha sauti /r/ na sauti // katika lugha ya Kiswahili. Kadhalika ukiangalia idadi kubwa ya wazungumuzaji wa lugha ya Kihaya hawawezi kutofautisha sauti /ngo/na /ng'o/ mara nyingi hutamka /ngombe/ badala ya /ng'ombe/.

1.4 Malengo ya Utafiti

1.4.1 Lengo Kuu la Utafiti

Lengo kuu la utafiti huu ni kuchunguza athari za Kikurya katika ujifunzaji wa Kiswahili Sanifu miongoni mwa Wakurya tukiangazia matumizi ya lugha ya kila siku.

1.4.2 Malengo Mahsusi ya Utafiti

Malengo mahususi ya utafiti huu ni kama yafuatayo:

- i) Kuonesha jinsi maneno ya lugha ya Kikurya yanayoathiri ujifunzaji wa Kiswahili sanifu.
- ii) Kubainisha sababu zinazohangia athari za Kikurya katika kujifunza Kiswahili sanifu.

1.5 Maswali ya Utafiti

Maswali ya utafiti ni dira ya kumuongoza mtafiti ili kufikia malengo yake ambayo ameyaaanisha. Katika utafiti huu, maswali yafuatayo ndio yatakayoongoza suala zima la utafiti unaohusu athari za Kikurya katika ujifunzaji wa Kiswahili Sanifu miongoni mwa Wakurya.

- i) Jinsi gani maneno ya lugha ya Kikurya yanaathiri ujifunzaji wa Kiswahili sanifu?
- ii) Ni sababu zipi zinachangia lugha ya Kikurya kuathiri ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili Sanifu?

1.6 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti ni utafutaji kwa minajili ya kuibua nyanja mpya ya taaluma au maarifa, au pengine kukuza ama kupanua nyanja ya taaluma ambayo ipo. Utafiti huu utasadia kwa kiasi kikubwa jamii mbalimbali kukabiliana na tatizo la athari za lugha za Kibantu katika ujifunzaji wa Kiswahili Sanifu, hususani jamii ya watu wanaozungumuza lugha ya Kikurya kama lugha yao ya kwanza katika suala la kujifunza Kiswahili Sanifu bila ya kukiathiri.

Katika taaluma, utafiti huu ukikamilika utakuwa msaada mkubwa kwa watafiti mbalimbali kwa kutoa muongozo kama sehemu ya mapitio ya kazi mbalimbali ili kuweza kuwapa mwanga katika tafiti zao. Pia utaibua chachu kwa watafiti wengine watakaopenda kutafiti juu ya athari za Kikurya katika ujifunzaji wa Kiswahili Sanifu miongoni mwa Wakurya pale watakapobainisha pengo. Aidha, utafiti huu utatumika kama mwongozo wa kuwasaidia walimu, wakufunzi, wanazuoni pamoja na wataalam wa isimu wanapokuwa wakifundisha, kutoa semina zinazohusiana na

maathiriano ya lugha, ama wakielimisha watu, kwani utasimama kama sehemu ya rejeleo.

1.7 Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu uliangalia athari zilizodhihirika katika matumizi ya Kiswahili miongoni mwa watumiaji wa lugha ya Kikurya kama lugha yao ya kwanza. Athari hizi ni zile zilizoonekana katika matamshi, tahajia pamoja na mofolojia (maumbo ya maneno katika sentensi). Aidha utafiti huu ulitegemewa kufanyika katika wilaya za Butiama, Tarime na Serengeti mkoani Mara. Na, kati ya hizo mtafiti alichagua wilaya ya Tarime tu. Ulihusisha watumiaji wote wa lugha ya Kikurya wanaotumia lugha hiyo kama lugha yao ya kwanza.

1.8 Mpangilio wa Tasnifu

Tasnifu hii imegawanyika katika sura tano. Kila sura imebeba mada kuu na mada ndogondogo zinazohusiana na utafiti huu. Sura ya kwanza ni utangulizi, ndani yake imeeleza vipengele mbalimbali ambavyo ni sehemu ya mwongozo katika utafiti huu. Sura ya pili inaeleza mapitio ya kazi tangulizi na mkabala wa kinadharia. Sura ya tatu iliwakilisha mbinu za utafiti, halikadhalika sura ya nne inaeleza juu ya uwasilishaji, uchambuzi na mjadala wa data za utafiti. Na sura ya tano ambayo ni ya mwisho ilieleza kuhusu hitimisho, muhtasari na mapendekezo ambayo yaliyotolewa na mtafiti baada ya kumaliza kazi ya utafiti.

1.9 Hitimisho

Katika sura hii tumejadili vipengele mbalimbali ambavyo ni sehemu ya mwongozo katika utafiti huu. Vipengele hivyo ni utangulizi, lugha ya Kikurya, lugha ya

Kiswahili, usuli wa tatizo, tamko la tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, mipaka ya utafiti pamoja na mpangilio wa utafiti.

SURA YA PILI

MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA KINADHARIA

2.1 Utangulizi

Sehemu hii iliwakilisha mapitio ya machapisho na kazi tangulizi mbalimbali ambazo zilihusiana moja kwa moja na mada ya utafiti au zinazokaribiana na mada ya utafiti pamoja na pengo la utafiti na mkabala wa kinadharia utakaotumika katika utafiti huu.

2.2 Mapitio ya Kazi Tangulizi

Mapitio ya kazi ni kitendo cha kurejea maandiko mbalimbali yanayohusiana na mada ya utafiti kwa kuyasoma. Maandiko ambayo yamekuwa yakirejelewa na watalam ama watafiti mbalimbali huwa na lengo la kuwasaidia kupata data wanazozitafuta. Maandiko hayo ni kama makala, vitabu, tafiti au majarida. Mtafiti alinufaika kupitia maandiko mengi kwa sababu alipata maarifa zaidi na kupanua uelewa wake kuhusiana na mada yake ya utafiti. Kutokana na kupitia kazi nyingi, ilikuwa rahisi kwa mtafiti kuweza kubaini pengo la utafiti na kulifanyia kazi.

2.3 Mapitio Mbalimbali Kuhusiana na Lugha za Asili Zinayoathiri Lugha ya Pili (Kiswahili)

Mada kuu ya utafiti ilihusu jinsi lugha mbalimbali za makabila zinavyoweza kuathiri lugha ya Kiswahili. Iliangalia athari za Kikurya katika ujifunzaji wa Kiswahili Sanifu miongoni mwa Wakurya. Waandishi wengi duniani wameandika kuhusu lugha nyingi za makabila zilivyoathiri Kiswahili. Walikubaliana kwa pamoja kuwa kila lugha ya kwanza huathiri lugha ya pili (Kiswahili) kwa njia yake ya kipekee kama

anavyoeleza Corder (1967). Mawazo haya katika ukweli wake yanaungwa mkono na Labov (1972) aliyesema kuna muachano mkubwa kati ya tabaka la chini na tabaka la juu. Aliendelea kusema kuwa mwachano huu husababisha athari katika matumizi ya lugha mahususi. Akitoa mfano, sauti /ʌ/ katika neno /sʌn/ inatumiwa na tabaka la juu wakati wa tabaka la chini wanatumia sauti /ɚ/ katika neno hilohilo. Vilevile, kiambishi /ɪŋ/ katika neno kama vile /coming/ kinatamkwa na tabaka la juu wakati tabaka la chini wanatamka kwa kuishia na kiambishi /ɪn/ katika neno hilohilo. Kazi ya Labov (ameshatajwa) ilitusaidia kuelewa pia kuwa maathiriano mengine katika lugha ni kutokana na matabaka yaliyopo katika jamii.

Ngonyani (1988) katika kuchunguza namna lugha za Kibantu zinavyoweza kuathiriana zenyewe kwa zenyewe hasa zile zenye uhusiano wa karibu, alilinganisha lugha ya Kindendeule, Kimatengo na Kingoni na akagundua lugha ya Kingoni imeathiriwa na lugha hizo. Kuathiriana kwa lugha hutokea kwa lugha zenye uhusiano wa karibu. Hata hivyo uhusiano huu ni mpana kiasi cha kuweza kutohoa maneno kutoka lugha moja kwenda nyingine ili kujiongezea msamiati utakaokidhi mahitaji ya jamii. Anaendelea kuonyesha kuwa lugha ya Kiswahili imetohoa baadhi ya maneno kutoka lugha za kigeni na hasa lugha za Kibantu. Kwa mfano, neno *Ikulu* kwa asili limetokana na lugha ya Kinyamwezi pia na neno *Ngeli* kwa asili limetokana na lugha ya Kihaya. Halikadhalika tukiangazia maneno ya kigeni pia lugha ya Kiswahili imetohoa. Kwa mfano neno *Mashine* kwa asili limetoka na lugha ya Kiingereza ‘Machinery’. Utafiti huu umetuongezea maarifa kwenye kazi hii kwani ulihusiana na mada ya utafiti.

Brown (1993) kama alivyonyukuliwa na Wenceslaus (2015) alifafanua kuwa athari za matamshi katika lugha ya pili hutokana na watumiaji wa hiyo lugha kukiuka kanuni na taratibu za lugha mahususi, yaani lugha ya pili. Naye Boshia (1993) katika kuchunguza athari za Kiarabu katika Kiswahili. Yeye alijikita katika ukopaji wa maneno kutoka katika Kiarabu yanayotumiwa katika Kiswahili. Aligundua kwamba asilimia arobaini na nne pointi tatu (44.3%) ya maneno yanayotumika katika Kiswahili chanzo chake ni Kiarabu. Anaendelea kueleza kwamba hali hiyo haifanyi lugha ya Kiswahili kuchukuliwa kuwa ni Kiarabu, lahaja ya Kiarabu au pijini ya Kiarabu. Mtaalamu huyu anasisitiza kwamba hakuna lugha ambayo inaweza kukua kipweke kama kisiwa bila kuathiriwa wala kuathiri lugha nyingine.

Were (1994) alitafiti athari zinazotokana na lugha ya kwanza ambazo huathiri lugha ya Kiswahili. Akitolea mfano wa wanafunzi, anasema kuna hali ya wanafunzi kujumlisha sheria na kuzihamisha toka lugha ya kwanza na kuzipeleka katika lugha ya pili ambayo ni Kiswahili Sanifu. Utafiti wake umetupatia maarifa zaidi katika kazi yetu kwani ulihusiana na mada iliyokuwa inahunguzwa. Wardhaugh (1994) kwa upande wake yeye alieleza kuwa lugha kuathiriana ni jambo la kawaida. Alisema kuwa sababu zinazoweza kuchangia lugha kuathiri au kuathiriwa na lugha nyingine ni kutokana na umbali wa kijografia hususani katika mazingira tofauti tofauti. Naye Onyango (1997) katika kazi yake aliangalia tofauti za kisarufi kati ya lugha ya Kinyala na Kiswahili na katika utafiti wake alijikita zaidi kwenye upatanifu wa Kisarufi. Kazi yake ilitusaidia kupata maarifa zaidi kwani ilihusika kama kazi tngulizi zilizo somwa na tafiti.

Muchome (1998) alichunguza mahusiano kati ya Cinamwanga na Kiingereza. Masuala aliyoyatilia maanani ni ujuzi wa lugha na tabia za kiisimu zinazotokana na mahusiano ya lugha hizi mbili. Madhumuni yake yalikuwa, kutoa maelezo ya kiisimu yanayotokana na maingiliano ya Cinamwanga na Kiingereza. Aligundua kuwa lugha ya Kiingereza imeathiriwa na lugha ya Cinamwanga ambayo ni lugha ya kwanza kutokana na watumiaji wa lugha ya Cinamwanga kuhamisha kanuni za lugha yao ya kwanza kwenye lugha ya Kiingereza kama anavyoeleza Ndungu (1999) kuwa kuna mtagusano mkubwa kwa watumiaji wa lugha ya kwanza wanapoitumia lugha ya pili. Mtagusano huo husababisha kuathiriana kwa lugha katika viwango vyote yaani fonolojia, mofolojia na sintakisia.

Munyua (2002) anasema kuwa athari za lugha ya kwanza kwa lugha ya pili husababisha makosa mbalimbali ya kimatumizi. Anaitumia dhana ya 'Viswahili' kurejelea matumizi potofu ya lugha ya Kiswahili kutokana na uhamishaji hasi kutoka kwa lugha mbalimbali za kwanza kama vile: Kibukusu, Kikisii, Kikikuyu, Kimeru, Kikalenjin na Kiluo. Alisisitiza kuwa athari husika hujitokeza katika viwango vyote vya lugha ambavyo ni: fonolojia, mofolojia, sintaksia na semantiki. Kuhusu idadi ya makosa katika tamko, Munyua alishikilia kuwa iwapo makosa ni mengi, tamko husika hukanganya; hivyo kutoeleweka. Alipendekeza kuwa tafiti zifanywe kuhusu 'Viswahili' kwa lengo la kuwaelekeza watunga mitaala ya Kiswahili kuzua mbinu mpya za ufundishaji wa Kiswahili sanifu. Ukweli huu unaungwa mkono na Ng'ang'a (2002) aliyetafiti juu ya makosa ya kisarufi katika insha za wanafunzi wa darasa la saba na jinsi yanavyoshughulikiwa na walimu katika tarafa ya Ndaragwa. Katika utafiti wake alibaini makosa ya kisintaksia, kisemantiki, kimofolojia na makosa ya

hijai kwenye insha za wanafunzi ambayo chanzo ni lugha mama. Lugha za kutafitiwa zilikuwa Kikuyu kama lugha ya kwanza na Kiingereza kama lugha ya pili.

Mukuthuria (2004), akichunguza kuathiriana kwa Kiswahili na lahaja ya Kitigania, alibaini ya kwamba kuna matatizo mengi ya kiisimu yanayowakumba wanafunzi wanaotumia lugha ya Kitigania wanapojifunza Kiswahili. Matatizo anayoyataja ni pamoja na yale ya kitahajia, kisarufi, uchanganyaji ndimi na kutafsiri dhana za Kiswahili kwa misingi ya Kitigania. Uchunguzi uliofanywa na mwanataaluma huyu ulithibitisha kwamba, chanzo cha matatizo hayo ni mifumo ya kifonolojia na kimofolojia ya lugha hizi.. Bartoo (2004) naye alichunguza kuhusu ujifunzaji wa sintaksia ya Kiingereza kwa wanafunzi wanaotumia Kikeiyo kama lugha ya kwanza, aligundua kuwa Kikeiyo kiliathiri mpangilio wa maneno katika sentensi za Kiingereza. Anasema kwamba, kutokana na tofauti za kimuundo kati ya lugha hizo mbili, wanafunzi husika walihamisha muundo wa nje wa kisintaksia wa lugha yao hadi kuwa katika lugha ya Kiingereza. Hali hii ilikuwa chanzo cha makosa aliyoyabainisha mtafiti huyu katika mpangilio wa maneno katika sentensi zilizotungwa na watafitiwa hao. Kazi zao ilitusaidia kupata maarifa zaidi kwani inahusiana na mada ya utafiti huu

Akichunguza athari za Kikisii katika ujifunzaji wa Kiswahili, Mangwa (2005) anaeleza kuwa kulikuwa na makosa yaliyodhihirika katika matumizi ya Kiswahili ambayo yalikuwa na chanzo chake katika lugha ya kwanza (Kikisii). Aliendelea kueleza kuwa makosa yaliyobainishwa yalichangia kuwapo kwa matokeo mabaya katika mtihani wa Kiswahili. Alieleza kuwa makosa hayo hujitokeza hasa katika

tahajia, sarufi na msamiati. Katika kuchunguza makosa husika, mtafiti huyu alitumia mijadala na uandishi wa insha kama chanzo cha data yake.

Masebo na Nyangwine (2007) na Mbaabu (2007) walithibitisha ukweli huu wa namna Kiswahili kilivyoathiriwa na lugha zingine hasa katika upande wa matamshi na tahajia. Kwa mfano, Wanyakyusa wanashindwa kutofautisha kati ya /f/ na /v/, “*hifi ni fiatu fyangu*” badala ya kusema “*hivi ni viatu vyangu*”. Hata hivyo walizidi kueleza kuwa mwingiliano kati ya Waarabu na Waswahili ulileta athari kubwa katika maneno ya lugha ya Kiswahili kwa sababu ilibidi Waarabu wajifunze Kiswahili kwa ajili ya mawasiliano, lakini hawakuweza kuzungumza Kiswahili fasaha na hivyo wakaiathiri lugha ya Kiswahili.

Hoja hii iliungwa mkono na Ngugi (2007), anasema kuwa lugha ya kwanza huathiri ujifunzaji wa lugha ya pili katika kiwango cha fonolojia. Katika kuchunguza namna lugha ya Kikikuyu ilivyoathiri ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili, mtafiti huyu aligundua kuwa athari husika zilijitokeza katika matamshi na pia katika tahajia. Ngugi amesisitiza kwamba makosa mengi yaliyojitokeza katika matumizi ya lugha ya wanafunzi wa shule za upili waliotumiwa kama watafitiwa, yalitokana na uchopekaji, udondoshaji na unazalishaji. Ameeleza kwamba, mifanyiko hiyo ya kifonolojia ilidhihirika katika matumizi ya lugha ya wanafunzi husika huku makosa yakijitokeza kutokana na tofauti katikamifumo ya lugha hizi mbili. Kadhalika King’ei na Kobia (2007) walionesha changamoto za lugha ya Sheng nchini Kenya ku zinayoathiri lugha ya Kiswahili. Kazi hizi zimemsaidia mtafiti kuongeza maarifa zaidi alipokuwa akichunguza kwani zilihusiana kwa ukaribu na mada ya utafiti.

Otiende (2013) katika utafiti wake alionesha athari za kimofonolojia za Kisoluba zinayoathiri lugha ya Kiswahili. Alidhihirisha kwamba kuna tofauti kubwa baina ya mifumo ya fonimu za Kiswahili na Kisoluba ambayo huathiri matumizi ya Kiswahili. Lusesa (2013) alichunguza athari zinazopatikana katika Kiswahili Sanifu kwa watumiaji wa lugha ya Kisukuma ikiwa ndiyo lugha yao ya kwanza. Anaendelea kusema, ni vyema watafiti mbalimbali wakijihusisha katika suala la kuchunguza athari za lugha ya Kibantu katika Kiswahili Sanifu na kisha kuvumbua mbinu ambayo itawasaidia watumiaji wa lugha za Kibantu katika kujifunza Kiswahili Sanifu kwa ufasaha bila ya kuvunja sheria na kanuni za lugha ya Kiswahili. Naye Macharia (2013) katika utafiti wake alichunguza athari za fonolojia ya lugha ya Kikikuyu katika uandikaji/othografia ya Kiingereza. Sampuli yake ilikuwa wanafunzi wa shule nne za upili (Kikuyu Township, Stonebic, shule ya wasichana ya Riaru Springs na Elizabeth Academy). Alibaini kuwa makosa mengi yaliyopatikana yalikusiana na fonolojia ya lugha ya kwanza. Kazi za watalam hawa zimetoa mchango katika kufanikisha utafiti huu kwani zilihusika kama kazi tangulizi ambazo mtafiti alizisoma na kupata maarifa zaidi kuhusiana na mada ya utafiti wake.

2.3.1 Tafiti Mahususi Zilizofanywa Tanzania Kuhusiana na Lugha za Asili

Zinayoathiri Lugha ya pili (Kiswahili)

Kuna tafiti mbalimbali ambazo zimekwisha fanyika nchini Tanzania zinazoongelea mada inayokaribiana au inayoelekeana na mada ya utafiti huu. Miongoni mwa tafiti hizo ni pamoja na Mochiwa (1979) alitafiti athari ya Kiswahili kwa Kizigua (lugha inayozungumzwa katika wilaya ya Handeni, eneo la Tanga, Kaskazini Mashariki mwa Tanzania). Utafiti huo ulichunguza ujuzi wa lugha; ruwaza zilizojitokeza katika

matumizi ya lugha, na mielekeo ya wanajamii kuhusu Kiswahili na Kizigua. Hivyo basi, kutokana na mapitio ya kazi mbalimbali tangulizi za waandishi inadhihirika wazi kuwa maingiliano ya makabila na matamshi mbalimbali ya lugha zao yanaathiri sana lugha ya Kiswahili Sanifu.

Ngonyani (1988) naye alichunguza namna lugha za Kibantu zinavyoweza kuathiriana hasa zile zenye uhusiano wa karibu. Kama ilivyoonesha kwenye ukurasa wa 14, alilinganisha lugha ya Kindendeule, Kimatengo na Kingoni na akagundua kuwa lugha ya Kingoni imeathiriwa na lugha hizo. Anasema lugha ya Kingoni haikuwa na fonimu /i/ katika matamshi yake lakini kwa sababu ya mahusiano ya karibu na hizi lugha fonimu /i/ sasa hupatikana katika matamshi ya lugha ya Kingoni.

Lusesa (2013) kwa upande wake alichunguza athari zinazopatikana katika Kiswahili Sanifu kwa watumiaji wa lugha ya Kisukuma ikiwa ndiyo lugha yao ya kwanza. Alishauri kuwa ni vyema watafiti mbalimbali wanapojihusisha katika kuchunguza athari za lugha ya Kibantu katika Kiswahili Sanifu pia wajikite vilevile kuvumbua mbinu ambazo zitawasaidia watumiaji wa lugha za Kibantu katika kujifunza Kiswahili Sanifu kwa ufasaha bila ya kuvunja sheria na kanuni za lugha ya Kiswahili

Wenceslaus (2015), yeye alitafiti kuhusu athari ya lugha ya Kijita katika kujifunza Kiswahili. Aliangalia athari za lugha ya Kijita zinazowafanya wanafunzi wasimudu kujifunza vyema wanapojifunza lugha ya Kiswahili. Alieleza ni njia zipi zitumike ili kuwasaidia wanafunzi walioathiriwa na lugha ya Kijita katika kujifunza Kiswahili sanifu. Nyanda (2015) katika kazi yake iliyohusu athari ya lugha ya Kinyamwezi

katika kujifunza Kiswahili, alishughulikia zaidi athari zinazopatikana katika matamshi, msamiati na maana kwa ujumla. Hata hivyo mtafiti huyu alibainisha mbinu za kutumia ili kuwasaidia watumiaji wa lugha ya Kinyamwezi hasa wanafunzi wanapojifunza Kiswahili kama lugha ya pili ili kuepuka makosa ya Kisarufi. Naye Athumani (2015) katika utafiti wake, alionesha athari za kiisimu za lugha ya Kiswahili katika lugha ya Kiyao. Alisema lugha ya Kiyao imeathiriwa sana na lugha ambazo zinahusiana nayo kwa karibu. Kazi za watalam hawa zilimsaidia mtafiti kupata marifa zaidi kuhusiana na utafiti aliokuwa anaufanya. Hivyo basi, mapitio ya kazi zote hizo yanadhihirisha kuwa hakuna utafiti uliofanyika katika lugha ya Kikurya kuonyesha mchango wake katika kuathiri ujifunzaji wa Kiswahili Sanifu miongoni mwa wakurya, na hivyo kusabibisha pengo la utafiti.

2.4 Mkabala wa Kinadharia

Kila utafiti unaofanywa huwa na lengo la kupata mafanikio. Ili utafiti uweze kufanikiwa ni lazima kuwe na muongozo ambao utakuwa dira kwa jambo hilo. Muongozo huo waweza kuwa nadharia ambayo itaongoza shughuli yote ya utafiti kwa sababu hubeba mawazo, dhana au maelezo juu ya jambo fulani. Tullock (1960) akinukuliwa na Kerlinger (1979) anaeleza kuwa nadharia ni muhimu kwa vile humwelekeza mtafiti katika kuyafikia malengo ya utafiti wake. Aidha, nadharia humwelekeza mtafiti katika uteuzi wa njia ambazo zitaweza kusaidia kupata data mwafaka ambayo itaibua majawabu yatakayoafikiana na nadharia iliyotolewa. Hivyo basi, nadharia kama ilivyofafanuliwa na Massamba (2004) ni kanuni na misingi ambayo hujengwa katika muundo wa kimawazo kwa madhuuni ya kutumia kama kiolezo ya kueleza jambo. Naye Mdee na wenzake (2011) kama

alivyonukuliwa na Matinde (2012) anasema nadharia ni mpango wa mawazo uliotungwa ili kueleza jinsi ya kufanya au kutekeleza jambo fulani.

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Fonolojia zalishi Asilia ambayo iliasisiwa na Venneman (1972). Sababu kubwa ya kutumia nadharia hii ni kwamba nadharia ya Fonolojia Zalishi iliyokuwepo ilionekana kuwa na mapungufu makubwa. Mfano, Massamba (2011) alielezea Fonolojia Zalishi kuwa ni mkabala wa kinadharia unaochunguza kanuni na sheria za kimajumui zinazoonesha jinsi gani umbo la ndani na la nje vinavyohusiana. Waasisi wake ambao ni Noam Chomsky na Morris Halle, wao walitilia mkazo umbo la ndani na umbo la nje katika uwakilishi wa vipengele vya kifonolojia na kuonesha uhusiano uliopo baina ya maumbo haya. Aidha walitoa sheria zinazoongoza ukokotoaji wa maumbo hayo na kuziita michakato ya kifonolojia. Fonolojia zalishi imejadiliwa katika kitabu maarufu kitiwacho *Sound Pattern of English*, yaani *Ruwaza ya Sauti katika lugha ya Kiingereza 1968*. Kutokana na udhaifu huo, nadharia ya Fonolojia Zalishi Asilia ilishika nafasi na kustawi. Iiendelezwa na Joan Hooper katika tasnifu yake iliyojulikana kwa jina la "Aspect of Generative Phonology" ambayo baadae aliichapa na kuwa kitabu mwaka 1976 na kilijulikana kwa jina la *Introduction to Natural Generative Phonology (INGP)*. Ilichunguza maumbo ndani ya maneno na kupunguza udhahania, kadhalika ilifanikiwa kuonesha muundo wa neno halisi yaani muundo wa ndani wa neno kutoka muundo wa nje. Aidha inamsaidia mchunguzi wa lugha kutabiri makosa yanayoweza kutokea pia usahihi kuhusu lugha asilia. Hooper (ameshatajwa) analieleza jambo hili kuwa ni kanuni ya ujumuishaji sahihi. Anazidi kueleza kuwa kanuni hii inasaidia kuonesha uhusiano kati ya miundo na kauli za kijumla

zinazotakiwa kudhihirika katika kila neno. Kadhalika sheria zinazomwongoza mzungumzaji hutokana na miundo nje ya maneno na si muundo ndani.

Sheria ya kurejelewa kwa kipande cha neno kisichokuwepo haikupata nafasi katika mtazamo wa nadharia hii na kwa kufanya hivyo ilidhibiti matumizi ya uwezekano pamoja na udhahania. Kwa hiyo, nadharia ya fonolojia zalishi asilia imedadavua kwa uwazi miundo ndani na nje kwa kutumia kanuni ya uasilia kamili. Kanuni ilisisitiza kwamba sheria zinazokubalika kifonolojia na kimofolojia lazima zioneshe ujumulishaji sahihi wa muundo nje wa maneno, pia ilionesha kuwa mtu anayechunguza lugha kwa kutumia data ya miundo nje ya maneno hataweza kushughulikia miundo dhahania. Nadharia hii imegawanyika katika makundi makuu manne ya sheria, ambayo ni sheria za Kifonetiki, sheria za Kimofolojia, sheria za Via pamoja na sheria za Sandhi.

i) Sheria za Kifonetiki

Kanuni hizi hutokea katika mazingira ambayo ni ya kifonetiki kamili. Kama anavyoeleza Mgullu (1999) kuwa fonetiki ni tawi la sayansi ya isimu linalo shughulikia utamkaji wa sauti za binadamu na usikiaji wake. Kwenye utafiti huu, hii sheria imesaidia kumwongoza mtafiti kuweza kushughulikia kipengele cha matamshi kwa kubainisha matamshi sahihi na yasiyo sahihi.

ii) Sheria za Mofolojia

Kanuni hizi zilihusika na uchanganuzi wa maumbo ya maneno yaani namna ambavyo zinaweza kurejelea kategoria za kisintaksia kama njeo, hali ya wingi wa maneno, nomino pamoja na vitenzi. Kadhalika kanuni hizi hushughulikia maana katika lugha husika. Katika utafiti huu, sheria hizi

zimesaidia kumwongoza mtafiti kuweza kushughulikia kipengele cha athari za mofolojia katika sentensi kwa kubainisha maana halisi ya sentensi pamoja na maumbo ya maneno jinsi yalivyotumika.

iii) Sheria za Via

Kanuni za via zinawawezesha watu kuhusisha elementi za kileksika ambazo hutofautia kwenye miundo nje. Kanuni hizi hazizalishi elementi kwa hiyo hazilinganishwi na nyingine katika maneno kwa wazungumzaji wa lugha. Kanuni hizi zimesaidia katika utafiti huu kuweza kubaini maana halisi ya maneno ambayo yamekosewa katika tungo au sentensi na kuonesha yanavyo stahili kuwa.

iv) Sheria za Sandhi

Sheria hizi hutokea wakati ambapo vokali zinazofanana huvutana na kutokea kama sauti nyingine. Kanuni hii imesaidia kubaini sauti ambazo zinaathiriana katika utafiti huu na kueleza sababu za kuathiriana hivyo.

Kwa hiyo mtafiti anaona vyema kutumia nadharia hii kwa sababu ina uwezo wa kuchunguza hata maneno yaliyotoholewa kutoka lugha ngeni na jinsi yalivyoweza kupatikana hasa katika lugha mahususi. Pia ina uwezo wa kufanya mabadiliko zaidi ya kimuundo katika neno lote. Mfano, maneno “*electric*” na “*electricity*” ukilinganisha na maneno “*coo*” na “*key*” katika jozi ya kwanza utaona *k* ya *electric* inakuwa *s* katika neno “*electricity*”. Hapa utaona umbo la sauti ile ya kwanza limebadilika kabisa na kuwa sauti tofauti kabisa. Aidha jozi ya pili utaona kuwa sauti ya kwanza katika neno *coo* (yaani *k*) ni sawa na sauti ya kwanza katika neno “*key*”, ila tu yenyewe imesogea mbele kwenye kaakaa imekuwa *ky*. Ubadilishaji wa

namna hii unapotokea hudhibitiwa na sheria ambazo zinahusu taarifa za kimofolojia, kisintaksia na kileksika. Kadhalika inaonesha muundo wa neno halisi. Jinsi ambavyo muundo ndani wa neno ulivyo katika uhalisi wake ikihusisha kutoka muundo nje wa neno. Hii ni kwa sababu ina uwezo wa kupanua miundo sahihi ya lugha zaidi ya moja na kueleza visababishi vya kila athari itakayodhihirika katika upanuzi wa miundo hiyo. Mfano katika maneno yafuatayo utaweza kutambua umbo ndani la neno (halisi) na umbo nje la neno.

| Umbo ndani la neno | umbo nje la neon |
|---------------------------|-------------------------|
| /si + tuka/ | stuka] |
| /mu + ana/ | mwa:na] |
| /ki +etu/ | čɛ: tu] |
| /Ma +ino/ | meno] |
| /N +bao / | Mbao] |
| /wa + ingi/ | [wengi] |

Hivyo basi, nadharia hii itakuwa ya pekee katika utafiti huu kwani ni sehemu ya kuweza kuhusianisha taratibu, kanuni na sheria zinazotawala mfumo mzima wa lugha hizi mbili yaani Kikurya pamoja na Kiswahili, na hivyo, itakuwa msaada wa kuweza kufanikisha lengo la utafiti huu.

2.5 Hitimisho

Katika sura hii tumeona mapitio ya kazi tangulizi ambazo zilihusiana moja kwa moja au kukaribiana na mada ya utafiti huu. Kadhalika pengo la utafiti pamoja na mkabala wa kinadharia uliotumika kuongoza utafiti vilibainishwa sehemu hii. Na sehemu ya mwisho kwenye sura hii ni hitimisho.

SEHEMU YA TATU

3.0 MBINU ZA UTAFITI

3.1 Utangulizi

Katika sehemu hii tuliangalia mbinu za utafiti ambazo zilitumika katika kukusanya na kutafiti data. Kwa mujibu wa Weiss (1972) mbinu za utafiti ni jumla ya mbinu zote zinazotumiwa katika kufanya utafiti. Vipengele vitakavyobainishwa katika sehemu hii ni eneo la utafiti, usanifu wa utafiti, sampuli na usamplishaji, data zitakazohusika katika utafiti pamoja na mbinu zitakazohusika kukusanyia data.

3.2 Eneo la Utafiti

Utafiti huu ulitegemea kufanyika katika Mkoa wa Mara wilaya za Tarime, Butiama na Serengeti. Kati ya hizi mtafiti alichagua wilaya ya Tarime tu kwa sababu ilikuwa rahisi kwake kupata data alizokusudia katika kufanikisha lengo la utafiti huu. Aliamini angepata athari za Kikurya katika hatua mbalimbali za ujifunzaji wa Kiswahili sanifu. Kijografia, maeneo haya yapo karibu na makazi ya mtafiti na kwa hivyo ilikuwa rahisi kwa mtafiti kuyafikia kwa haraka na pia kupunguza gharama kwa matumizi ya mtafiti, kama vile gharama ya usafiri.

3.3 Usanifu wa Utafiti

Usanifu wa utafiti ni mchoro, ramani au mpangilio unaoonyesha namna utafiti utakavyofanyika, tangu zoezi la kukusanya data, kuchambua data na kuandika ripoti ya utafiti. Utafiti wetu ulikuwa uchunguzi wa kifani na ulifanyika katika mkoa wa Mara. Mkabala uliotumika katika utafiti huu ni mkabala wa kinaelezo ambao ulijikita katika nadharia ya Fonolojia Zalishi asilia. Mtafiti alichagua mkabala huu

kwa sababu data zilikazokusanywa zilifafanuliwa kwa njia ya maelezo. Pia asilimia kubwa ya tafiti zinazohusu lugha kama vile isimu na fasihi ni za kimaelezo. Kama anavyoeleza Cohen (2000) kuwa mkabala huu ni wa kupanga kutoa sababu na kuzieleza data kama zilivyoielezwa na walengwa wa utafiti. Utafiti huu ulikuwa wa maskani. Utafiti wa maskani kwa kawaida huhusisha ukusanyaji wa data kutoka maskanini kwa kutumia mbinu mbalimbali kama hojaji pamoja na mahojiano.

3.4 Kundi Lengwa

Kulingana na Cooper (1989), Vans (1990) na Orodhoo (2004) kundi lengwa linamaanisha wanachama wote au hata mtu mmoja, kundi ama elementi ambazo mtafiti amekusudia kuzihusisha katika utafiti wake. Yaani, ni jumla ya walengwa wote wa utafiti ambapo sampuli inaweza kuchaguliwa. Utafiti huu katika kuainisha kundi lengwa, ulihusisha makundi rika ya vijana, watu wenye umri wa kati pamoja na wazee kwa kuzingatia jinsia zao. Makundi yote haya ni mahiri katika uzungumzaji wa lugha ya Kikurya na wanaoishi katika wilaya ya Tarime katika mkoa wa Mara. Mtafiti alichagua makundi hayo kwani yalimwezesha kupata data zilizomsaidia kufanikisha utafiti wake uliohusu Athari ya Lugha ya Kikurya katika Kiswahili Sanifu. Aidha, aliamini kuwa kwa kufanya hivyo kutamsaidia kutimiza malengo yake kwa usanifu mkubwa.

3.5 Sampuli na Usamplishaji

3.5.1 Sampuli

Sampuli ni sehemu ya idadi ya watu ambayo mtafiti anavutiwa nayo katika kupata taarifa na kutoa hitimisho la utafiti wake. Mtazamo wa Kothari (1990, 2004) na

Babbie (1992) hauko mbali pale wanaposema kuwa sampuli ni kundi dogo la watafitiwa lililochaguliwa kuwakilisha sifa na tabia za kundi zima ambalo humsaidia mtafiti kupata taarifa kutoka sampuli hiyo ili kutoa majumuisho ya utafiti wake. Utafiti huu ulitumia mbinu mbili za uteuzi wa sampuli ambazo ni mbinu bahatishi (Sampuli nasibu) na mbinu ya makusudi (sampuli lengwa). Jumla ya watafitiwa katika utafiti huu walikuwa watu mia (100). Lakini kwa kutumia mbinu hizi mbili zilizotajwa hapo juu, sampuli sasa ilikuwa na watu ishirini na moja (21), ambapo kundi rika la vijana lilikuwa na watu saba (7), kundi rika la watu wa kati nalo watu saba (7) na kundi rika la wazee watu saba (7). Madhumuni ya uteuzi wa mbinu hizi mbili ni kuzuia hali ya upendeleo na kumfanya kila mtafitiwa kuona ana haki ya kushiriki. Aidha uchaguzi na mgawanyo wa sampuli lengwa ulifanywa kwa kuzingatia maelezo ya Kothari (ameshatajwa).

3.5.2 Usampulishaji

Usampulishaji ni mchakato wa kuchagua kundi dogo kutoka katika kundi kubwa la watafitiwa ili kufanya makisio ya kundi lengwa. Maelezo haya yanaungwa mkono na Sigh (2007), Adam na Kauzora (2008) wanaosema kuwa usampulishaji ni mbinu, mchakato au kitendo cha kuwatafuta walengwa wa utafiti. Hivyo basi, walengwa wa utafiti wetu walipatikana kupitia sampuli nasibu na sampuli lengwa. Mbinu iliyotumika kupata sampuli kati ya kundi rika la vijana na kundi rika la watu wa kati ni usampulishaji nasibu. Kwa upande wa kundi rika la wazee mbinu iliyotumika kuwapata ni usampulishaji lengwa (makusudi). Mgawanyo wa kupata sampuli kutoka kwenye kundi kubwa la watafitiwa ulikuwa kama unavyooneshwa kwenye jedwali hapa chini.

Jedwali 3.1: Mgawanyo wa Kupata Sampuli Kutoka Kwenye Kundi Kubwa

| Na | Aina ya kundi | Idadi ya kundi lengwa (populesheni) | Idadi ya sampuli kwa kila kundi | Mbinu zilizotumika kuteua sampuli lengwa |
|----|----------------------------|-------------------------------------|---------------------------------|--|
| 1 | Kundi rika la vijana | 34 | 7 | Sampuli nasibu |
| 2 | Kundi rika la watu wa kati | 33 | 7 | Sampuli nasibu |
| 3 | Kundi rika la wazee | 33 | 7 | Sampuli makusudi |
| 4 | Jumla kuu | 100 | 21 | 2 |

Usampulishaji katika kupata sampuli ya watu ishirini na moja (21) kwa ulinganifu wa watu saba (7) kutoka kila kundi ulizingatia alichokisema Patton (2001) kuwa hakuna sheria za idadi katika uteuzi wa sampuli ya utafiti, muhimu ni mtafiti kufikia sampuli kifu. Katika kundi rika la vijana mtafiti aliandaa namba kuanzia moja hadi thelathini na nne (1 - 34) kisha watafitiwa wote waliokuwa uwanjani wakicheza mpira walichukua namba, kila mmoja alichukua namba moja. Namba hizo ziliwekwa kwenye kikapu kimoja na wale waliochukua namba moja hadi saba waliingia kwenye sampuli ya kundi rika la vijana.

Zoezi hili lilirudiwa kwenye kundi rika la watu wa kati, ambapo mtafiti aliandaa namba kuanzia moja hadi thelathini na tatu (1 - 33) kisha kila mmoja aliambiwa aokote namba moja tu. Wote waliokuwa uwanjani wakishangilia mchezo wa mpira walipata fursa ya kuokota namba hizo. Waliookota namba kuanzia moja hadi saba walichukuliwa kuwa sampuli katika kundi rika la watu wa kati. Kadhalika kwenye kundi la wazee, kama ambavyo imeelezwa walipatikana kupitia usampulishaji lengwa (makusudi). Kothari (ametajwa) na Haule (ametajwa) wanasema usampulishaji makusudi wa watafitiwa katika sampuli kwa kawaida huchaguliwa

kulingana na sifa zao kuhusiana na data ambazo mtafiti anazihitaji. Katika utafiti huu sampuli ya wazee saba (7) ilifikiwa kulingana na sifa zao. Sifa iliyotumika kubwa ni umri. Katika wazee thelathini na tatu (33) waliokuwa kwenye kundi lengwa la wazee waliochukuliwa ni wale ambao walikuwa na umri kuanzia miaka themanini (80) hadi mia (100). Katika kundi hili walipatikana wazee saba tu (7). Wakitokea katika vijiji saba vya eneo la utafiti ambalo mtafiti alilitembelea. Vijiji hivyo ni Komaswa, Kemakorere, Kibhumai, Nyarero, Nyamwaga, Sulubu na Bisarwi. Mtafiti alimfikia kila mmoja aliyekuwa na sifa alizozihitaji.

3.6 Data Zitakazokusanywa

3.6.1 Data za Msingi

Data za msingi ni data halisi. Kama anavyoeleza Mligo (2012) ni halisi kwa maana ya kwamba ni zile zinazokusanywa kwa mara ya kwanza na mtafiti ambazo hazikukusanywa na mtu mwingine kwa mara ya kwanza. Katika utafiti wetu data za msingi zilikusanywa maskanini ambazo zilionesha athari za matamshi, mofolojia na tahajia kutoka lugha ya Kikurya kwenda lugha Kiswahili. Berg (2007) anasema maskanini ni mahali ambapo watu wanaishi na ambapo mtafiti anakwenda kutafuta data ambazo ni mpya, halisi, ghafi na ambazo hazijawahi kukusanywa na mtu mwingine yeyote kwa ajili ya utafiti wake. Mtafiti alidhamiria kukusanya data halisi kwa sababu zilimsaidia kupata matokeo halisi (ukweli wa jambo ulivyo kwa sasa) kwa kuwa zilikuwa mpya na hazijawahi kutumika katika utafiti wowote hasa katika mada zinazoelekeana na utafiti huu. Pia aliona data hizi zilikuwa bora zaidi katika kumsaidia kufanikisha lengo la utafiti wake ukilinganisha na data zingine. Sababu kubwa ya kukusanya data mpya ni kutokana na ukweli kwamba katika eneo hilo la

utafiti huenda kuna mabadiliko yaliyotokea ambayo ukitumia data zingine kama vile data za upili unaweza usitimize kwa ufasaha lengo la utafiti wako kwani unaweza ukapata taarifa ambazo zimepitwa na wakati.

3.6.2 Data za Upili

Hizi ni data ambazo tayari zimekwisha kusanywa na watafiti tangulizi ambazo zinapatikana maktaba. Maktaba ni mahali maalum palipohifadhiwa nyaraka, vitabu, majarida na magazeti yenye taarifa mbalimbali kwa wasomaji na watafiti wa kada tofauti tofauti, Ewan na Calvert (2000). Ili kupata data za upili lazima mtafiti ahusike kusoma vitabu, tasnifu, majarida, makala na ikibidi kutafuta katika mtandao. Katika utafiti wetu data za upili zilibainika kupitia kazi mbalimbali ambazo mtafiti amezitumia kurejelea tarifa alizozihitaji, kwa mfano utafiti wa Otiende (ameshatajwa), Lusesa (ameshatajwa), Nyanda (ameshatajwa) zote zimeeleza namna lugha ya kwanza inayoathiri lugha ya pili yaani lugha Kiswahili. Mtafiti alinufaika kwa sababu zilikuwa ni sehemu ya mwongozo katika utafiti wake. Hasa akijiridhisha kama suala lililo katika utafiti lilishafanyiwa utafiti au bado.

3.7 Mbinu za Kukusanyia Data

Ukusanyaji wa data ni shughuli muhimu sana katika utafiti wowote. Kombo na Tromp (2006) wanaeleza ukusanyaji wa data ni zoezi la awali katika utafiti ambalo humwezesha mtafiti kupata taarifa alizokusudia ili kumfikisha kwenye malengo ya utafiti. Anaendelea kueleza kuwa hatua ya uwasilishaji na uchanguzi wa data haiwezi kufanyika kabla ya hatua hii ya ukusanyaji data. Hivyo ni mhimu kuhakiki mbinu za utafiti zinazotoa aina ya taarifa zinazohitajika kujibu swali la utafiti. Mtafiti

atahitajika kuwa na ala madhubuti ili kuifaulisha shughuli ya ukusanyaji data. Katika utafiti huu tulikuwa na mbinu za kukusanyia data za msingi na data za upili. Mbinu za kukusanyia data za msingi zilizotumiwa na mtafiti ni hojaji, mahojiano pamoja na kushiriki, yaani ushirikishwaji. Data za upili zilikusanywa kwa kusoma vitabu, tasnifu, makala mbalimbali pamoja na maandishi yote yanayofanana ama kuelekeana na mada ya utafiti.

3.7.1 Hojaji

Goods na Hatt (1952) wanasema hojaji ni seti ya maswali yaliyoandikwa au kauli zinazohusiana na suala linalotafitiwa ambayo mtafiti hutoa kwa wasailiwa kwa minajili ya kuibua habari, majibu, maoni, mitazamo na mikabala mahususi kuhusu mada ya utafiti. Kothari (1990) anaeleza kuwa hojaji kuwa ni mbinu ya utafiti ambayo kwayo mtafiti huandaa maswali kuhusiana na jambo Fulani. Maswali hayo yanaweza kuhitaji majibu marefu ama mafupi kutegemeana na taarifa inayohitajika na mtu anayepewa maswali hayo. Hojaji hujumuisha maswali yaliyotungwa kwa njia maalum ili kutolewa kwa sampuli ya wasailiwa waliolengwa katika utafiti fulani. Maswali haya yanafungamana na malengo ya utafiti. Williman (2010) anayafafanua maswali ya hojaji kuwa yapo ya aina mbili. Aina ya kwanza ni yale yanayohusisha maswali funge ambayo hutoa nafasi kwa watafitiwa kuchagua jibu miongoni mwa orodha ya majibu aliyopewa. Aina ya pili ya maswali ni yale yanayohusisha maswali yasiyo funge yaani maswali wazi. Haya hutoa fursa kwa watafitiwa kuwa huru kueleza wanachokijua kuhusu jambo waliloulizwa. Katika utafiti huu aina zote za hojaji zilitumika katika kukusanya data ambazo zilijibu swali

la pili la utafiti huu na watafitiwa wote ishirini na moja walihojiwa. Mbinu hii ilimfaa mtafiti kwa sababu alipata data kwa watu wengi na kwa muda mfupi.

3.7.2 Mahojiano

Mahojiano yameelezwa na Kombo na Tromp (2006) kuwa ni majibizano ya ana kwa ana, ya simu, barua pepe yanayofanyika kati ya watu wawili au zaidi kwa lengo la kukusanya taarifa au maoni kuhusu suala fulani la utafiti lililoainishwa. Njia hii huwasilishwa kwa mdomo baina ya mtafiti na mtafitiwa. Katika utafiti huu mahojiano yalitumika katika kukusanyia data za kipengele cha matashi ambapo makundi yote matatu yalishiriki mahojiano. Njia hii ilionekana kuwa bora kwa mtafiti kwa sababu iliwahusisha watu wote wanaojua kusoma na wasiojua kusoma. Pili, ilimruhusu mtafiti kuuliza ufafanuzi wa majibu yasiyoeleweka. Tatu, humpatia mtafiti uhakika kwamba walengwa wake ndio waliojibu maswali.

3.7.3 Usomaji wa Nyaraka Maktabani

Katika maktaba ndipo tunapata nyaraka, vitabu, makala pamoja na tasnifu mbalimbali. Kutokana na usomaji wa kazi mbalimbali mtafiti alinufaika kwa kupata maarifa zaidi ambayo yalimsaidia kupanua uelewa wake hususani zile kazi zilizoelekeana na mada aliyokuwa anaitafiti.

3.8 Uchambuzi wa Data

Uchambuzi wa data umeelezwa na Babbie (1999), Kothari (2008) kuwa ni kitendo cha kufupisha na kupangilia vizuri data zilizokusanywa kwa namna ambayo zitasaidia kujibu maswali ya utafiti husika. Data katika utafiti huchambuliwa kwa

kutumia mikabala ya aina mbili. Mkabala wa kimaelezo na mkabala wa kimahesabu. Mkabala wa kimaelezo umeelezwa na Enon (1998) na Kress (2008) kuwa ni mbinu ya kuchambua na kufafanua data ambapo mtafiti hueleza na kubainisha data zake kwa kutumia maelezo.

Mkabala wa kimahesabu ni mbinu ya uchambuzi na ufafanuzi wa data kwa kutumia namba ili kurekodi taarifa na kuwasilisha kwa kutumia mbinu za takwimu, maelezo haya ni ya williman (ameshatajwa). Katika utafiti huu, mtafiti alitumia mkabala wa maelezo katika kuwasilisha data zake kwa sababu hauna mambo mengi changamano, hulenga uchambuzi wa data jinsi zilivyo pasipo kubadili. Vilevile ni mkabala pekee ambao mara nyingi uhusishwa katika tafiti mbalimbali zinazozungumzia lugha. Hata hivyo, ikiwa kuna ulazima wa mtafiti kutumia mkabala wa kimahesabu, basi, atautumia.

3.9 Hitimisho

Katika sura hii tumejadili na kufafanua mbinu za utafiti kwa kuhusianisha na muundo wa utafiti, sampuli na usampulishaji, kadhalika ukusanyaji wa data pamoja na uchambuzi wa data.

SURA YA NNE

4.0 UWASILISHAJI, UCHAMBUZI NA MJADALA WA DATA

4.1 Utangulizi

Sehemu hii iliwasilisha data zilizokusanywa, kuchambuliwa na kujadiliwa kuhusiana na zoezi zima la utafiti. Kama alivyoeleza Mbweza (2006) kuwa, uwasilishaji, uchambuzi na mjadala wa data ni jumla ya shughuli na taratibu zote ambazo mtafiti hufanya ili kufikia uamuzi na matokeo fulani kutokana na data hiyo. Lengo kuu la utafiti, kama lilivyoelezwa kwenye kipengele cha malengo ya utafiti ni kuchunguza athari za Kikurya katika ujifunzaji Kiswahili sanifu miongoni mwa Wakurya. Ili kufikia adhima ya lengo hili, mtafiti katika kukusanya data za utafiti alijikita zaidi kwenye maswali makuu mawili ya utafiti ambayo ni; kwanza, “Jinsi gani maneno ya lugha ya Kikurya yanaathiri ujifunzaji wa Kiswahili sanifu”, na pili, “Ni sababu zipi zinachangia lugha ya Kikurya kuathiri ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili sanifu”.

4.2 Jinsi Maneno ya Lugha ya Kikurya Yanavyoathiri Ujifunzaji wa Kiswahili Sanifu

Katika kipengele cha 2.3 cha mapitio mbalimbali kuhusiana na mada ya utafiti, tuliona kuwa kila lugha imesheheni utamaduni wa jamii husika. Hii imedhihirishwa na tafiti mbalimbali zilizokwisha fanyika ambazo zaidi zilizungumzia uhusiano uliopo kati ya utamaduni na lugha fulani, hasa katika suala la matamshi. Kwamba, ni vigumu utamaduni kufichika pale mzungumzaji wa lugha fulani anapozungumza lugha nyingine. Kwa vile Wakurya ni kati ya jamii ambazo zina utamaduni, desturi

pamoja na mila, ndio maana mtafiti anajikita kuchunguza ni jinsi gani maneno ya lugha ya Kikurya yanaathiri ujifunzaji wa Kiswahili sanifu. Uchunguzi (utafiti) huu ulijikita katika vipengele vitatu vya; athari katika matamshi, athari katika mofolojia na athari katika tahajia.

4.2.1 Athari katika Matamshi (Fonolojia)

Katika taaluma ya fonolojia, neno matamshi lina maana moja tu, nayo ni ule utaratibu utumikao katika utoaji wa sauti za maneno ya lugha za binadamu. Yaani kama wanavyosema Habwe na Karanja (2004), Msanjila na wenzake (2011) ni namna mtu anatamka neno au jinsi mtu anavyozungumza lugha. Tazama mfano ufuatao hapo chini unavyoonesha.

1. Usiniretee maswara ya ubagusi wa kikabira [Wakurya]
2. Amemupiga mutoto ya watu juu amemuibia mafaranga makumi mawili [Wakongo]
3. Ukikaa nchale, ukichimama nchale [Wamakonde]
4. Wewe unakamuaga mang'ombe mangapi kwa siku? [Wasukuma]

Katika kutafiti athari za matamshi ya lugha ya Kikurya dhidi ya Kiswahili sanifu, mtafiti aliwatumia watafitiwa wote ishirini na moja (21). Ambapo kundi la wazee lilikuwa na watu 7, kundi la kati watu 7 na kundi la vijana watu 7. Makundi yote haya yalipewa kutamka maneno 15 ya Kiswahili. Lengo lilikuwa kuona kama wanaweza kuyatamka kwa ufasaha kama yanavyotamkwa katika lugha ya Kiswahili sanifu. Matokeo ya matamshi hayo ni kama yafuatavyo.

4.2.1.1 Kundi la Wazee

Katika kundi la Wazee ambalo lilikuwa na watu saba, waliohojiwa kutamka maneno kumi na tano (15) ya Kiswahili. Wote waliyakosea. Hivyo Walishindwa kwa asilimia mia moja (100%). Angalia jedwali namba moja (1)

Jedwali 4.1: Kundi la Wazee (Watu Saba) Maneno Yaliyotolewa Kutamkwa

| Na | Matamshi fasaha ya Kiswahili yaliyotolewa | Matamshi yasiyofasaha ya Kiswahili yaliyotamkwa na wazee | Sauti iliyokosewa kutamkwa |
|----|---|--|----------------------------|
| 1 | Jamvi | Shamvi | /sh/ |
| 2 | Kuoga | Kuogha | /h/ |
| 3 | Suruali | Suruari | /r/ |
| 4 | Soksi | Soghiksi | /ghi/ |
| 5 | Uji | Ushi | /sh/ |
| 6 | Kitana | Ghetana | /ghe/ |
| 7 | Mbuzi | Mbusi | /s/ |
| 8 | Sketi | Sigheti | /gh/ |
| 9 | Chumvi | Shumvi | /sh/ |
| 10 | Mboga | Mbogha | /gh/ |
| 11 | Msiba | Musibha | /bh/ |
| 12 | Tafadhali | Tavadhari | /va/ |
| 13 | Nibipu | Nibhipu | /h/ |
| 14 | Blankenti | Bhurankenti | /hur/ |
| 15 | Friji | Firishi | /sh/ |

Kulingana na data zilizo katika jedwali hili inaonyeshwa kuwa asilimia mia moja (100%) ya wazee waliohojiwa kutamka maneno kumi na tano (15) kwa lugha fasaha ya Kiswahili waliyakosea. Kwa mfano, hawakuweza kutamka silabi \$ Fri \$ kwa pamoja, isipokuwa walitenganisha silabi hiyo na kuongeza irabu /i/ na matokeo yake wakatengeneza silabi mbili tofauti ambazo ni \$ Fi \$ na \$ ri \$ pamoja na silabi \$ Shi\$ badala ya silabi \$ ji \$. Matamshi yaliyokosewa ni kutokana na athari za lugha mama.

4.2.1.2 Kundi la Kati

Katika kundi la watu wa kati ambao nao walipewa maneno kumi na tano (15) kama yale waliyopewa wazee ili kuyatamka, wao waliweza kutamka maneno matano kwa ufasaha, na walikosea kutamka maneno kumi (10) kwa ufasaha. Hii ina maana walishindwa kwa asilimia sitini na saba (67%), na walifaulu kutamka kwa ufasaha kwa asilimia thelathini na tatu (33%). Tazama jedwali namba mbili.

Jedwali 4.2: Kundi la Watu wa Kati (watu 7) Maneno Yaliyotolewa Kutamkwa

| Na | Matamshi fasaha ya Kiswahili yaliyotolewa | Matamshi yaliyokosewa kutamkwa na watu kundi la kati | Sauti iliyokosewa kutamkwa | Matamshi fasaha yaliyotamkwa |
|----|---|--|----------------------------|------------------------------|
| 1 | Jamvi | Shamvi | /sh/ | |
| 2 | Kuoga | ----- | ----- | Kuoga |
| 3 | Suruali | Suruari | /r/ | |
| 4 | Soksi | Soghiksi | /gh/ | |
| 5 | Uji | Ushi | /sh/ | |
| 6 | Kitana | ----- | ----- | Kitana |
| 7 | Mbuzi | Mbusi | /s/ | |
| 8 | Sketi | Sigheti | /gh/ | |
| 9 | Chumvi | ----- | ----- | Chumvi |
| 10 | Mboga | Mbogha | /gh/ | |
| 11 | Msiba | ----- | ----- | Msiba |
| 12 | Tafadhali | ----- | ----- | Tafadhali |
| 13 | Nibipu | Nibhipu | /h/ | |
| 14 | Blankenti | Bhurankenti | /hur/ | |
| 15 | Friji | Firishi | /sh/ | |

Kulingana na data zilizo katika jedwali hili inaonyeshwa kuwa asilimia sitini na saba (67%) ya maneno yaliyotolewa yalikosewa kutamkwa. Na, asilimia thelathini na tatu (33%) ya maneno yaliyotolewa yalitamkwa kwa ufasaha.

4.2.1.3 Kundi la Vijana

Katika kundi la vijana pia walipewa maneno kumi na tano (15) yale yale ya Kiswahili waliopewa makundi mengine ili wayatamke kama inavyotakiwa. Kati ya maneno hayo waliweza kutamka maneno saba (7) kwa ufasaha. Na walishindwa kutamka maneno nane (8) kiufasaha. Hivyo walishindwa kutamka maneno kwa ufasaha kwa asilimia hamsini na tatu (53%), na walifaulu kutamka kwa ufasaha kwa asilimia arobaini na saba (47%). Angalia jedwali namba tatu (3).

Jedwali 4.3: Kundi la Vijana (Watu 7) Maneno Yaliyotolewa Kutamkwa

| Na | Matamshi fasaha ya Kiswahili yaliyotolewa | Matamshi yalikosewa kutamkwa na kundi la vijana wenye elimu ya kawaida | Sauti iliyokosewa kutamkwa | Matamshi yaliyopatiwa kutamkwa |
|----|---|--|----------------------------|--------------------------------|
| 1 | Jamvi | Shamvi | /sh/ | |
| 2 | Kuoga | ----- | ----- | Kuoga |
| 3 | Suruali | Suruari | /r/ | |
| 4 | Soksi | ----- | ----- | Soksi |
| 5 | Uji | Ushi | /sh/ | |
| 6 | Kitana | ----- | ----- | Kitana |
| 7 | Mbuzi | Mbusi | /s/ | |
| 8 | Sketi | Sigheti | /gh/ | |
| 9 | Chumvi | ----- | ----- | Chumvi |
| 10 | Mboga | Mbogha | /gh/ | |
| 11 | Msiba | ----- | ----- | Msiba |
| 12 | Tafadhali | ----- | ----- | Tafadhali |
| 13 | Nibipu | Nibhipu | /h/ | |
| 14 | Blankenti | ----- | ----- | Brankenti |
| 15 | Friji | Frishi | /sh/ | |

Kulingana na data zilizo kwenye jedwali hili zinaonyesha kuwa kati ya maneno kumi na tano (15) ya Kiswahili yaliyotolewa kutamkwa, asilimia arobaini na saba (47%) ya maneno hayo yalitamkwa kwa ufasaha na asilimia hamsini na tatu (53) ya maneno hayo yalikosewa kutamkwa kwa ufasaha. Hivyo basi, kutokana na data

zilizowasilishwa hapo juu (jedwali namba 1 – 3) zinaonesha kwamba, kwa makundi yote matatu yenye jumla ya watu ishirini na moja (21) waliohojiwa, walikosea kutamka maneno ya Kiswahili fasaha waliyolizwa kwa asilimia sabini na moja (71%).

Miongoni mwa sauti zilizokosewa kutamkwa wakati wa utamkaji ni kama vile sauti /sha/ /gha/, /ri/, /shu/, /si/ ambazo zilipaswa kutamkwa kama sauti /ja/, /ga/. /li/, /chu/, /zi/. Hivyo basi, data zilizokusanywa na kujadiliwa kama zilivyo kwenye majedwali hapo juu, zinaonyesha wazi kuwa lugha ya Kikurya ina athari kubwa katika matamshi ya lugha ya Kiswahili sanifu. Matokeo ya utafiti huu yanaoana na kazi mbalimbali za watalamu waliozungumzia juu ya lugha ya kwanza kuathiri lugha ya pili hususani kipengele cha matamshi. Miongoni mwa watalamu hao ni pamoja na Roethlisber (1954) alisema lugha moja huathiri lugha nyingine kutokana na vikwazo vilivyopo kwenye mawasiliano kama vile tofauti katika uzoefu, motisha na maarifa ya nyuma waliyonayo watumiaji wa lugha. Alieleza kuwa wazungumzaji wote wa lugha wanaathiriwa na vikwazo – ndani ambavyo husababisha kuathiri lugha nyingine wakati wa ujifunzaji hasa katika matamshi na maandishi. Vikwazo – ndani husababisha kukiuka kanuni na taratibu za lugha ya pili (Kiswahili) Kama anavyoeleza Selinker (1969) kwenye utafiti wake.

Changamoto ya kutozingatia kanuni na misingi inayotawala lugha ya Kiswahili ndiyo iliyosababisha watumiaji wa lugha ya Kikurya kukosea wakati wa utamkaji. Wao walihamisha kanuni za lugha ya Kikurya walipokuwa wakizungumza lugha ya Kiswahili na hivyo kuiathiri lugha ya Kiswahili. Matokeo haya pia hayatofautiani na

alichokisema Otiende (ameshatajwa) katika utafiti wake. Yeye alionesha athari za lugha ya Kisoluba katika Kiswahili. Alieza kuwa, watumiaji wa lugha ya Kisoluba waliathiri lugha ya Kiswahili kwa sababu ya kuhamisha sauti za lugha yao ya kwanza na kuzipachika katika lugha ya pili (Kiswahili), sawia kabisa kama tulivyoona kwenye utafiti huu. Mifano ifuatayo ni matokeo ya utafiti wake akionesha lugha ya Kisoluba ilivyoathiri lugha ya Kiswahili.

Kisoluba (umbo lisilo sahihi)

Kiswahili (umbo sahihi)

Hasubui

[asubuhi]

Zambi

[ðambi]

Zarau

[ðarau]

Azuuri

[aðuhuri]

Kama inavyoonekana hapo juu, wazungumzaji wa lugha ya Kisoluba walichopeka sauti /h/ na kudondosha sauti /h/ kwenye baadhi ya maneno. Wanafanya hivyo kwa sababu hakuna fonimu /h/ katika lugha yao ya kwanza. Kadhalika fonimu /ð/ haipo katika lugha ya Kisoluba na hivyo hujikuta wakitamka sauti /z/ badala ya /ð/. Hivi ndivyo ilivyokuwa pia katika utafiti wetu.

Kwamba asilimia kubwa ya watafitiwa walitamka maneno kulingana na mfumo na taratibu za lugha yao ya kwanza. Kwa mfano, neno *Friji* katika makundi yote matatu lilikosewa kutamkwa na badala yake walitamka neno *frishi* kwa sababu hawakuweza kutamka silabi \$ Fri \$ kwa pamoja, isipokuwa walitenganisha silabi hiyo na kuongeza irabu /i/ na matokeo yake wakatengeneza silabi mbili tofauti ambazo ni \$ Fi \$ na \$ ri \$ pamoja na silabi \$ Shi\$ badala ya silabi \$ ji \$. Matamshi yaliyokosewa

ni kutokana na athari za lugha mama. Kama anavyosema Corder (ameshatajwa) kuwa athari katika lugha ya pili hutokana na mapokezi au kuhamisha sifa fulani za lugha ya kwanza na kuzileta katika lugha ya pili. Makosa hayo hujitokeza katika viwango vya mofolojia, sintaksia na fonolojia (kipengele cha matamshi tunachokianguka) kama anavyosema Onyango (1997), Ndung'u (1999) na Mutugu (2001). Kadhalika matokeo ya utafiti wetu yanaoana na kile alichokisema Athuman (ameshatajwa) kwenye kazi yake. Katika matokeo ya utafiti wake alionesha namna lugha ya Kiswahili ilivyoathiri lugha ya Kiyao. Anasema kuwa, lugha moja inapokuwa na watumiaji wengi ni rahisi kuathiri lugha nyingine ambayo matumizi yake siyo kwa kiasi kikubwa miongoni mwa jamii hiyo. Dai hili liliungwa mkono na Thomason (2001) aliyesema kuwa, athari za kiisimu kwa kawaida zinategemea athari za jamii lugha. Kwamba lugha ya jamii yenye nguvu kubwa ndiyo inayoathiri zaidi lugha ya jamii yenye nguvu ndogo kama ilivyokuwa katika utafiti huu. Jamii ya watumiaji wa lugha ya Kikurya ilikuwa na nguvu hata kuathiri lugha ya Kiswahili katika matamshi.

Halikadhalika matokeo ya utafiti huu yanakubaliana na matokeo ya utafiti alioufanya Nyanda (ameshatajwa) katika kazi yake. Akizungumzia kipengele cha matamshi, alionesha matumizi potofu ya sauti yalivyoathiri lugha ya Kiswahili sanifu. Anasema kuwa watumiaji wa lugha ya Kinyamwezi walichopeka sauti zisizo sahihi wakati wa utamkaji wa maneno ya Kiswahili na hivyo kuathiri matamshi ya lugha ya Kiswahili. Baadhi ya sauti walizochopeka wakati wa utamkaji ni pamoja na silabi *ga, ge, gi, go na gu*. Hivi ndivyo ilivyowatokea pia watumiaji wa lugha ya Kikurya kama tulivyoona kwenye kielelezo cha jedwali namba 1, 2, na 3. Kadhalika matokeo ya

utafiti huu yanakubaliana kabisa na utafiti alioufanya Massamba (1986) alipokuwa akichunguza athari za lugha mama (lugha za kienyeji) kwenye ujifunzaji wa lugha ya pili (Kiswahili). Aligundua kuwa lugha za kienyeji ziliathiri lugha ya Kiswahili kifonolojia, kimsamiati na kisarufi kama ilivyoonekana pia katika utafiti huu, ya kwamba watumiaji wa lugha ya Kikurya waliathiri lugha ya Kiswahili katika nyanja zote kama zilivyozotajwa hapo awali. Aidha matokeo ya utafiti huu yanakubaliana na matokeo ya Mukuthuria (2004), Ngugi (2007), Amen (2017) katika kazi zao. Walikubaliana kabisa kuwa athari za matamshi katika lugha ya pili maranyingi husababishwa na athari za lugha ya kwanza. Kwamba, wazungumzaji wengi hubadili (Tabadili) sauti na kutamka sauti zisizo sahihi ambazo husababisha athari za kimatamshi kwenye lugha ya pili (Kiswahili). Ukweli huu pia ulionekana kwa watumiaji wa lugha ya Kikurya ambao walibadilisha sauti katika matamshi yao na kutamka sauti ambayo haikupaswa kutamkwa mahali hapo katika lugha ya Kiswahili. Mfano ufuatao unaonesha athari za ubadilishaji wa sauti katika matamshi

| Kiswaili | Kikurya | Sauti Halisi | Sauti Iliyobadilishwa |
|-----------------|----------------|---------------------|------------------------------|
| Suruai | Suruari | /l/ | /r/ |
| Chumvi | Shumvi | /ch/ | /sh/ |
| Mbuz | Mbusi | /z/ | /s/ |

Mfano ulioneshwa hapo juu unadhihirisha kuwa lugha ya Kikurya ina ukosefu wa baadhi ya sauti kama vile /l/, /ch/, /z/, ambazo zilionekana kuwa ni changamoto wakati wa utamkaji. Richards (1974) anaeleza kuwa uzoefu alionao mtu wa kuzungumza katika lugha yake ya kwanza anapouhamishia kwenye lugha ya pili

(Kiswahili) husababisha makosa ya mtamshi katika lugha ya pili . Matokeo ya utafiti huu kadhalika yanaangazia kile kilichozungumzwa na Gaithuma (2016) katika kazi yake. Yeye alionesha namna lugha ya Kiswahili ilvyoathiriwa na lugha ya kwanza kwa kutumia lahaja ya Kiamu pamoja na Kitukuu. Alisema kuwa lugha ya Kiswahili imeathiriwa kwa kiasi kikubwa katika matamshi kutokana na uzoefu wa utamkaji wa lugha ya kwanza kuhamishia kwenye lugha ya pili kama tulivyoona kwa watumiaji wa lugha ya Kikurya. Mfano ufuatao unaonesha namna lugha ya Kiswahili ilivyoathirika katika matamshi na watumiaji wa lahaja ya Kiamu pamoja Kitukuu.

| Kiamu | | Kiswahili sanifu | |
|----------------|----------|-------------------------|-----------|
| Moya | [mɔja] | Moja | [mɔja] |
| Yua | [jua] | Jua | [Jua] |
| Pamoya | [pamɔja] | Pamoja | [pamɔja] |
| Mayani | [majani] | Majani | [maʃani] |
| Kitikuu | | Kiswahili sanifu | |
| Kadhi | [kaði] | Kazi | [kazi] |
| Ndhuri | [nðuri] | Nzuri | [nzuri] |
| Mwedhi | [mweði] | Mwezi | [mwezi] |
| Matodhi | [matɔði] | Machozi | [matʃɔzi] |

Kutokana na matamshi yao, wazungumzaji hawa walijikuta wakitengeneza lugha ambayo si ya kwanza kwa maana ya lugha mama wala si lugha ya pili kwa maana ya Kiswahili na hivyo wakatengeneza lugha kati kama anavyoieleza Selinker (1972) ni lugha ambayo huzaliwa pale mtu anapokuwa akijifunza lugha ya pili (Kiswahili) ambayo iliathiri lugha ya Kiswahili sanifu kama tulivyoona mfano hapo juu. Kutokana na changamoto hizo ndio maana Massamba (2006) alikuja na swali ambalo aliuliza “Je Kiswahili hiki ni mwanzo wa kuibuka kwa lahaja katika maeneo mengine ya bara?” Changamoto hii ni kutokana na uchunguzi wake alioufanya mkoani Mara na kugundua kuwa lugha ya kwanza ina athari kubwa katika lugha ya

pili (Kiswahili). Alitumia matamshi ya lugha ya Kikurya kuonesha athari za lugha ya kwanza katika lugha ya pili

| Na | Matamshi kwa lugha ya Kikurya | Kiswahili sanifu |
|-----------|--------------------------------------|-------------------------|
| 1 | Nitakuup ^h iga | Nitakupiga sana |
| 2 | Viiba ^h aya | Vibaya sana |
| 3 | Nimekungooja | Nimekungoja sana |
| 4 | Amecheeka | Amecheka sana |

Kama inavyoonekana kwenye jedwali, mtafiti aligundua kuwa kwenye matamshi ya lugha ya Kikurya kuna urefushaji wa silabi kama inavyoonekana kwenye jedwali hapo juu. Urefu wa hizo silabi kwenye maneno ya Kiswahili sanifu ni kutokana na athari za lugha mama yaani wamefata kanuni na taratibu za lugha yao ya kwanza katika kutamka maneno ya lugha ya pili (Kiswahili), kama anavyoeleza Were (1994) kuwa wazungumzaji wanapojumlisha sheria na pia kuzihamisha kutoka lugha ya kwanza hadi lugha ya pili ambayo ni Kiswahili Sanifu hujikuta wakiathiri lugha hiyo katika nyanja mbalimbali. Jambo hili ndilo lililotokea kwa wazungumzaji hawa, kwamba walijumuisha sheria za lugha yao katika Kiswahili sanifu. Aligundua kuwa athari za matamshi katika lugha ya Kiswahili sanifu ni kutokana na ujumlishaji wa kanuni, taratibu na sheria za lugha ya kwanza katika lugha ya pili. Dai hili liliungwa mkono na Nickel (1972) katika Lange (1974), Valdman (1975), Lucius (1978) na Corder (1981) ambao kwa pamoja walionyesha makosa ya ujumlishaji wa sheria na kanuni za lugha ya kwanza katika lugha ya pili yanavyoweza kuathiri lugha ya pili katika viwango vyote vya lugha yaani fonolojia, mofolojia na hata sintaksia. Jambo hili lilionekana pia kwa watumiaji wa lugha ya Kikurya walipotumia lugha ya Kiswahili kama lugha yao ya pili. Walitumia kanuni za lugha ya kwanza katika kutamka maneno ya lugha ya pili (Kiswahili) na wakajikuta wakiathiri matamshi ya

lugha hiyo. Ukweli huu ulithibitika kupitia maneno waliyopewa kutamka kama ifuatavyo

| Kiswahili sanifu | Matamshi ya Kikurya | Sauti jumuishi |
|-------------------------|----------------------------|-----------------------|
| Jamvi | Shamvi | /sh/ |
| Sketi | Sigheti | /gh/ |
| Soksi | Soghiksi | /gh/ |
| Chumvi | Shumvi | /sh/ |
| Uji | Ushi | /sh/ |

Kadhalika matokeo ya utafiti huu yaligundua kuwa makosa ya kimatamshi yaliyofanywa na wazungumzaji wa lugha ya Kikurya katika lugha ya pili (Kiswahili) yalichangiwa kwa kiasi fulani na uhusiano wa mpangilio wa sauti (mfanano wa mfumo wa sauti) pamoja na muundo wa silabi kati ya lugha hizo (Kikurya na Kiswahili). Sauti hizo ni irabu na konsonanti. Ilionekana maneno mengi ya Kikurya na Kiswahili hayana silabi funge inayoishia na konsonanti badala yake maneno mengi katika lugha hizi huishia na irabu. Mfano (I, KI, KKI). Matokeo haya yanaoana na kile alichokieleza Wenceslaus (ameshatajwa) kwenye utafiti wake, kuwa asilimia kubwa ya watumiaji wa lugha ya kwanza huchanganya mpangilio wa sauti hususani katika lugha ya pili (Kiswahili) wanapokuwa wakizungumza na hivyo kuiathiri lugha ya Kiswahili. Katika kipengele hiki cha matamshi, mtafiti amefanikiwa kuonesha athari za lugha ya kwanza (Kikurya) kwa lugha ya pili Kiswahili kwa kuhusianisha na kazi mbalimbali za watalam kama tulivyoona hapo awali ambazo zimekubaliana na ukweli wa utafiti huu kuwa athari za lugha ya kwanza huchangia kuathiri lugha ya pili (Kiswahili) katika viwango tofauti tofauti vya lugha kama vile fonolojia, sintaksia, semantiki na mofoljia.

Hata hivyo, utafiti huu haukuangalia kipengele cha undondoshaji wa sauti kinavyoweza kuathiri matamshi ya Kiswahili sanifu. Hii ni kwa sababu maneno waliyopewa kutamka haikuonekana sauti iliyodondoshwa. Hali hii imeleta utofauti katika uchambuzi wa data kati ya utafiti huu na tafiti zingine. Watafiti kama Otiende (ameshatajwa), Massamba (ameshatajwa) Amen (ameshatajwa) pamoja na Nyagah (2016) katika kazi zao walionesha na kujadili udondoshaji wa baadhi ya sauti kwenye lugha ya pili (Kiswahili) jinsi unavyoweza kuathiri matamshi sahihi ya lugha ya Kiswahili. Kwa mfano Nyagah (ameshatajwa) alionesha udondoshaji wa sauti /m/ katika maneno yafuatayo:

Matamshi ya Kimeru

| | | |
|------------|--------------|---------|
| Kumraba | /kumraba/ | kitenzi |
| Balamwezi | /balamwezi/ | nomino |
| Matebezi | /matebezi/ | nomino |
| Nikakubuka | /nikakubuka/ | kitenzi |

Matamshi ya Kiswahili sanifu

| | |
|-------------|--------------|
| kumramba | /kumramba/ |
| mbalamwezi | /mbalamwez/i |
| matembezi | /matembezi/ |
| nikakumbuka | /nikakumbuka |

Kwa kuangalia mfano huu utagundua kuwa ni ukweli usiopingika kuwa Kiswahili kimeathiriwa katika matamshi yake na watumiaji wa lugha ya Kimeru. Mtafiti alieleza kuwa udondoshwaji wa /m/ katika lugha ya pili (Kiswahili) unaweza kuhusishwa na sababu tatu. Kwanza, fonimu /m/ haimo katika mfumo wa sauti za Kimeru. Pili, husababishwa na watumiaji kurahisisha miundo ya lugha lengwa kama mkakati wa mawasiliano. Tatu, ujumuishaji mno wa kanuni za lugha lengwa kwenye lugha kati kama anavyoeleza Selinker (ameshatajwa).

Kwa ujumla, tuliona awali jinsi tafiti mbalimbali zilivyoonyesha kwamba, lugha ina tabia ya kuathiri na kuathiriwa na lugha nyingine. Maathiriano hayo kwa kiasi kikubwa huikumba lugha iliyodhaifu kwa maana ya kwamba watumiaji wake ni wachache. Kwa kina utafiti huu umejadili na kuonesha mfanano uliopo na utofauti katika kazi husika na kazi za watafiti mbalimbali ambazo zinakubaliana na hoja hii ya lugha ya kwanza kuathiri lugha ya pili katika kipengele cha matamshi. Watalamu kama Masamba (ameshatajwa), Otiende (ameshatajwa) Lusesa (ameshatajwa) wote wanakubaliana na hoja hii kuwa lugha ya kwanza huathiri lugha ya pili. Kwa mfano, Lusesa alionyesha kuwa lugha ya Kisukuma iliathiri kwa kiasi kikubwa lugha ya Kiswahili Sanifu. King’ei na Kobia (wamesahatajwa), kama walivyochunguza kabila la Sheng walikubaliana na Lusesa (ameshatajwa) kuwa lugha ya kwanza huathiri sana Kiswahili sanifu. Jambo hili ndilo lililowatokea watafitiwa wazungumzaji wa lugha ya Kikurya katika kipengele hiki cha matamshi kama ilivyoonekana kwenye makundi yote matatu yaliyotafitiwa ambapo lugha ya Kiswahili iliathiriwa. Kutokana na data zilizowasilishwa hapo juu na kuchambuliwa kuhusiana na athari za matamshi (fonolojia) ya lugha ya Kikurya dhidi ya Kiswahili Sanifu, mtafiti anakubaliana kwa asilimia mia moja (100%) na tafiti zilizotangulia (kama zilivyochambuliwa hapo awali kwa kuhusianisha na kazi hii) kuwa lugha mama za makabila mbalimbali zina athari kubwa katika kutamka maneno ya Kiswahili kwa usanifu. Hivyo basi, uchambuzi huu unathibitisha bila wasiwasi ukweli wa swali la kwanza la utafiti huu kipengele cha 1.5:1 lililouliza “Jinsi gani maneno ya lugha ya Kikurya yanaathiri ujifunzaji wa Kiswahili sanifu?” Kwamba, ni kweli pasipo mashaka yoyote kuwa maneno ya lugha ya Kikurya yanaathiri

ujifunzaji wa Kiswahili sanifu kama uchambuzi wa data za utafiki katika kipengele hiki ulivyo dhihirisha.

4.2.2 Athari katika Mofolojia

Dhana ya mofolojia katika utanzu wa isimu hujishughulisha na uchanganuzi wa maumbo ya maneno au umbo la neno. Laufer (1997) anaeleza kuwa uchanganuzi huo lazima uzingatie sheria na kanuni ambazo huongoza katika kuyapanga maneno yake katika mfuatano unaokubalika yaani umbo halisi la neno lenye kuleta maana inayoeleweka. Kwa hiyo, mofolojia au isimu maumbo ni utanzu wa isimu ambao huchunguza, hupambanua na kuchanganua maumbo ya maneno. Maelezo haya yanatolewa na Matinde (ameshatajwa). Katika utafiti huu ilionekana kuwa watumiaji wa lugha ya Kikurya walishindwa kuandika baadhi ya darajia sahihi kwenye sentensi walizopewa na hivyo kuathiri mofolojia ya lugha ya Kiswahili. Sababu iliyochangia washindwe kuandika vyema ni athari ya lugha mama. Kama ambavyo anaeleza James (1998) kuwa mtu yeyote anaposhindwa kuelewa mfumo wa sauti wa lugha fulani ni rahisi kukosea pindi anapotamka au kuandika. Changamoto hii ndio iliyowapata watumiaji wa lugha ya Kikurya walipotumia lugha ya Kiswahili.

Ili kudhihirisha kilichosemwa hapo awali mtafiti aliamua kuchunguza namna ambavyo matamshi ya lugha ya Kikurya yanaweza kuathiri maumbo ya maneno ya Kiswahili Sanifu. Aliwashirikisha watafitiwa kumi na tano (15) kutunga sentensi (ambazo aliwatamkia kwa kila mtafitiwa kwa kuzingatia mtafitiwa namba moja hadi kumi na tano) zinazozingatia sheria na kanuni zinazoongoza uandishi katika lugha ya Kiswahili. Mtafiti aliamua kutumia watafitiwa kumi na tano (15) badala ya

watafitiwa ishirini na moja (21) kwa sababu aliona idadi hiyo ingefaa kumpatia data faafu. Kama anavyoeleza patton (ameshatajwa) kuwa hakuna sheria za idadi katika uteuzi wa sampuli watafitiwa, isipokuwa mtafiti kufikia sampuli kifu. Watafitiwa hao walipewa namba yaani mtafitiwa namba moja (1) hadi mtafitiwa namba kumi na tano (15) ambaye ni mtafitiwa wa mwisho katika kipengele hiki cha mofolojia.

Mtafitiwa namba moja (1)

Mtafitiwa namba moja alitamkiwa sentensi kumi na tano na mtafiti na kumtaka aziandike kwa kutumia lugha ya Kiswahili sanifu inayozingatia sarufi ya lugha husika. Jedwali lifuatalo linaonesha alivyoweza kuandika sentensi hizo.

Jedwali namba 5: Sentensi zilivyoandikwa na mtafitiwa namba moja (1)

| Na | Sentensi alizotamkiwa na mtafiti | Sentensi zivyoandikwa na mtafitiwa |
|----|---|--|
| 1 | Chacha, nenda ukarudishe ng'ombe | Chacha nenda ukarutishe ng'ombe |
| 2 | Nimekula lakini sina pahala pa kulala | Nimekurarakini sina bhahara bha kurara |
| 3 | Usiku ilinyesha mvua kubwa | Usiku ilinyesha mvua kubwa |
| 4 | Naomba kalamu moja | Naombako karamu moja |
| 5 | Jumapili tutaenda mnadani | Jumabhiri tutaenda mnatani |
| 6 | Mazao yameharibiwa na wadudu | Mazao yameharibiwa na wadudu |
| 7 | Huu mwaka kuna njaa hapa kijijini | Huu mwaka kuna njaa hapa kijijini |
| 8 | Peleka barua kwenye ofisi ya mtendaji | Bhereka barua kwenye ovisi ya mtendashi |
| 9 | Twende kushangilia mpira | Twende kushangiria mubhira |
| 10 | Mlango umeharibika kitasa | Murango umeharibhika ghitasa |
| 11 | Gari imeondoka hapa saa kumi na mbili asubuhi | Ghari imeondoka habha saa kumi na mbiri asubhuhi |
| 12 | Ngozi ya ng'ombe ina faida sana | Ngosi ya ngo'mbe ina faida sana. |
| 13 | Mwalimu ametuadhibu tuliochelewa kuhesabu namba | Mwalimu ametuadhibu tuliochelewa kuhesabu namba |
| 14 | Jana nilienda kuchota maji | Shana nirienda kuchota maji |
| 15 | Tunafuga mifugo mbalimbali | Tunafuga mifugo mbalimbali |

Kama inavyooneka katika jedwali hapo juu, mtafitiwa alifaulu kuandika sentensi tano (5) tu kati ya sentensi kumi na tano (15) alizopaswa kuziandika kwa usahihi. Hii ni sawa na asilimia 34% na alishindwa kuandika sentensi kumi (10) kati ya kumi na tano. Ambayo ni sawa na asilimia 66% kama inavyoonekana katika jedwali.

Mtafitiwa namba mbili (2)

Kadhalika mtafitiwa namba mbili (2) naye alitamkiwa sentensi kumi na tano na mtafiti na kumtaka aziandike kwa kufuata kanuni, taratibu, na sheria zinazoongoza katika matumizi ya Kiswahili sanifu. Jedwali lifuatalo linaonesha alivyoweza kuandika sentensi hizo.

Jedwali 4.4: Sentensi Zilivyoandikwa Na Mtafitiwa Namba Mbili

| Na | Sentensi alizotamkiwa na mtafiti | Sentensi zivyoandikwa na mtafitiwa |
|----|---|--|
| 1 | Chacha, nenda ukarudishe ng'ombe | Chacha nenda ukarutishe ng'ombe |
| 2 | Nimekula lakini sina pahala pa kulala | Nimekula lakini sina pahalala pakulala |
| 3 | Usiku ilinyesha mvua kubwa | Usiku ilinyesha mvua kubwa |
| 4 | Naomba kalamu moja | Naombako karamu moja bhabha |
| 5 | Jumapili tutaenda mnadani | Jumapili tutaenda mnadani |
| 6 | Mazao yameharibiwa na wadudu | Mazao yameharibiwa na wadudu |
| 7 | Huu mwaka kuna njaa hapa kijijini | Huu mwaka kuna njaa hapa kijijini |
| 8 | Peleka barua kwenye ofisi ya mtendaji | Bhereka barua kwenye ovisi ya mtendashi |
| 9 | Twende kushangilia mpira | Twende kushangilia mpira |
| 10 | Mlango umeharibika kitasa | Murango umeharibika ghitasa |
| 11 | Gari imeondoka hapa saa kumi na mbili asubuhi | Ghari imeondoka habha saa kumi na mbiri asubhuhi |
| 12 | Ngozi ya ng'ombe ina faida sana | Ngosi ya ngo'mbe ina faida sana. |
| 13 | Mwalimu ametuadhibu tuliochelewa kuhesabu namba | Mwalimu ametuadhibu tuliochelewa kuhesabu namba |
| 14 | Jana nilienda kuchota maji | Shana nirienda kushota maji |
| 15 | Tunafuga mifugo mbalimbali | Tunafuga mifugo mbalimbali |

Mtafitiwa namba mbili katika uandishi wake, alifanikiwa kuandika sentensi nane (8) kwa usahihi kati ya sentensi kumi na tano ambazo alipewa kuziandika. Idadi ya sentensi zilizo sahihi ni sawa na asilimia 53%. Hivyo alishindwa kuandika sentensi kwa usahihi kwa asilimia 47%

Mtafitiwa namba 3

Na mtafitiwa namba tatu (3) naye alitamkiwa sentensi kumi na tano na mtafiti na kumtaka aziandike kwa kufuata kanuni, taratibu, na sheria zinazoongoza katika matumizi ya Kiswahili sanifu. Jedwali lifuatalo linaonesha mtafitiwa alivyoweza kuandika sentensi hizo.

Jedwali 4.5: Sentensi Zilivyoandikwa Na Mtafitiwa Namba Tatu

| Na | Sentensi alizotamkiwa na mtafiti | Sentensi zivyoandikwa na mtafitiwa |
|----|---|---|
| 1 | Chacha, nenda ukarudishe ng'ombe | Chacha nenda ukarutishe ng'ombe |
| 2 | Nimekula lakini sina pahala pa kulala | Nimekula lakini sina pahala pakulala |
| 3 | Usiku ilinyesha mvua kubwa | Usiku ilinyesha mvua kubwa |
| 4 | Naomba kalamu moja | Naombako kalamu moja |
| 5 | Jumapili tutaenda mnadani | Jumapili tutaenda mnadani |
| 6 | Mazao yameharibiwa na wadudu | Mazao yameharibiwa na watutu |
| 7 | Huu mwaka kuna njaa hapa kijijini | Huu mwaka kuna njaa hapa kijijini |
| 8 | Peleka barua kwenye ofisi ya mtendaji | Bhereka barua kwenye ovisi ya mtendashi |
| 9 | Twende kushangilia mpira | Twende kushangilia mubhira |
| 10 | Mlango umeharibika kitasa | Murango umeharibhika ghitasa |
| 11 | Gari imeondoka hapa saa kumi na mbili asubuhi | Ghari imeondoka habha saa kumi na mbiri asubuhi |
| 12 | Ngozi ya ng'ombe inafaida sana | Ngosi ya ngo'mbe inafaida sana. |
| 13 | Mwalimu ametuadhibu tuliochelewa kuhesabu namba | Mwalimu ametuadhibu tuliochelewa kuhesabu namba |
| 14 | Jana nilienda kuchota maji | Shana nirienda kushota maji |
| 15 | Tunafuga mifugo mbalimbali | Tunafuga mifugo mbalimbali |

Naye mtafitiwa namba (3) hakuwa tofauti sana na watafitiwa waliotangulia kwa sababu ni sentensi sita tu (6) alizoziandika kwa ufasaha kati ya sentensi kumi na tano alizotamkiwa na mtafiti. Kwa hiyo aliweza kuandika sentensi sahihi kwa kiwango cha asilimia 40% na alishindwa kuandika sentensi tisa (9) kwa usahihi ambayo ni sawa na asilimia 60%.

Mtafitiwa namba 4

Hali kadhalika mtafitiwa namba nne alitamkiwa sentensi zilezile walizotamkiwa watafitiwa wenzake ili kuona kama ataweza kupanga viambishi vya maneno kwa kuzingatia mofolojia ya lugha ya Kiswahili. Jedwali lifuatalo linaonesha alivyoweza kuandika sentensi hizo.

Jedwali 4.6: Sentensi Zilivyoandikwa Na Mtafitiwa Namba Nne

| Na | Sentensi alizotamkiwa na mtafiti | Sentensi zivyoandikwa na mtafitiwa |
|----|---|--|
| 1 | Chacha, nenda ukarudishe ng'ombe | Chacha nenda ukarutishe ng'ombe |
| 2 | Nimekula lakini sina pahala pa kulala | Nimekula lakini sina pahalala pakulala |
| 3 | Usiku ilinyesha mvua kubwa | Usiku ilinyesha mvua kubwa |
| 4 | Naomba kalamu moja | Naombako karamu moja |
| 5 | Jumapili tutaenda mnadani | Jumapili tutaenda mnatani |
| 6 | Mazao yameharibiwa na wadudu | Mazao yameharibiwa na watutu |
| 7 | Huu mwaka kuna njaa hapa kijijini | Huu mwaka kuna njaa hapa kijijini |
| 8 | Peleka barua kwenye ofisi ya mtendaji | peleka barua kwenye ovisi ya mtendashi |
| 9 | Twende kushangilia mpira | Twende kushangilia mubhira |
| 10 | Mlango umeharibika kitasa | Murango umeharibhika ghitasa |
| 11 | Gari imeondoka hapa saa kumi na mbili asubuhi | Ghari imeondoka habha saa kumi na mbiri asubhuhi |
| 12 | Ngozi ya ng'ombe inafaida sana | Ngosi ya ngo'mbe inafaida sana. |
| 13 | Mwalimu ametuadhibu tuliochelewa kuhesabu namba | Mwalimu ametuadhibu tuliochelewa kuhesabu namba |
| 14 | Jana nilienda kuchota maji | Shana a nirienda kushota maji |
| 15 | Tunafuga mifugo mbalimbali | Tunafuga mifugo mbalimbali |

Katika jedwali tunaoneshwa kuwa ni sentensi sita tu (6) ambazo mtafitiwa ameweza kuziandika kwa ukamilifu (kuzingatia mofolojia) wake katika lugha ya Kiswahili na sentensi tisa (9) hakuweza kuziandika vyema. Kwa hiyo aliweza kuandika sentensi sahihi kwa asilimia 40% na alishindwa kwa asilima 60%

Mtafitiwa namba 5

Halikadhalika mtafitiwa namba tano alipewa sentensi zilizile ili aweze kuziandika katika lugha ya Kiswahili fasaha kwa kuzingatia mofolojia ya kila neno. Matokeo ya kile alichokiandika yamewekwa katika jedwali lifuatalo

Jedwali 4. 7: Sentensi Zilivyoandikwa Na Mtafitiwa Namba Tano

| Na | Sentensi alizotamkiwa na mtafiti | Sentensi zivyoandikwa na mtafitiwa |
|----|---|--|
| 1 | Chacha, nenda ukarudishe ng'ombe | Chacha nenda ukarudishe ng'ombe |
| 2 | Nimekula lakini sina pahala pa kulala | Nimekula lakini sina pahala pakulala |
| 3 | Usiku ilinyesha mvua kubwa | Usiku ilinyesha mvua kubwa |
| 4 | Naomba kalamu moja | Naombako karamu moja |
| 5 | Jumapili tutaenda mnadani | Jumapili tutaenda mnatani |
| 6 | Mazao yameharibiwa na wadudu | Mazao yameharibiwa na watutu |
| 7 | Huu mwaka kuna njaa hapa kijijini | Huu mwaka kuna njaa hapa kijijini |
| 8 | Peleka barua kwenye ofisi ya mtendaji | peleka barua kwenye ovisi ya mtendashi |
| 9 | Twende kushangilia mpira | Twende kushangilia mubhira |
| 10 | Mlango umeharibika kitasa | Murango umeharibhika ghitasa |
| 11 | Gari imeondoka hapa saa kumi na mbili asubuhi | Ghari imeondoka habha saa kumi na mbiri asubhuhi |
| 12 | Ngozi ya ng'ombe inafaida sana | Ngosi ya ngo'mbe inafaida sana. |
| 13 | Mwalimu ametuadhibu tuliochelewa kuhesabu namba | Mwalimu ametuadhibu turiochelewa kuhesabu namba |
| 14 | Jana nilienda kuchota maji | Jana nilienda kushota maji |
| 15 | Tunafuga mifugo mbalimbali | Tunafuga mifugo mbalimbali |

Mtafitiwa namba (5) naye hakuwa tofauti sana na watafitiwa waliotanguli kwa sababu ni sentensi saba tu (7) alizoziandika kwa ufasaha kwa kuzingatia mofolojia ya

kila neno kati ya sentensi kumi na tano alizotamkiwa na mtafiti. Kwa hiyo aliweza kuandika sentensi sahihi kwa kiwango cha asilimia 46% na alishindwa kuandika sentensi nane (8) kwa usahihi ambayo ni sawa na asilimia 54%

Mtafitiwa namba (6)

Hali kadhalika mtafitiwa namba sita alitamkiwa sentensi zilezile walizotamkiwa watafitiwa wenzake ili kuona kama ataweza kupanga viambishi vya maneno kwa kuzingatia mofolojia yaa lugha ya Kiswahili. Jedwali lifuatalo linaonesha alivyoweza kuandika sentensi hizo.

Jedwali 4.8: Sentensi Zilivyoandikwa na Mtafitiwa Namba Sita

| Na | Sentensi alizotamkiwa na mtafiti | Sentensi zivyoandikwa na mtafitiwa |
|----|---|---|
| 1 | Chacha, nenda ukarudishe ng'ombe | Chacha nenda ukarudishe ng'ombe |
| 2 | Nimekula lakini sina pahala pa kulala | Nimekula lakini sina pahalala pakulala |
| 3 | Usiku ilinyesha mvua kubwa | Usiku irinyesha mvua kubwa |
| 4 | Naomba kalamu moja | Naombako karamu moja bhabha |
| 5 | Jumapili tutaenda mnadani | Jumapili tutaenda mnatani |
| 6 | Mazao yameharibiwa na wadudu | Masao yameharibiwa na watutu |
| 7 | Huu mwaka kuna njaa hapa kijijini | Huu mwaka kuna njaa hapa kijijini |
| 8 | Peleka barua kwenye ofisi ya mtendaji | peleka barua kwenye ovisi ya mtendashi |
| 9 | Twende kushangilia mpira | Twende kushangilia mubhira |
| 10 | Mlango umeharibika kitasa | Murango umeharibhika ghitasa |
| 11 | Gari imeondoka hapa saa kumi na mbili asubuhi | Ghari imeondoka habha saa kumi na mbiri asubhuhu |
| 12 | Ngozi ya ng'ombe inafaida sana | Ngosi ya ngo'mbe inafaida sana. |
| 13 | Mwalimu ametuadhibu tuliochelewa kuhesabu namba | Mwarimu ametuadhibu turiochelewa kuhesabu namba |
| 14 | Jana nilienda kuchota maji | Jana nirienda kuchota maji |
| 15 | Tunafuga mifugo mbalimbali | Tunafuga mifugho mbalimbali |

Kama inavyooneka katika jedwali hapo juu, mtafitiwa namba sita alifaulu kuandika sentensi tatu (3) tu kwa ufasaha kati ya sentensi kumi na tano (15) alizopaswa

kuziandika kwa usahihi. Hii ni sawa na asilimia 20% na alishindwa kuandika sentensi kwa asilimia 80% kama inavyoonekana kwenye jedwali.

Mtafitiwa namba 7

Pia mtafitiwa namba saba (7) naye alitamkiwa sentensi kumi na tano na mtafiti na kumtaka aziandike kwa kufuata mofolojia ya kila neno inavyopaswa kuandikwa kwa lugha ya Kiswahili. Jedwali lifuatalo linaonesha alivyoweza kuandika sentensi hizo

Jedwali 4.9: Sentensi Zilivyoandikwa na Mtafitiwa Namba Saba

| Na | Sentensi alizotamkiwa na mtafiti | Sentensi zivyoandikwa na mtafitiwa |
|----|---|---|
| 1 | Chacha, nenda ukarudishe ng'ombe | Chacha nenda ukarudishe ng'ombe |
| 2 | Nimekula lakini sina pahala pa kulala | Nimekula lakini sina pahalala pakulala |
| 3 | Usiku ilinyesha mvua kubwa | Usiku irinyesha mvua kubwa |
| 4 | Naomba kalamu moja | Naomb ako karamu moja |
| 5 | Jumapili tutaenda mnadani | Jumapili tutaenda mnadani |
| 6 | Mazao yameharibiwa na wadudu | Masao yameharibiwa na wat ut u |
| 7 | Huu mwaka kuna njaa hapa kijijini | Huu mwaka kuna njaa hapa k ish ishini |
| 8 | Peleka barua kwenye ofisi ya mtendaji | peleka barua kwenye o visi ya mtend ashi |
| 9 | Twende kushangilia mpira | Twende kushangilia m ub hira |
| 10 | Mlango umeharibika kitasa | Mur ango umeharib ika g hi itasa |
| 11 | Gari imeondoka hapa saa kumi na mbili asubuhi | G hari imeondoka hab ha saa kumi na mb iri asub hu hi |
| 12 | Ngozi ya ng'ombe inafaida sana | Ngos i ya ngo'mbe inafaida sana. |
| 13 | Mwalimu ametuadhibu tuliochelewa kuhesabu namba | Mwar im u ametuadhibu tur io chelewa kuhesabu namba |
| 14 | Jana nilienda kuchota maji | Jana n iri enda kuchota maji |
| 15 | Tunafuga mifugo mbalimbali | Tunafuga mifugo mbalimbali |

Kama inavyooneka katika jedwali hapo juu, mtafitiwa namba saba alifaulu kuandika sentensi nne (4) tu kwa ufasaha kati ya sentensi kumi na tano (15) alizopaswa

kuziandika kwa usahihi. Hii ni sawa na asilimia 26% na alishindwa kuandika sentensi kiufasaha kwa asilimia 74% kama inavyoonekana katika jedwali.

Mtafitiwa namba 8

Pia mtafitiwa namba nane (8) naye alitamkiwa sentensi kumi na tano na mtafiti na kumtaka aziandike kwa mofolojia sahihi ya lugha ya Kiswahili. Jedwali lifuatalo linaonesha alivyoandika sentensi hizo.

Jedwali 4. 10: Sentensi Zilivyoandikwa Na Mtafitiwa Namba Nane

| Na | Sentensi alizotamkiwa na mtafiti | Sentensi zivyoandikwa na mtafitiwa |
|----|---|--|
| 1 | Chacha, nenda ukarudishe ng'ombe | Chacha nenda ukarudishe ng'ombe |
| 2 | Nimekula lakini sina pahala pa kulala | Nimekura lakini sina pahalala pakulala |
| 3 | Usiku ilinyesha mvua kubwa | Usiku irinyesha mvua kubwa |
| 4 | Naomba kalamu moja | Naombakaramu moja |
| 5 | Jumapili tutaenda mnadani | Jumapili tutaenda mnadani |
| 6 | Mazao yameharibiwa na wadudu | Mazao yameharibiwa na watutu |
| 7 | Huu mwaka kuna njaa hapa kijijini | Huu mwaka kuna njaa hapa kishishini |
| 8 | Peleka barua kwenye ofisi ya mtendaji | peleka barua kwenye ovisi ya mtendashi |
| 9 | Twende kushangilia mpira | Twende kushangilia mubhira |
| 10 | Mlango umeharibika kitasa | Murango umeharibhika ghitasa |
| 11 | Gari imeondoka hapa saa kumi na mbili asubuhi | Ghari imeondoka habha saa kumi na mbiri asubhuhi |
| 12 | Ngozi ya ng'ombe inafaida sana | Ngosi ya ngo'mbe inafaida sana. |
| 13 | Mwalimu ametuadhibu tuliochelewa kuhesabu namba | Mwarimu ametuadhibu turiochelewa kuhesabu namba |
| 14 | Jana nilienda kuchota maji | Jana nirienda kushota maji |
| 15 | Tunafuga mifugo mbalimbali | Tunafuga mifugo mbalimbali |

Kama inavyoonekana katika jedwali hapo juu, mtafitiwa namba sita alifaulu kuandika sentensi tatu (3) tu kwa ufasaha kati ya sentensi kumi na tano (15) alizopaswa kuziandika kwa usahihi. Hii ni sawa na asilimia 20% na alishindwa kuandika sentensi kwa asilimia 80% kama inavyoonekana katika jedwali.

Mtafitiwa namba 9

Pia mtafitiwa namba saba (9) naye alitamkiwa sentensi kumi na tano na mtafiti na kumtaka aziandike kwa kufuata mofolojia ya kila neno inavyopaswa kuandikwa kwa lugha ya Kiswahili. Jedwali lifuatalo linaonesha mtafiwa alivyoweza kuandika sentensi hizo.

Jedwali 4.11: Sentensi Zilivyoandikwa Na Mtafitiwa Namba Tisa

| N a | Sentensi alizotamkiwa na mtafiti | Sentensi zivyoandikwa na mtafitiwa |
|----------------|---|--|
| 1 | Chacha, nenda ukarudishe ng'ombe | Chacha nenda ukarudishe ng'ombe |
| 2 | Nimekula lakini sina pahala pa kulala | Nimekura lakini sina pahalala pakulala |
| 3 | Usiku ilinyesha mvua kubwa | Usiku irinyesha mvua kubwa |
| 4 | Naomba kalamu moja | Naombako karamu moja |
| 5 | Jumapili tutaenda mnadani | Jumapili tutaenda mnadani |
| 6 | Mazao yameharibiwa na wadudu | Masao yameharibiwa na watutu |
| 7 | Huu mwaka kuna njaa hapa kijijini | Huu mwaka kuna njaa hapa kishishini |
| 8 | Peleka barua kwenye ofisi ya mtendaji | pereka barua kwenye ovisi ya mtendashi |
| 9 | Twende kushangilia mpira | Twende kushangilia mubhira |
| 10 | Mlango umeharibika kitasa | Murango umeharibika ghitasa |
| 11 | Gari imeondoka hapa saa kumi na mbili asubuhi | Ghari imeondoka habha saa kumi na mbiri asubuhi |
| 12 | Ngozi ya ng'ombe inafaida sana | Ngosi ya ngo'mbe inafaida sana. |
| 13 | Mwalimu ametuadhibu tuliochelewa kuhesabu namba | Mwarimu ametuadhibu turiochelewa kuhesabu namba |
| 14 | Jana nilienda kuchota maji | Jana nirienda kuchota maji |
| 15 | Tunafuga mifugo mbalimbali | Tunafuga mifugo mbalimbali |

Kama inavyooneka katika jedwali hapo juu, mtafitiwa namba tisa naye alifaulu kuandika sentensi tatu (3) tu kwa ufasaha kati ya sentensi kumi na tano (15) alizopaswa kuziandika kwa usahihi. Hii ni sawa na asilimia 20% na alishindwa kuandika sentensi kwa asilimia 80%.

Mtafitiwa namba (10)

Kadhalika mtafitiwa namba saba (10) naye alitamkiwa sentensi kumi na tano na mtafiti na kumtaka aziandike kwa kufuata mofolojia ya kila neno inavyopaswa kuandikwa kwa lugha ya Kiswahili. Jedwali lifuatalo linaonesha mtafiwa alivyoweza kuandika sentensi hizo.

Jedwali 4.12: Sentensi Zilivyoandikwa Na Mtafitiwa Namba Kumi

| Na | Sentensi alizotamkiwa na mtafiti | Sentensi zivyoandikwa na mtafitiwa |
|----|---|---|
| 1 | Chacha, nenda ukarudishe ng'ombe | Chacha nenta ukarudishe ng'ombe |
| 2 | Nimekula lakini sina pahala pa kulala | Nimekura lakini sina pahalala pakulala |
| 3 | Usiku ilinyesha mvua kubwa | Usiku irinyesha mvua kubwa |
| 4 | Naomba kalamu moja | Naombako karamu moja bhabha |
| 5 | Jumapili tutaenda mnadani | Jumapili tutaenda mnatani |
| 6 | Mazao yameharibiwa na wadudu | Masao yameharibiwa na wadudu |
| 7 | Huu mwaka kuna njaa hapa kijijini | Huu mwaka kuna njaa hapa kishishini |
| 8 | Peleka barua kwenye ofisi ya mtendaji | peleka barua kwenye ofisi ya mtendaji |
| 9 | Twende kushangilia mpira | Twende kushangilia mubhira |
| 10 | Mlango umeharibika kitasa | Murango umeharibika ghitasa |
| 11 | Gari imeondoka hapa saa kumi na mbili asubuhi | Gari imeondoka hapa saa kumi na mbiri asubhui |
| 12 | Ngozi ya ng'ombe inafaida sana | Ngoziya ngo'mbe inafaida sana. |
| 13 | Mwalimu ametuadhibu tuliochelewa kuhesabu namba | Mwarimu ametuadhibu turiochelewa kuhesabu namba |
| 14 | Jana nilienda kuchota maji | Jana nirienda kushota maji |
| 15 | Tunafuga mifugo mbalimbali | Tunafuga mifugo mbalimbali |

Vilevile mtafitiwa namba kumi naye alifaulu kuandika sentensi nne (4) tu kwa ufasaha kati ya sentensi kumi na tano (15) alizopaswa kuziandika kwa usahihi. Hii ni sawa na asilimia 27% na alishindwa kuandika sentensi kwa asilimia 73% kama inavyoonekana katika jedwali.

Mtafitiwa namba (11)

Mtafitiwa namba kumi na moja naye alitamkiwa sentensi kumi na tano na mtafiti na kumtaka aziandike kwa mofolojia sahihi ya lugha ya Kiswahili. Jedwali lifuatalo linaonesha alivyoweza kuandika sentensi hizo.

Jedwali 4.13: Sentensi Zilivyoandikwa Na Mtafitiwa Namba Kumi Na Moja

| Na | Sentensi alizotamkiwa na mtafiti | Sentensi zivyoandikwa na mtafitiwa |
|----|---|---|
| 1 | Chacha, nenda ukarudishe ng'ombe | Chacha nenta ukarudishe ng'ombe |
| 2 | Nimekula lakini sina pahala pa kulala | Nimekura lakini sina pahalala pakulala |
| 3 | Usiku ilinyesha mvua kubwa | Usiku irinyesha mvua kubwa |
| 4 | Naomba kalamu moja | Naombako karamu moja |
| 5 | Jumapili tutaenda mnadani | Jumapili tutaenda mnatani |
| 6 | Mazao yameharibiwa na wadudu | Masao yameharibiwa na wadudu |
| 7 | Huu mwaka kuna njaa hapa kijijini | Huu mwaka kuna njaa hapa kijijini |
| 8 | Peleka barua kwenye ofisi ya mtendaji | peleka barua kwenye ofisi ya mtendaji |
| 9 | Twende kushangilia mpira | Twende kushangilia mpira |
| 10 | Mlango umeharibika kitasa | Murango umeharibhika ghitasa |
| 11 | Gari imeondoka hapa saa kumi na mbili asubuhi | Gari imeondoka hapa saa kumi na mbiri asubhui |
| 12 | Ngozi ya ng'ombe inafaida sana | Ngosiya ngo'mbe inafaida sana. |
| 13 | Mwalimu ametuadhibu tuliochelewa kuhesabu namba | Mwarimu ametuadhibu turiochelewa kuhesabu namba |
| 14 | Jana nilienda kuchota maji | Jana nilienda kushota maji |
| 15 | Tunafuga mifugo mbalimbali | Tunafuga mifugho mbalimbali |

Halikadhalika mtafitiwa namba kumi na moja naye alifaulu kuandika sentensi nne (4) tu kwa ufasaha kati ya sentensi kumi na tano (15) alizopaswa kuziandika kwa usahihi. Hii ni sawa na asilimia 27% na alishindwa kuandika sentensi kwa asilimia 73% kama inavyoonekana katika jedwali.

Mtafitiwa namba (12)

Kadhhalika mtafitiwa namba saba (12) naye alitamkiwa sentensi kumi na tano na mtafiti na kumtaka aziandike kwa kufuata mofolojia ya kila neno inavyopaswa kuandikwa kwa lugha ya Kiswahili. Jedwali lifuatalo linaonesha alivyoweza kuandika sentensi hizo

Jedwali 4.14: Sentensi Zilivyoandikwa Na Mtafitiwa Namba Kumi Na Mbili

| Na | Sentensi alizotamkiwa na mtafiti | Sentensi zivyoandikwa na mtafitiwa |
|----|---|---|
| 1 | Chacha, nenda ukarudishe ng'ombe | Chacha nenda ukarudishe ng'ombe |
| 2 | Nimekula lakini sina pahala pa kulala | Nimekula rakini sina pahalala pakurara |
| 3 | Usiku ilinyesha mvua kubwa | Usiku ilinyesha mfua kubwa |
| 4 | Naomba kalamu moja | Naomba karamu moja |
| 5 | Jumapili tutaenda mnadani | Jumapili tutaenda mnatani |
| 6 | Mazao yameharibiwa na wadudu | Masao yameharibiwa na wadudu |
| 7 | Huu mwaka kuna njaa hapa kijijini | Huu mwaka kuna njaa hapa kijijini |
| 8 | Peleka barua kwenye ofisi ya mtendaji | peleka barua kwenye ofisi ya mtendashi |
| 9 | Twende kushangilia mpira | Twende kushangilia mbhira |
| 10 | Mlango umeharibika kitasa | Murango umeharibhika ghitasa |
| 11 | Gari imeondoka hapa saa kumi na mbili asubuhi | Gari imeondoka hapa saa kumi na mbiri asubhui |
| 12 | Ngozi ya ng'ombe inafaida sana | Ngosiya ngo'mbe inafaida sana. |
| 13 | Mwalimu ametuadhibu tuliochelewa kuhesabu namba | Mwarimu ametuadhibu turiochelewa kuhesabu namba |
| 14 | Jana nilienda kuchota maji | Jana nilienda kuchota maji |
| 15 | Tunafuga mifugo mbalimbali | Tunafugha mifugo mbalimbali |

Aidha mtafitiwa namba kumi na mbili naye alifaulu kuandika sentensi nne (4) tu kwa ufasaha kati ya sentensi kumi na tano (15) alizopaswa kuziandika kwa usahihi. Hii ni sawa na asilimia 27% na alishindwa kuandika sentensi kwa asilimia 73% kama inavyoonekana katika jedwali.

Mtafitiwa namba (13)

Hata mtafitiwa namba kumi na tatu naye alitamkiwa sentensi kumi na tano na mtafiti na kumtaka aziandike kwa mofolojia sahihi wa lugha ya Kiswahili. Jedwali lifuatalo linaonesha alivyoweza kuandika sentensi hizo.

Jedwali 4.15: Sentensi Zilivyoandikwa Na Mtafitiwa Namba Kumi Na Tatu

| Na | Sentensi alizotamkiwa na mtafiti | Sentensi zivyoandikwa na mtafitiwa |
|----|---|---|
| 1 | Chacha, nenda ukarudishe ng'ombe | Chacha nenda ukarudishe ng'ombe |
| 2 | Nimekula lakini sina pahala pa kulala | Nimekula rakini sina pahalala pakurara |
| 3 | Usiku ilinyesha mvua kubwa | Usiku irinyesha mvua kuuuubwa |
| 4 | Naomba kalamu moja | Naombako karamu moja |
| 5 | Jumapili tutaenda mnadani | Jumapili tutaenda mnatani |
| 6 | Mazao yameharibiwa na wadudu | Masao yameharibiwa na wadudu |
| 7 | Huu mwaka kuna njaa hapa kijijini | Huu mwaka kuna njaa hapa kijijini |
| 8 | Peleka barua kwenye ofisi ya mtendaji | peleka barua kwenye ovisi ya mtendaji |
| 9 | Twende kushangilia mpira | Twende kushangiria mpira |
| 10 | Mlango umeharibika kitasa | Murango umeharibhika ghitasa |
| 11 | Gari imeondoka hapa saa kumi na mbili asubuhi | Gari imeondoka hapa saa kumi na mbiri asubhui |
| 12 | Ngozi ya ng'ombe inafaida sana | Ngosiya ngo'mbe inafaida sana. |
| 13 | Mwalimu ametuadhibu tuliochelewa kuhesabu namba | Mwarimu ametuadhibu turiochelewa kuhesabu namba |
| 14 | Jana nilienda kuchota maji | Jana nilienda kushota maji |
| 15 | Tunafuga mifugo mbalimbali | Tunafuga mifugho mbalimbali |

Aidha mtafitiwa namba kumi na tatu (13) naye alifaulu kuandika sentensi mbili (2) tu kwa ufasaha kati ya sentensi kumi na tano (15) alizopaswa kuziandika kwa usahihi. Hii ni sawa na asilimia 13% na alishindwa kuandika sentensi kwa asilimia 87%.

Mtafitiwa namba (14)

Katika kuchunguzwa kwake mtafitiwa namba kumi na nne (14) naye alitamkiwa sentensi kumi na tano na mtafiti na kumtaka aziandike kwa mofolojia sahihi ya lugha ya Kiswahili. Jedwali lifuatalo linaonesha mtafiwa alivyoweza kuandika sentensi hizo.

Jedwali 4.16: Sentensi Zilivyoandikwa Na Mtafitiwa Namba Kumi Na Nne

| Na | Sentensi alizotamkiwa na mtafiti | Sentensi zivyoandikwa na mtafitiwa |
|----|---|---|
| 1 | Chacha, nenda ukarudishe ng'ombe | Chacha nenda ukarudishe ng'ombe |
| 2 | Nimekula lakini sina pahalala pa kulala | Nimekula rakini sina pahalala pakurara |
| 3 | Usiku ilinyesha mvua kubwa | Usiku irinyesha mvua kubwa |
| 4 | Naomba kalamu moja | Naombako karamu moja |
| 5 | Jumapili tutaenda mnadani | Jumapili tutaenda mnatani |
| 6 | Mazao yameharibiwa na wadudu | Masao yameharibiwa na wadudu |
| 7 | Huu mwaka kuna njaa hapa kijijini | Huu mwaka kuna njaa hapa kijijini |
| 8 | Peleka barua kwenye ofisi ya mtendaji | peleka barua kwenye ovisi ya mtendaji |
| 9 | Twende kushangilia mpira | Twende kushangiria mpira |
| 10 | Mlango umeharibika kitasa | Murango umeharibika kitasa |
| 11 | Gari imeondoka hapa saa kumi na mbili asubuhi | Gari imeondoka hapa saa kumi na mbiri asubui |
| 12 | Ngozi ya ng'ombe inafaida sana | Ngosiya ngo'mbe inafaida sana. |
| 13 | Mwalimu ametuadhibu tuliochelewa kuhesabu namba | Mwarimu ametuadhibu turiochelewa kuhesabu namba |
| 14 | Jana nilienda kuchota maji | Jana nilienda kushota maji |
| 15 | Tunafuga mifugo mbalimbali | Tunafuga mifugo mbalimbali |

Aidha mtafitiwa namba kumi na nne naye alifaulu kuandika sentensi tatu (3) tu kwa ufasaha kati ya sentensi kumi na tano (15) alizopaswa kuziandika kwa usahihi. Hii ni sawa na asilimia 20% na alishindwa kuandika sentensi kwa asilimia 80% kama inavyoonekana kwenye jedwali.

Mtafitiwa namba (15)

Naye mtafitiwa namba kumi na tano ambaye ndio wa mwisho katika kipengele hiki cha athari kwa upande wa mofolojia alitamkiwa sentensi zilezile kumi na tano na mtafiti na kumtaka aziandike kwa kuzingatia mofolojia sahihi kwa kila neno kulingana na lugha ya Kiswahili. Jedwali lifuatalo linaonesha alivyoweza kuandika sentensi hizo

Jedwali 4.17: Sentensi Zilivyoandikwa Na Mtafitiwa Namba Kumi Na Tano

| Na | Sentensi alizotamkiwa na mtafiti | Sentensi zivyoandikwa na mtafitiwa |
|----|---|---|
| 1 | Chacha, nenda ukarudishe ng'ombe | Chacha nenda ukarudishe ng'ombe |
| 2 | Nimekula lakini sina pahalala pa kulala | Nimekula rakini sina pahalala pakurara |
| 3 | Usiku ilinyesha mvua kubwa | Usiku irinyesha mvua kubwa |
| 4 | Naomba kalamu moja | Naombako karamu moja |
| 5 | Jumapili tutaenda mnadani | Jumapili tutaenda mnadani |
| 6 | Mazao yameharibiwa na wadudu | Masao yameharibiwa na wadudu |
| 7 | Huu mwaka kuna njaa hapa kijijini | Huu mwaka kuna njaa hapa kijijini |
| 8 | Peleka barua kwenye ofisi ya mtendaji | peleka barua kwenye ovisi ya mtendaji |
| 9 | Twende kushangilia mpira | Twende kushangiria mpira |
| 10 | Mlango umeharibika kitasa | Murango umeharibika kitasa |
| 11 | Gari imeondoka hapa saa kumi na mbili asubuhi | Gari imeondoka hapa saa kumi na mbiri asubui |
| 12 | Ngozi ya ng'ombe inafaida sana | Ngosiya ngo'mbe inafaida sana. |
| 13 | Mwalimu ametuadhibu tuliochelewa kuhesabu namba | Mwarimu ametuadhibu turiochelewa kuhesabu namba |
| 14 | Jana nilienda kuchota maji | Jana nilienda kushota maji |
| 15 | Tunafuga mifugo mbalimbali | Tunafuga mifugo mbalimbali |

Mtafitiwa namba kumi na tano, yeye aliweza kuandika sentensi nne (4) tu kwa ufasaha kati ya sentensi kumi na tano (15) alizopaswa kuziandika kwa usahihi. Hii ni sawa na asilimia 27% na alishindwa kuandika kwa usahihi sentensi 11 sawa na asilimia 73%. Kutokana na data zilizokusanywa kwa watafitiwa kuanzia namba moja

hadi kumi na tano zinaonesha matokeo ya jumla kwa mfumo wa asilimia namna ambavyo watafitiwa wameweza kuandika sentensi kwa kuzingatia mofolojia sahihi ya kila neno na pia waliposhindwa kuandika kwa kufuata mofolojia inayokubalika katika lugha ya Kiswahili sanifu. Jedwali lifuatalo linaonesha matokeo ya jumla kama walivyoandika watafitiwa.

Jedwali 4.18: Matokeo ya Jumla ya Watafitiwa

| Watafitiwa | Mofolojia sahihi katika sentensi (%) | Mofolojia zisizo sahihi kwenye sentensi (%) |
|-------------------|---|--|
| 1 | 34 | 66 |
| 2 | 53 | 47 |
| 3 | 40 | 60 |
| 4 | 40 | 60 |
| 5 | 47 | 54 |
| 6 | 20 | 80 |
| 7 | 26 | 74 |
| 8 | 20 | 80 |
| 9 | 20 | 80 |
| 10 | 27 | 73 |
| 11 | 27 | 73 |
| 12 | 27 | 73 |
| 13 | 13 | 87 |
| 14 | 20 | 80 |
| 15 | 27 | 73 |
| Jumla | 441 | 1060 |

Kama inavyoonekana kwenye jedwali, ni matokeo ya jumla kwamba kati ya watafitiwa kumi na tano waliopewa kuandika sentensi kwa kuzingatia mofolojia sahihi ya lugha ya Kiswahili sanifu, walioweza kuandika kwa usahihi ilikuwa ni asilimia (29.4%) na walioshindwa kuandika kwa usahihi kwa kigezo cha mofolojia ilikuwa ni asilimia (70.6%) kama data zinavyoonesha. Data hizi za uandishi wa sentensi kwa makosa ya kimofolojia uliofanywa na watafitiwa, mtafiti anakubaliana na tafiti mbalimbali zilizotangulia ambazo zinadhihirisha kwamba katika kuandika

sentensi ni dhahiri kuwa baadhi ya maneno mwandishi anaweza kuongeza viambishi/vipashio ama akafanya tabadili, uchopekaji, udondoshaji au urefushaji wa baadhi ya sauti akiwa na maana ya kuisitiza jambo fulani. Mambo haya yanapotokea katika uandishi wa neno ama sentensi huathiri mofolojia halisi ya neno husika. Mfano, katika sentensi zilizotungwa, fonimu /li/, /ra/, /bha/, /sha/, /ghi/, /si/, /she/, /gha/, /sha/, /bhu/, /re/, /bhe/, /ko/, /ti/, /ri/, /bha/, hazikubaliki katika mfumo wa uandishi wa lugha ya Kiswahili sanifu kwani maumbo yake ni tofauti na mofolojia inayotumika na inayokubalika katika lugha ya Kiswahili sanifu. Hivyo basi, matokeo ya utafiti huu yanakubaliana na kazi za watalamu mbalimbali waliozungumzia athari za mofolojia ambazo kwa kiasi kikubwa hutokana na athari za lugha mama. Kwa mfano, matokeo ya utafiti wetu yanakubaliana na matokeo ya Haroon (1998), ambaye alionesha namna lugha ya Kiswahili ilivyoathirika kimofolojia kutokana na athari ya lugha ya Kigisu kama lugha ya kwanza. Aligundua kuwa Kigisu kiliathiri mpangilio wa maneno katika sentensi za Kiswahili kutokana na tofauti za kimofolojia kati ya lugha hizi mbili kama ilivyokuwa kwa watafitiwa wa utafiti huu. Walihamisha muundo wa nje wa kisintaksia wa lugha yao kwa lugha ya Kikurya kwenda kwenye lugha ya pili (Kiswahili) na kuathiri maumbo ya maneno ya Kiswahili sanifu. Hali hii ilikuwa chanzo cha makosa kwenye mpangilio wa maneno katika sentensi zilizotungwa na watafitiwa husika. Ukweli huu pia umeungwa mkono na Chepkwony (2011) katika utafiti wake alipokuwa akishughulikia matatizo ya kisarufi miongoni mwa wanafunzi wa Kipigis wanapojifunza Kiswahili sanifu. Mfano ufuatao unaonesha kile Chomsky anachokizungumza

Kiswahili sanifu**Wanafunzi walivyoandika**

Mwanafunzi mzuri

Mwanafunzi *n*zuri

Mwanafunzi mzuri

Mwanafunzi *m*azuri

Mwanafunzi mzuri

Mwanafunzi – zuri

Namna sentensi zilivyoandikwa zinaonesha kuwa wanafunzi walishindwa kufanya upatanisho wa nomino na kivumishi. Waliongeza viambishi (uchopekaji) na pia walidondosha baadhi ya herufi /m/, /ma/ katika tungo. Kwa hiyo waliandika sentensi hizo pasipo kuzingatia uamilifu wa mofolojia ya lugha ya Kiswahili na kuleta athari katika lugha ya Kiswahili. Imekuwa ni mazoea ya lugha ya kwanza kuathiri mofolojia ya lugha ya pili katika utumizi wa lugha ya pili. Kwa mfano, Obara (2014) alionesha wanafunzi wa Ekegusi walivyoshindwa kuandika sentensi kwa ufasaha kwa sababu ya kuhamisha kanuni za lugha ya kwanza wakati wa uandikaji wa sentensi kwenye lugha ya pili (Kiswahili) na hivyo kuathiri mofolojia ya lugha ya Kiswahili kama ilivyokuwa kwa watafitiwa wetu (rejea jedwali hapo juu) walikosea kwa asilimia 71% na hivyo wakajikuta wakiathiri maumbo ya maneno ya lugha ya Kiswahili. Mfano ufuatao unaonesha wanafunzi wa Ekegusi walivyokosea katika muundo wa sentensi pindi walipokuwa wakiandika.

Sentensi yenye makosa ya Kimofolojia

Ilifika siku ya kurudi nyumbani, nikaanza safari yangu saa kumi unusu nalipanda ndege.

Sentensi sahihi Kimofolojia

Ilifika siku ya kurudi nyumbani, nikaanza safari yangu saa kumi unusu, nikapanda ndege

Sentensi yenye makosa ya Kimofolojia Wavulana wasita walitokea ghafula

Sentensi sahihi Kimofolojia Wavulana sita walitokea ghafula

Kama data zinavyoonesha, sentensi zote zilikosewa. Hazikuandikwa katika mofolojia sahihi ya lugha ya Kiswahili. Wanafunzi walitumia kiambishi kiwakilishi cha nafsi ya kwanza vibaya, badala ya kiambishi “ni” wao wakatumia “na”. Sababu iliyochangia kosa hili ni ujumlishaji mno pamoja na kutolewa kanuni za lugha lengwa kama ilivyokuwa kwa watumiaji wa lugha ya Kikurya walipokuwa wakiandika sentensi walizopewa na mtafiti. Waliamisha kanuni za lugha ya kwanza na kuzilazimisha kwenye lugha ya pili ambayo ni Kiswahili. Aidha matokeo ya utafiti huu yalibaini kuwa athari za kimofolojia zimekuwepo kwa sababu ya watumiaji wa lugha chanzi kutozingatia sarufi ya lugha husika (Kiswahili). Kapinga (1983) anaeleza vizuri kuwa sarufi ni utaratibu wa kanuni ambazo humwezesha mtumiaji wa lugha kutunga tungo sahihi zinazoeleweka katika lugha mahususi. Katika utafiti wetu tuliona kuwa watumiaji wa lugha ya Kikurya walishindwa kutunga sentensi zinazoeleweka kwasababu ya kutozingatia mofolojia inayokubalika ya lugha ya Kiswahili. Kulingana na data zilivyoonesha walikosea kwa sababu ya athari za lugha mama. Kama alivyoeleza Albert na wenzake (1978), akinukuliwa na Baljit (1999) kuwa, lugha ambazo huwa na mofolojia pamoja miundo inayoshabihiana huweza kudhihirisha viwango vikubwa vya mwathiriano. Jambo hili ndilo lililowatokea watumiaji wa lugha ya Kikurya walipokuwa wakiandika sentensi kwa lugha ya Kiswahili. Sentensi zifuatazo zinaonesha makosa ya kimofolojia katika lugha ya Kiswahili

| Sentensi zilivyoandikwa na watafitiwa | Umbo la neno lililokosewa | umbo la neno sahihi |
|--|---------------------------|---------------------|
| a/ Ngosiya ngo'mbe inafaida sana. [ngo] + [si] | /s/ | /z/ |
| b/ Masao yameharibiwa na wadudu [ma] + [sa] + [o] | /s/ | /z/ |

Watafitiwa waliweka mofimu kimakosa mahali pa mofimu zingine. Mfano mofimu, [si] badala ya mofimu [zi], [sa] badala ya [za]. Makosa haya yanatokana na athari ya lugha ya kwanza.

Ukweli huu uliungwa mkono na Kisakwah (2014) katika kazi yake, ambayo ilichanganua makosa ya kimofolojia kwa kulinganisha sentensi sanifu za Kiswahili na sentensi za Kisuba. Kama matokeo ya utafiti huu yanavyoeleza, naye alionesha watafitiwa walivyoshindwa kuandika sentensi kwa kufuata sarufi ya lugha ya Kiswahili. Walishindwa kwa sababu ya athari za lugha ya kwanza. Sentensi zifuatazo zinathibitisha ukweli huo;

| | |
|----------------------|--|
| Sentensi iliyokosewa | Kichwa zote kitakatwa |
| Sentensi sahihi | Kichwa chote kitakatwa |
| Sentensi iliyokosewa | Shamba yote litalimwa |
| Sentensi sahihi | Shamba lote litalimwa |
| Sentensi iliyokosewa | Viti zote zitapanguswa na wanafunzi |
| Sentensi sahihi | Viti vyote vitapanguswa na wanafunzi |

Kama sentesi zinavyoonesha, watumiaji wa lugha ya Kisuba walishindwa kufanya upatanifu wa kisarufi kwenye ngeli za Kiswahili. Katika lugha ya Kisuba nomino shamba na Kichwa huainishwakatika ngeli moja ilihali katika lugha ya Kiswahili kila nomino huwa na ngeli yake. Tofauti hizo zilisababisha mofolojia ya lugha ya Kiswahili kuathirika wakati wa kuandika sentensi. Changamoto hii pia ilijitokeza kwenye kazi ya Ontieri (2010). Matokeo ya utafiti huu pia yaligundua kuwa makosa ya kimofolojia yametokana na kutokujua sheria au kaida za lugha husika. Katika utafiti huu, watafitiwa walitumia kaida za lugha yao ya kwanza katika uandishi wa sentensi kwa lugha ya pili (Kiswahili). Uandishi huo ulitengeneza mofolojia ambayo haikubaliki katika lugha ya Kiswahili. Kwa mfano, sentensi ifuatayo inaonesha walivyoandika kwa kufuata kaida za lugha ya kwanza

Sentensi yenye makosa

Naombako karamu moja

Naombako karamu moja

Sentensi sahihi

Naomba kalamu moja

Naomba kalamu moja

Watafitiwa walipewa sentensi moja kuandika (Naomba kalamu moja) lakini kila mtu aliandika sentensi hiyo tofauti na ile waliyopewa. Sentensi ya kwanza iliambikwa kiambishi [ko]. Kiambishi hiki kimeambikwa kwa makosa, mwandishi alitumia umilisi wa lugha yake wakati alipoandika sentensi. Kadhalika sentensi ya pili iliongezwa kiambishi [ko] ambacho katika lugha ya Kiswahili hakina maana yoyote na pia kimewekwa kwa sababu ya athari za lugha mama. Kwa hiyo uhamishaji wa sheria na kaida za lugha ya kwanza zilisababisha makosa ya kimofolojia kwenye lugha ya pili na hivyo kuathiri lugha ya Kiswahili.

Ukweli huu pia ulipata mashiko kutoka kwa Lengo (1995) katika utafiti wake ambao ulionesha makosa mengi ya kimofolojia yanayotokea kwenye sentensi chanzo chake ni kutokana na kutozingatia sheria, kanuni na taratibu zinazotawala lugha ya pili (Kiswahili). Maelezo haya yanaaksi kile alichokisema Ellis (1994) kwenye kazi yake ya kuwa upotofu wa mofolojia katika lugha ya pili (Kiswahili) mara nyingi huletwa na athari za lugha ya kwanza. Naye Filmore (1968) kama alivyonukuliwa na Aruba (ameshatajwa) anaungana na wenzake kwa kuonesha zaidi namna ambavyo lugha ya kwanza imeleta changamoto katika mofolojia ya lugha ya pili. Anasema katika kiwango cha sentensi mofolojia inapaswa kuzingatiwa ili kuweza kupata maana halisi ya neno. Kinachotakiwa kuzingatiwa ni dhana ya kisarufi itumikayo kuonyesha dhima ya maneno katika tungo ili kuepuka athari za kimofolojia katika lugha ya pili. Katika utafiti wetu wahusika wa lugha ya Kikurya walishindwa kutambua dhana ya uhusika katika sentensi na hivyo kusababisha athari katika mofolojia ya lugha ya Kiswahili. Hoja hii ilizidi kupata mashiko pia kwa Gouala (1991) ambaye alichunguza juu ya athari za lugha ya asili kwa lugha ya Kiingereza nchini Kongo. Alionesha kuwa wanafunzi wengi hukumbwa na matatizo katika matamshi (fonolojia) na mofolojia ya Kiingereza kwa sababu ya lugha zao za asili. Changamoto iliyowapata wanafunzi hawa inafanana na changamoto iliyowapata watafitiwa katika utafiti wetu, kwa kuwa hata wao walishindwa kutamka na kuandika kwa mofolojia sanifu ya lugha ya Kiswahili.

Matokeo ya utafiti huu pia hatofautiani na alichozungumza Aruba (2017) katika utafiti wake. Yeye anaunga mkono kile walichozungumza wenzake kwa kuonesha makosa ya mawasiliano ya mandishi katika lugha ya Kiswahili sanifu maranyingi

hutokana na athari za lugha mama. Kwenye kazi yake alionesha namna athari za lugha kwanza zilivyosababisha wanafunzi wa shule za upili kaunti ya Kakamega kushindwa kuandika sentensi kwa ufasaha katika insha walizopewa kutokana na kuathiriwa na lugha mama. Sentensi zifuatazo zinaonesha wanafunzi walivyoshindwa kuzingatia mofolojia ya lugha ya Kiswahili.

Baba *hendi* katika kuvua leo

Niposoma magazeti *silewe*

Mama *alikimbilia* wakati baba alimchapa kwa usalama

Ukitazama mfano yote hapo juu, utaona sentensi ya kwanza badala ya mwanafunzi kuandika **haendi** yeye aliandika *hendi* kwa kuwa alidondosha herufi /a/, kadhalika sentensi ya pili kuna udondoshaji wa herufi /e/ na pia tabadili /e/ badala ya /i/ kwenye neno *silewe* na sentensi ya tatu nayo inakasoro ya kurudia kiambishi /li/ katika neno *alikimbilia*. Hivyo wanafunzi walikosea kuandika sentensi katika mofolojia ya lugha ya Kiswahili kwa sababu ya kutozingatia kaida zinazotawala lugha hiyo kama ilivyokuwa kwa watafitiwa wa utafiti huu (watumiaji wa lugha ya Kikurya). Hali hii inashabihiana kabisa na anavyoeleza Cruse (1986) kuwa sentensi ni kipashio huru cha kimuundo ambacho kinasheheni fikra kamili. Kwa maana yake, tukilinganisha na sentensi zilizoandikwa na watafitiwa, zote hazijatoa maana kamili kwa sababu ya kutozingatia mofolojia ya lugha husika ya Kiswahili.

Sovu (2011) naye hakuwa mbali na matokeo ya utafiti huu katika kipendele cha kimofolojia. Alionesha athari za matamshi ya Kiha (lugha ya kwanza) katika

Kiswahili sanifu yanavyosababisha makosa ya kimuundo. Alitoa mfano kushadadia ukweli huo aliouzungumza katika sentensi zifuatazo.

**Sentensi zenye makosa ya kimofolojia (Kiha) Sentensi katika mofolojia ya
Kiswahili sanifu**

Juma amekwenda **mumpira**

Juma amekwenda mpirani

Rose ameweka chakula **musufuria**

Rose ameweka chakula kwenye sufuria

Salome weka maji **mumtungi**

Salome weka maji mtungini

Kama inavyoonekana hapo juu, sentensi zilizoandikwa na watumiaji wa lugha ya Kiha zilikuwa na makosa ya kimofolojia ukihusisha na mofolojia inayokubalika wa lugha ya Kiswahili. Walikosea kuandika sentensi hizi kwa sababu ya hali ya mazoea iliyowatawala kama ilivyoonekana kwa watafitiwa wa la lugha ya Kikurya katika utafiti huu. Yaani wakahamisha sheria na kaida za uzungumzaji wa lugha chanzi na kuhamishia katika maandishi kama inavyoonekana kwenye sentensi.

Kadhalika Mohamed (1984) katika kazi yake alionesha namna ambavyo maumbo ya maneno ya lugha ya Kiswahili sanifu yalivyoathiriwa na lugha za asili za maeneo tofauti. Akitoa mfano kwa watumiaji wa lahaja za Kipemba na Kiunguja namna ambavyo wamekuwa wanakosea kuandika kwa kutozingatia mofolojia ya lugha ya Kiswahili piautamkaji waowa maneno kwa kiasi kikubwa hauzingatii kanuni za fonolojia kwa kiasi kikubwa na hivyo kuiathiri lugha ya Kiswahili kama ambavyo ilionekana pia katika kazi ya Maganga (1997) iliyozungumzia mahusiano ya kimofonolojia ya lugha ya Kiswahili na baadhi ya lahaja kama Kimakunduchi,

Kitumbatu na Kipemba. Mtafiti aligundua kwamba maumbo ya maneno ya lugha ya Kiswahili yalikuwa yameathiriwa na watumiaji wa hizo lahaja ambazo walizitumia kama lugha zao za asili za maeneo waliokuwa wanaishi. Nabea (2009) naye anaunga mkono matokeo ya utafiti huu katika kazi yake ambayo alionesha namna lugha ya Kiswahili ilivyoathiriwa na lugha ya Kiingereza katika maumbo ya maneno na pia muundo. Anaeleza kuwa watu wenye uwezo wa kuzungumza lugha hizi hubadilisha msimbo wanapozungumza, na Kiingereza hutumika na leksia ya lugha za kienyeji na hivyo kuathiri mofolojia ya lugha ya Kiswahili. Katika utafiti wake pia alichunguza pia lugha ya Kimeru na kugundua kuwa watumiaji wa hiyo lugha wana tabia ya kukopa maneno ama kutoka kwa Kiswahili au Kiingereza na kuyaingiza katika muundo na mofolojia ya Kimeru. Mfano:

Bantrain (They trained me) train + Meru structure

Gatwaforcethilwe (We were forced) force + Meru structure

Nitwavamiilwe (We were attacked) Kiswahili + Meru structure

Mifano iliyo hapo juu inaonyesha kuwa Kimeru kimeathiriwa na Kiswahili na Kiingereza katika kiwango cha kimofolojia hivi kwamba pahali ambapo kuna pengo la msamiati, lugha hizi hujaza pengo hilo na kurahisisha mawasiliano kama ilivyokuwa kwa watumiaji wa lugha ya Kikurya kwenye lugha ya Kiswahili.

Ukimtazama Nyanda (ameshatajwa) naye anakubaliana na ukweli huu katika kazi yake kwa kusema, athari mbalimbali zinazojitokeza katika lugha ya Kiswahili huweza kusababishwa na lugha mama. Kwenye utafiti wake alionesha jinsi lugha ya Kinyamwezi inavyoweza kuathiri lugha ya Kiswahili pindi mtu anapojifunza.

katika utafiti huu waliotumika ni raia wa kawaida (wasio wanafunzi) ambao ni watumiaji wa lugha ya Kikurya kama lugha yao ya kwanza. Hata hivyo mwisho wa kazi zote za watalam hawa zinaonesha kwamba lugha ya kwanza ya mama inaathiri mofolojia katika lugha ya Kiswahili.

Kwa sababu hiyo, mtafiti anakubaliana kabisa na tafiti zilizotangulia kuwa makosa katika mofolojia mara nyingi hutokana na jinsi mwandishi alivyoathiriwa na lugha ya kwanza na kujikuta akihamisha kanuni za uandishi wa lugha ya kwanza kwenda lugha ya pili. Kwamba, hali hii ndio iliyowatokea watafitiwa wote kumi na tano (15) wa lugha ya Kikurya waliopewa kuandika senetensi. Yaani, walihamisha kanuni za uandishi wa lugha mama ya Kikurya kwenda katika lugha ya pili ambayo ni Kiswahili Sanifu. Aidha tatizo hili la kushindwa kuandika kwa kuzingatia mofolojia sahihi ya lugha husika yaani lugha ya Kiswahili linajitokeza vizuri zaidi katika kipengele cha athari za tahajia kama ifuatavyo.

4.2.3 Athari katika Tahajia

Tahajia (Orthografia) ni uwakilishaji wa sauti za herufi za maneno katika maandishi. Ujifunzaji wa tahajia yaani uandikaji wa maneno sawa sawa ni muhimu kwa sababu uwezo wa kuandika maneno kwa usahihi unamsaidia mtu kuweza kuepuka makosa ya kisarufi katika lugha. Tahajia inakuwa haina umuhimu wowote tunapozungumuza, lakini tunapoandika, tahajia huwa na umuhimu mkubwa kwa sababu ulimwengu wa leo umejaa maandishi. Sababu hii ndio iliyomsukuma mtafiti kuwataka watafitiwa kila mmoja kuandika kwani anaweza akatamka neno vyema

linavyopaswa kutamka lakini katika kuandika akashindwa kuzingatia othografia sahihi na hivyo kuiathiri lugha ya Kiswahili.

Kwa mfano, jumbe fupi za maandishi katika simu, barua pepe, majukwaa ya kijamii, na mitandao ya habari ya watu binafsi au vikundi, sehemu zote hizi zinatumia maandishi. Ikiwa mwandishi atatumia tahajia mbovu yaani uandikaji mbovu wa maneno unaweza ukamfanya msomaji awe na wasiwasi na uhalali wa yale anayoyasoma, kadhalika unaweza ukamfanya msomaji ahisi kwamba aliyeandika hamheshimu hususani pale ujumbe lengwa unapokuwa umekosewa. Kwa hiyo mtu anapokuwa amezingatia tahajia inamaanisha atakuwa amezingatia kaida zote za uandishi zinazokubalika katika misingi ya lugha hiyo.

Mfano mzuri ni sentensi zifuatazo hapa chini ambazo zina makosa ya kitahajia:

- i) “Mwenyekiti wa chama cha wananzego alihutubia kwa **khadhabu** kuhusu kutokuwa na umoja katika nzengo”.

Sehemu hiyo iliyokolezwa katika sentensi haikutamkwa kwa usahihi na matokeo yake imeandikwa isivyo sahihi. Tahajia sahihi hapa ni **ghadhabu**.

- ii) “Hata hivyo nchi hiyo imeweza kugeuka kuwa moja ya mataifa yanayoku**wa** kwa kasi kubwa barani Afrika”. Kadhalika sehemu iliyokolezwa katika sentensi hii haikuandikwa kwa usahihi. Tahajia sahihi ya neno hili ni **yanayokua**.

Makosa ya tahajia yameonekana kuwa na sehemu kubwa katika kuathiri lugha ya Kiswahili hususani upande wa maandishi. Watafiti wengi wanaonyesha kuwa

makosa haya yanayofanyika ya uandishi wa herufi ni kutokana na athari za lugha mama. Wanasema kuwa watoto wanaposhindwa kufundishwa na kuelekezwa kwa usahihi uandishi bora katika kipindi cha utotoni wanaweza wasimudu kuandika kwa usahihi. Mfano Selinker (1972) aligundua kuwa ni ukweli usiopingika kuwa lugha za asili zinaposemwa kwa muda mrefu na jamii mbali mbali ni rahisi kwa wanajamii hao kukosea lugha ya pili wanapokuwa wakitamka na kuandika.

Tafiti hizi katika kipengele hiki cha tahajia, ndizo zilizomsukuma mtafiti kuchunguza namna watumiaji wa lugha ya Kikurya walivyoweza kuathiri Kiswahili Sanifu hasa upande wa maandishi. Jumla ya watafitiwa tisa (9) kati ya watu ishirini na moja waliokuwa kwenye sampuli walichunguzwa. Watafitiwa hawa walipatikana kwa kuchaguliwa baadhi tu miongoni mwa wale ishirini na moja. Mtafiti aliwateua hawa kwa kuzingatia kile alichokisema Pattom (ameshatajwa) kuwa hakuna sheria za idadi katika uteuzi wa sampuli kwenye utafiti. Isipokuwa mtafiti aangalie sampuli itakayotosheleza kufikia lengo madhubuti alilokusudia. Watahiniwa wote tisa walitamkiwa na mtafiti maneno ya Kiswahili il kila mmoja aweze kuyaandika kadri alivyoweza. Maneno waliyotamkiwa ni Almasi, Magadi, Uzi, Mweupe, Rula, Shule, Chakula, Jembe na Mpira. Mtokeo ya uandishi wao ni kama anavyooneshwa kwenye majedwali zifuatazo.

Mtafitiwa namba moja (1)

Mtafitiwa katika kuandika maneno ya Kiswahili aliyotamkiwa na mtafiti aliweza kuyaandika kama inavyooneshwa kwenye jedwali namba kumi na tisa.

Jedwali 4.19: Tahajia Sahihi na Tahajia Iliyokosewa Na Mtafitiwa Namba 1

| Na | Tahajia sahihi | Tahajia (iliyokosewa na wazungumzaji)yenye makosa |
|----|----------------|---|
| 1 | Almasi | <i>Arimasi</i> |
| 2 | Magadi | <i>Maghadi</i> |
| 3 | Uzi | <i>Usi</i> |
| 4 | Mweupe | <i>Mweubhe</i> |
| 5 | Rula | <i>Rura</i> |
| 6 | Shule | <i>Shure</i> |
| 7 | Chakula | |
| 8 | Jembe | |
| 9 | Mpira | <i>Mbhira</i> |

Katika jedwali hili inaonyesha kuwa mtafitiwa alifanikiwa kuandika maneno mawili (2) tu. Ya “Chakula” na “debe” kwa usahihi kati ya maneno tisa (9) aliyotamkiwa na mtafiti kuyaandika. Maneno mengine yaliyobaki saba (7) alishindwa kuyaandika kwa usahihi. Hii ina maana kuwa alifaulu kuandika maneno aliyotamkiwa kwa usahihi kwa asilimia 23% na kushindwa kuandika ipasavyo kwa asilimia 77%.

Wilkins (ameshatajwa) alishawahi kusema katika utafiti wake kuwa athari katika tahajia mara nyingi hutokana na athari za lugha mama. Hivyo basi, mtafiti anakubaliana na Wilkins (ameshatajwa) kuwa ni dhahiri kwamba mtafitiwa alikosea kuandika maneno aliyotamkiwa kwa usahihi kwa asilimia 77% kwa sababu ya kuathiriwa na lugha yake ya asili ambayo ni Kikurya. Utafiti huu umethibitisha ukweli huu kwa asilimia mia (100%)

Mtafitiwa namba mbili (2)

Kadhalika mtafitiwa namba mbili naye alitamkiwa na mtafiti maneno yaleyale kuyandika ili kuona kama atafanikiwa kuandika katika tahajia inayokubalika.

Jedwali lifuatalo linaonesha namna alivyoandika

Jedwali 4.20: Tahajia Sahihi Na Tahajia Iliyokosewa Na Mtafitiwa Namba 2

| Namba | Tahajia sahihi | Tahajia yenye makossa |
|--------------|-----------------------|------------------------------|
| 1 | Almasi | <i>Arimasi</i> |
| 2 | Magadi | <i>Maghadi</i> |
| 3 | Uzi | Uzi |
| 4 | Mweupe | <i>Mweubhe</i> |
| 5 | Rula | Rula |
| 6 | Shule | <i>Shure</i> |
| 7 | Chakula | <i>Shakura</i> |
| 8 | Jembe | <i>Shembe</i> |
| 9 | Mpira | Mpira |

Kulingana na data katika Kama inavyoonekana kwenye jedwali mtafitiwa namba mbili alifanikiwa kuandika maneno matatu tu ya *mpira, Rula na Uzi* kwa usahihi ambayo ni sawa na asilimia 33%, alikosea kuandika maneno sita ambayo ni sawa na asilimia 67%. Hii ni dhahiri kuwa sababu iliyopelekea makosa katika tahajia hizo ni kuathiriwa na lugha yake ya kwanza (Kikurya). Kama ilivyoelezwa na Nyanda (ameshatajwa) katika utafiti wake kuwa makosa mengi ambayo hushamiri katika maandishi maranyingi hutokana na athari za lugha ya kwanza (mama). Na hivi ndivyo ilivyo kwenye matokeo ya utafiti huu.

Mtafitiwa namba tatu (3)

Na mtafitiwa namba tatu naye alipewa maneno yaleyale na mtafitiwa kuyandika ili kuona kama atafanikiwa kuandika katika tahajia inayokubalika. Jedwali lifuatalo linaonesha namna alivyoandika.

Jedwali 4.21: Tahajia Sahihi Na Tahajia Iliyokosewa Na Mtafitiwa Namba 3

| Namba | Tahajia sahihi | Tahajia yenye makossa |
|-------|----------------|-----------------------|
| 1 | Almasi | <i>Arimasi</i> |
| 2 | Magadi | <i>Maghadi</i> |
| 3 | Uzi | <i>Uzi</i> |
| 4 | Mweupe | <i>Mweupe</i> |
| 5 | Rula | <i>Rura</i> |
| 6 | Shule | <i>Shure</i> |
| 7 | Chakula | <i>Shakula</i> |
| 8 | Jembe | <i>Shembe</i> |
| 9 | Mpra | <i>Mpira</i> |

Kadhalika mtafitiwa namba tatu alifanikiwa kuandika maneno matatu tu kwa usahihi kati ya tisa aliyopewa na mtafiti kukuandika ambayo ni sawa 33% na alikosea kuandika maneno sita ambayo ni sawa na asilimia 67% kama inavyoonyeshwa kwenye jedwali. Hivyo mtafiti anadhihirisha kwa asilimia mia (100%) kuwa mtafitiwa huyu naye aliathiriwa na lugha ya mama (Kikurya) kama watafiti mbalimbali walivyoonesha kwenye kipengele cha 2.2 na 2.3 cha mapitio ya kazi tangulizi.

Mtafitiwa namba nne (4)

Kama ilivyokuwa kwa watafitiwa waliopita, mtafiti huyu naye alitamkiwa maneno yaleyale na mtafiti ili kuona kama atafanikiwa kuandika katika tahajia sahihi. Jedwali lifuatalo linaonesha namna mtafitiwa alivyoandika.

Kati ya maneno tisa aliyotamkiwa kuandika, mtafiti huyu alifanikiwa kuandika maneno mawili kwa tahajia inayokubalika katika lugha ya Kiswahili. Jedwali hapo juu linafafanua zaidi kwa kuonesha maneno hayo. Kwa hiyo alifaulu kuandika tahajia sahihi kwa kiwango cha asilimia 23% na alishindwa kwa kiwango cha

asilimia 77%. Kushindwa kwake kuandika maneno usahihi kunadhihirisha jinsi gani naye alivyoathiriwa na lugha ya kwanza (Mama) ya Kikurya.

Jedwali 4.22: Tahajia Sahihi Na Tahajia Iliyokosewa Na Mtafitiwa Namba 4

| Namba | Tahajia sahihi | Tahajia yenye makossa |
|--------------|-----------------------|------------------------------|
| 1 | Almasi | <i>Arimasi</i> |
| 2 | Magadi | <i>Maghadi</i> |
| 3 | Uzi | <i>Usi</i> |
| 4 | Mweupe | <i>Mweupe</i> |
| 5 | Rula | <i>Rura</i> |
| 6 | Shule | <i>Shure</i> |
| 7 | Chakula | <i>Shakula</i> |
| 8 | Jembe | <i>Jembe</i> |
| 9 | Mpira | <i>Mbhira</i> |

Mtafitiwa namba tano (5)

Mtafitiwa huyu naye hakuwa tofauti na waliopita kwani alipewa maneno yaleyale waliopewa wengine kuyaandika ili kuona kama ataweza kuandika kwa kuzingatia tahajia inayokubalika katika lugha ya Kiswahili sanifu. Matokeo ya alichokiandika yanaonekana kwenye jedwali lifuatalo.

Jedwali 4.23: Tahajia Sahihi Na Tahajia Iliyokosewa Na Tافitiwa Namba 5

| Namba | Tahajia sahihi | Tahajia yenye makossa |
|--------------|-----------------------|------------------------------|
| 1 | Almasi | <i>Arimashi</i> |
| 2 | Magadi | <i>Maghadi</i> |
| 3 | Uzi | <i>Usi</i> |
| 4 | Mweupe | <i>Mweubhe</i> |
| 5 | Rula | <i>Rura</i> |
| 6 | Shule | <i>Shure</i> |
| 7 | Chakula | <i>Chakula</i> |
| 8 | Jembe | <i>Jembe</i> |
| 9 | Mpira | <i>Mbhira</i> |

Kama inavyoonekana kwenye jedwali hapo juu, mtafitiwa alishindwa kuandika maneno saba kwa tahajia inayokubalika katika lugha ya Kiswahili sanifu ambayo ni sawa na asilimia 77%. kuandika maneno mawili kwa usahihi kama inavyoonekana kwenye jedwali, ambayo ni sawa na asilimia 23%.

Mtafitiwa namba sita (6)

Kama ilivyokuwa kwa watafitiwa waliopita, mtafitiwa huyu naye alitamkiwa maneno yaleyale na mtafiti ili kuona kama atafanikiwa kuandika katika tahajia sahihi. Jedwali lifuatalo linaonesha namna mtafitiwa alivyoandika.

Jedwali 4.24: Tahajia Sahihi Na Tahajia Iliyokosewa Na Mtafitiwa Namba 6

| Namba | Tahajia sahihi | Tahajia yenye makossa |
|--------------|-----------------------|------------------------------|
| 1 | Almasi | <i>Arimas</i> |
| 2 | Magadi | Magadi |
| 3 | Uzi | Uzi |
| 4 | Mweupe | Mweupe |
| 5 | Rula | Rura |
| 6 | Shule | Shure |
| 7 | Chakula | Chakula |
| 8 | Jembe | Jembe |
| 9 | Mpira | Mpira |

Kama jedwali linavyoonesha, mtafitiwa namba sita alifanikiwa kuandika maneno sita kwa tahajia sahihi inayokubalika katika lugha ya Kiswahili, na alishindwa kuandika maneno matatu kwa usahihi. Hivyo, aliweza kuandika kwa usahihi kwa asilimia 66% na alishindwa pia kuandika kwa usahihi kwa asilimia 34%

Mtafitiwa namba saba (7)

Kama ilivyokuwa kwa watafitiwa waliopita, naye alitamkiwa maneno yaleyale na mtafiti ili kuona kama atafanikiwa kuandika katika tahajia sahihi. Jedwali lifuatalo linaonesha namna mtafitiwa alivyoandika.

Jedwali 4.25: Tahajia Sahihi Na Tahajia Iliyokosewa Na Mtafitiwa Namba 7

| Namba | Tahajia sahihi | Tahajia yenye makossa |
|-------|----------------|-----------------------|
| 1 | Almasi | <i>Arimas</i> |
| 2 | Magadi | Magadi |
| 3 | Uzi | Uzi |
| 4 | Mweupe | Mweupe |
| 5 | Rula | Rura |
| 6 | Shule | Shure |
| 7 | Chakula | Shakula |
| 8 | Jembe | <i>Shembe</i> |
| 9 | Mpira | Mpira |

Kama data zinavyoonekana katika jedwali, mtafitiwa namba saba alifanikiwa kuandika maneno manne kwa tahajia sahihi kati ya maneno tisa, alishindwa kuandika maneno matano kwa usahihi tunavyooneshwa kwenye jedwali. Kwa hiyo alifaulu kuandika kwa usahihi kwa asilimia 44% na alishindwa kuandika kwa kusahihi kwa asilimia 56%.

Mtafitiwa namba nane (8)

Mtafitiwa huyu naye hakuwa tofauti na waliopita kwani alipewa maneno yaleyale waliopewa wengine kuyaandika ili kuona kama ataweza kuandika kwa kuzingatia tahajia inayokubalika katika lugha ya Kiswahili sanifu. Matokeo ya kile alichokiandika yanaonekana kwenye jedwali lifuatalo.

Jedwali 4.26: Tahajia Sahihi Na Tahajia Iliyokosewa Na Mtafitiwa Namba 8

| Namba | Tahajia sahihi | Tahajia yenye makossa |
|--------------|-----------------------|------------------------------|
| 1 | Almasi | <i>Arimasi</i> |
| 2 | Magadi | <i>Maghadi</i> |
| 3 | Uzi | Uzi |
| 4 | Mweupe | Mweupe |
| 5 | Rula | Rura |
| 6 | Shule | Shure |
| 7 | Chakula | Chakula |
| 8 | Jembe | <i>Shembe</i> |
| 9 | Mpira | Mpira |

Kama data zinavyoonekana katika jedwali, mtafitiwa namba nane alifanikiwa kuandika maneno manne kwa tahajia sahihi kati ya maneno tisa. Alishindwa kuandika maneno matano kwa usahihi tunavyooneshwa kwenye jedwali. Kwa hiyo alifaulu kuandika kwa usahihi kwa asilimia 44% na alishindwa kuandika kwa kusahihi kwa asilimia 56%

Mtafitiwa namba tisa (9)

Kama ilivyokuwa kwa watafitiwa waliopita, mtafitiwa huyu naye alitamkiwa maneno yaleyale na mtafiti ili kuona kama atafanikiwa kuandika katika tahajia sahihi. Jedwali lifuatalo linaonesha namna mtafitiwa alivyoandika.

Jedwali 4. 27: Tahajia Sahihi Na Tahajia Iliyokosewa Na Mtafitiwa Namba Tisa

| Namba | Tahajia sahihi | Tahajia yenye makossa |
|--------------|-----------------------|------------------------------|
| 1 | Almasi | <i>Arimas</i> |
| 2 | Magadi | <i>Maghadi</i> |
| 3 | Uzi | Uzi |
| 4 | Mweupe | Mweupe |
| 5 | Rula | Rura |
| 6 | Shule | Shure |
| 7 | Chakula | Chakula |
| 8 | Jembe | Jembe |
| 9 | Mpira | Mpira |

Kama data zinavyoonekana katika jedwali, mtafitiwa namba tisa (9) alifanikiwa kuandika maneno matano kwa tahajia sahihi kati ya maneno tisa. Alishindwa kuandika maneno manne (4) kwa usahihi kama tunavyooneshwa kwenye jedwali. Kwa hiyo alifaulu kuandika kwa usahihi kwa asilimia 56% na alishindwa kuandika kwa kusahihi kwa asilimia 44%. Hivyo basi, matokeo ya jumla yanaonesha kuwa ni asilimia 35% ya waliopatia kuandika tahajia sahihi ya lugha ya Kiswahili na asilimia 65% walikosea kuandika. Jedwali lifuatalo linaonesha matokeo yalivyokuwa kwa ujumla.

Jedwali 4.28: Linaonesha Matokeo ya Jumla ya Watafitiwa

| Watafitiwa | Maneno yaliyopatiwa kuandika | Maneno yaliyokosewa kuandika |
|-------------------|-------------------------------------|-------------------------------------|
| 1 | 77 | 23 |
| 2 | 67 | 33 |
| 3 | 67 | 33 |
| 4 | 77 | 23 |
| 5 | 77 | 23 |
| 6 | 66 | 34 |
| 7 | 56 | 44 |
| 8 | 56 | 44 |
| 9 | 44 | 56 |
| Jumla | 65.2 | 34.7 =35 |

Kulingana na data zinavyoonekana katika jedwali hapo juu, karibu watafitiwa wote walikosea kuandika. Mtafiti ilibidi awahoji watafitiwa hao juu ya kukosea kwao katika kipengele hiki cha uandishi wa maneno ya Kiswahili. Wote walikiri kuwa ni kwa sababu ya kuathiriwa na lugha mama. Hivyo matokeo haya ya utafiti yanakubaliana na watafiti mbalimbali katika kazi zao walizochunguza. Matokeo haya yanakubaliana kabisa na utafiti alioufanya Noam Chomsky (1957) kama alivyonukuliwa na Matinde (ameshatajwa). Katika utafiti wake aligundua kuwa kila

mzungumzaji hujifunza sauti zinazohusika katika lugha yake, na kwamba iwapo atakumbana na sauti za lugha nyingine basi kuna kawaida ya yeye kuhamisha umilisi alionao wa sauti za lugha yake ya kwanza kwenda kwenye lugha ngeni (Kiswahili). Na hiki ndicho kilichotokea kwa watafitiwa ambao waliandika maneno ya lugha ya Kiswahili kwa kufuata sauti zao za lugha ya Kikurya. Matokeo haya pia hayatofautiani na alichokisema Wilkins (ameshatajwa). Katika kuchunguza athari za lugha mama katika lugha ya pili aligundua kuwa makosa ya matamshi, tahajia, sarufi na msamiati yana mtindo wa kujitokeza katika lugha za wahusika mbalimbali kutokana na kasoro za lugha ya kwanza na hivyo kuiathiri lugha ya pili. Akiongelea kipengele cha tahajia, alieleza kuwa tahajia mbovu ni changamoto katika lugha husika kwa sababu hupotosha mawasiliano na kufanya yasieleweke kama ilivyokusudiwa hususani uhalisia wa ujumbe. Mfano ufatao hapa chini unaonesha wanafunzi walivyoshindwa kuandika kwa usahihi maneno ya Kiswahili sanifu.

Tahajia iliyokosewa

Fundiswa
Mbegani
Nilundi
Ngari

Tahajia sahihi

Fundishwa
Begani
Nirudi
Gari

Ukweli huu kwa ujumla ndio uliojitokeza kwa watafitiwa wote tisa (9) waliotamkiwa maneno sahihi ya Kiswahili ili wayaandike. Kwamba, kukosea kwao kuyaandika kwa usahihi kwa asilimia kubwa ilitokana na wao kuathiriwa na lugha yao ya kwanza ya Kikurya. Kadhalika matokeo haya hayapingani na kile alichokieleza Wanyoike (1978) katika kazi yake. Alionesha namna watumiaji wa lugha za Kiluo, Kikamba, Kikuyu walivyoathiri maandishi ya lugha ya Kiswahili sanifu kutokana na athari za lugha ya kwanza. Anasema waliandika maneno ya lugha ya Kiswahili kwa

kuathiriwa na kanuni za lugha yao ya kwanza na hivyo kuiathiri lugha ya Kiswahili kama ilivyokuwa kwa watumiaji wa lugha ya Kikurya katika utafiti huu, waliathiri lugha ya Kiswahili kwa kuhamisha kanuni za uandishi wa lugha yao ya kwanza kwenda kwenye lugha ya pili (Kiswahili). Kwa upande wa Faki (2018), naye kazi yake haitofautiani na matokeo ya watafiti wenzake waliotangulia. Pamoja na kwamba alitafiti juu ya matumizi ya lugha tandawazi katika mitandao ya kijamii, bado alithibitisha kwamba makossa yanayofanyika ya uandishi wa herufi ni kutokana na athari za lugha mama. Ukweli huu unadhihirishwa na matokeo ya utafiti huu ambapo watafitiwa wote tisa walikosea kwa kiwango kikubwa kuandika kwa usahihi maneno waliotamkiwa na mtafiti. Hii ni kwa sababu waliathiriwa na lugha yao ya kwanza.

Halikadhalika, matokeo ya utafiti huu yanashabihiana kabisa na alichokisema Ahmad Kipacha (2012). Katika kazi yake, alionyesha athari za kitahajia kwenye lugha ya pili (Kiswahili) ambazo chanzo chake ni kutokana na athari za lugha mama. Makosa ya tahajia yanapojitokeza katika lugha yanakuwa ni kikwazo wakati wa mawasiliano kwa sababu msomaji hataelewa dhumuni mahususi la ujumbe. Mtafiti huyu alitoa mfano kwa kuonesha baadhi ya tahajia zilivyoandikwa isivyo sahihi namna zilivyoweza kuathiri lugha ya Kiswahili kama ifuatavyo hapa chini

Tahajia mbovu

Amkua
Yoyote
Yapi
Zoga
Ng'ambu

Tahajia sahihi

Amkia
Yeyote
Yepi
Zogo
Ng'ambo

Anaendelea kueleza kuwa pamoja athari za lugha mama kuonekana kuwa sababu ya tahajia mbovu bado mtafiti huyu aliongezea kwa kusema utohoaji pia ni sababu nyingine ya kuwa na tahajia mbovu katika maandishi, kwani mtu anapotohoa neno la kigeni na kuliingiza katika lugha ya Kiswahili lisivyostahili linaathiri tahajia ya lugha ya Kiswahili. Maelezo haya yanaowana na kile alichozungumza Timothy (2016) katika kazi yake, kwamba makosa mengi ya kiuandishi chanzo chake huwa athari za lugha mama. Na yanapoendelea kuhalalishwa katika utumizi wa lugha ya pili (Kiswahili) huifanya lugha ya pili (Kiswahili) kuonekana kuwa ni lugha holela isiyokuwa na hadhi. Matokeo ya tafiti hizi yanaonekana kufanana na matokeo ya utafiti wetu ambao ulichunguza athari za tahajia zilizotokana na athari za lugha ya Kikurya katika Kiswahili sanifu.

Utafiti huu vilevile katika kipengele cha tahajia unaoana kabisa matokeo ya utafiti alioufanya Mtungu (2010) ambaye alionesha vile wanafunzi walivyoshindwa kuandika insha kwa kutumia maneno sanifu ya lugha ya Kiswahili kwa sababu ya kuathiriwa na lugha yao ya asili (mama). Makosa ya uandishi (tahajia) yaliyoonekana katika insha yalihafifisha maana halisi ya ujumbe uliokuwa umekusudiwa kama ilivyoonekana kwenye matokeo ya utafiti huu, kwamba watumiaji wa lugha ya Kikurya hawakuweza kuandika tahajia sahihi kwa sababu ya kuathiriwa na lugha yao ya kwanza na hivyo kupoteza maana halisi za maneno waliyopewa kuandika.

Kitsao (2015) halikadhalika, kazi yake inakubaliana na ukweli wa utafiti huu kuwa athari za lugha ya kwanza huweza kusababisha tahajia isiyo sahihi katika lugha ya

Kiswahili. Akiwatumia wanafunzi kutoka shule ishirini na nne (24) kata ya Ganze kama sampuli yake. Alionesha namna ambavyo waliathiri tahajia ya lugha ya Kiswahili katika insha walizozindika. Alieleza kuwa, wanafunzi hao walikosea kwa sababu ya kuhamisha kanuni za lugha yao ya kwanza na kuziweka kwenye lugha ya Kiswahili. Mfano ufuatao unaonesha tahajia mbovu zilizopatikana kwenye insha walizozindika.

Sentensi/ neno lililokosewa

Sentensi/ neno sahihi

a/ Nguo yako ina ngara sana

Nguo yako inang'ara sana

b/ N'gombe

Ng'ombe

c/ Piya

Pia

Kama inavyoonekana kwenye mfano, wanafunzi hawakufaulu kuandika kwa usahihi tahajia husika kama ilivyo katika lugha ya Kiswahili. Chanzo cha makosa hayo ni athari za lugha mama kama ilivyoelezwa na mtafiti. Pamoja na kwamba kazi ya Kitsao (ameshatajwa) inatofautiana kidogo kimalengo na utafiti huu lakini bado matokeo ya tafiti zote mbili yanafanana. Kwamba, Utafiti wetu ulichunguza namna lugha ya Kikurya inavyoweza kuathiri lugha ya Kiswahili wakati wa ujifunzaji kwa kutalii vipengele vya matamshi, muundo na tahajia.

Lakini kazi ya Kitsao (ameshatajwa) ilijikita kuchunguza makosa ya kisarufi katika insha za wanafunzi kwa kutalii vipengele vya tahajia, udondoshaji pamoja na kukata maneno. Hata hivyo, mwisho wa kazi zote mbili unaonyesha kwamba lugha ya kwanza ya mama inaathiri tahajia katika lugha ya Kiswahili. Naye Corder (ameshatajwa) katika kazi yake anakubaliana na utafiti wetu kuwa athari katika

tahajia husababishwa na athari za lugha ya kwanza. Anaeleza kwamba watu wanapojifunza lugha ya pili huwa wanayo lugha ya kwanza, nao hutumia kanuni wanazozielewa za lugha ya kwanza katika kuandika maneno kwenye lugha ya pili, kisha huhamisha muundo wa lugha ya kwanza kwa lugha ya pili. Jambo hili ndilo lililowatokea watumiaji wa lugha ya Kikurya. Kwamba walihamisha kanuni za lugha yao ya kwanza katika kuandika maneno ya lugha ya Kiswahili na kuiyathiri lugha ya Kiswahili. Maoni haya yanawiana pia na matokeo ya utafiti wa Halliday (1964). Kadhalika kazi ya Fromkin, Rodman na Hyams (2007) inakubaliana kabisa na matokeo ya utafiti huu kuwa ni ukweli usiopingika kwamba athari za lugha mama huathiri lugha ya pili katika vipengele vya matamshi, muundo, maumbo na hata tahajia ya neno. Walitoa mfano kwa kuonesha mjapani anaejifunza lugha ya Kiingereza anavyoshindwa kutofautisha namna ya kuandika na kutamka neno “*write*” na “*light*” na kuiathiri lugha ya Kiingereza.

Alishindwa kuandika vyema kwa kuwa [r] na [l] si fonimu katika lugha yao kama ambavyo iliwatokea watumiaji wa lugha ya Kikurya. Waliandika fonimu zisizo sahihi katika maneno waliyopewa kwa sababu ya kuathirika na lugha ya kwanza. Utafiti wao unafanana kabisa na utafiti wetu japo unatofautiana kidogo na kazi yetu kwa kipengele cha watafitiwa waliohusishwa katika utafiti. Kadhalika wao walichunguza athari ya lugha ya Kijapani katika kujifunza lugha ya Kiingereza na wakagundua kuwa lugha ya Kiingereza iliathirika katika matumizi hayo kwa sababu Wajapani waliathiriwa na lugha yao ya kwanza kama ilivyokuwa kwa watumiaji wa lugha ya Kikurya katika lugha ya Kiswahili. Hivyo basi, utafiti huu unathibitisha kwamba lugha ya pili (Kiswahili) iliathirika katika mfumo wake wote wa matamshi,

maandishi na hata pia mpangilio wa sentensi pamoja na vipashio vyake. Hii ni kutokana na fonolojia, maumbo na miundo ya lugha yao ya kwanza yaani Kikurya kuwa tofauti na lugha ya pili ambayo ni Kiswahili.

4.3 Sababu Zinazochangia Lugha ya Kikurya Kuathiri Ujifunzaji wa Lugha ya Kiswahili Sanifu

Katika kufanya utafiti juu ya swali hili, jumla ya watu ishirini na moja (21) waliokuwa kwenye sampuli ya utafiti walipewa hojaji ili wajaze sababu ambazo wanazifahamu zinazochangia lugha ya Kikurya kuathiri ujifunzaji wa Kiswahili sanifu. Kila mtafiti alishiriki kwa nafasi yake pamoja na kutoa mtazamo wake juu ya sababu za lugha ya Kikurya zinavyoathiri ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili sanifu. Matokeo ya utafiti yalionyesha kuwa sababu kubwa ni athari ya lugha ya kwanza, mitazamo finyu katika jamii na mwisho walisema ni kukosekana kwa baadhi ya sauti (mofimu) katika lugha ya Kikurya zinazoweza kutamkwa kwa usahihi katika lugha ya Kiswahili.

4.3.1 Athari za Lugha ya Kwanza

Watafitiwa wote ishirini na moja (21) waliopewa hojaji walitaja “Athari ya lugha ya kwanza” kuwa ni sababu kubwa iliyoathiri ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili sanifu. Hii ina maana kuwa asilimia mia moja (100%) ya waliohojiwa walitaja sababu hii. Walisema kuwa wao wamezoea Kwamba, kutokana na mazoea hayo hawakuona umuhimu wa kujifunza lugha ya Kiswahili kwa sababu mahitaji yao yote ya mawasiliano yalitimia kupitia lugha yao ya kwanza ya Kikurya. Matokeo haya ya utafiti yanathibitisha alichokisema Noam Chomsky (1957) aliyenukuliwa na Matinde

(ameshatajwa) akisema kuwa kila mtu hujifunza na kumudu mfumo wa lugha yake ya kwanza lakini anapoanza kujifunza lugha nyingine hutumia mfumo wake wa lugha ya kwanza aliouzoa kuweza kujifunza lugha ya pili. Kwa kufanya hivyo ni lazima lugha ya pili Kiswahili iathirike kwa sababu maandishi, mpangilio wa vipashio pamoja na sauti za lugha hiyo ya pili zilitamkwa na kuandikwa isivyo sahihi. Cruse (1985) naye anakubaliana na ukweli huo katika uchunguzi wake ambapo aligundua kwamba makosa mengi katika lugha ya pili huwa na ufananisho wa lugha ya kwanza. Anaendelea kusema makosa hayo ni kutokana na watu wanapojifunza lugha ya pili huwa tayari wanayo lugha ya kwanza, hivyo hutumia kanuni wanazozielewa katika lugha ya kwanza wakati wa mazungumzo (usemaji) na uandishi wa lugha ya pili. Kutokana na hali hii ya kuwa na mazoea ya kutumia kanuni za lugha ya kwanza katika lugha ya pili imekuwa ni chanzo cha kuathiri lugha ya pili katika usemaji na pia uandishi (tahajia). Changamoto hii ndio iliyowapata watumiaji wa lugha ya Kikurya walipozungumza lugha ya Kiswahili kama lugha ya pili kwao.

Pia tafiti zaidi zilizotangulia ikiwemo ya Wenceslaus (ameshatajwa) zinathibitishwa na matokeo ya utafiti kuwa lugha ya Kiswahili kama lugha ya pili mara nyingi huanza kujifunzwa pale watoto wanapoanza shule. Na kwamba, wanapojifunza lugha ya Kiswahili, kwao hushindwa kumudu vyema kutamka, kuandika na hata kupanga vipashio vizuri katika sentensi na hivyo kujikuta wakiathiri lugha ya Kiswahili Sanifu katika nyanja mablimbali. Hii pia inathibitishwa na Romaine (1994) ambaye anaonesha kuwa lugha moja kuathiri nyingine ni matokeo ya vikwazo – ndani kwa kuwa kila mzungumzaji wa lugha unakuta ameathiriwa na lugha yake ya

asili, na hivyo anapojifunza lugha ya pili (Kiswahili) lazima ahamishe kanuni za lugha yake ya kwanza kwenda lugha ya pili na hivyo kuiathiri lugha hiyo. Sovu (ameshatajwa) naye anathibitshwa na utafiti wetu kuwa alikuwa sahihi kwa kuonesha kuwa lugha ya Kiswahili iliathiriwa na lugha ya Kiha katika matamshi na hata maandishi. Alisema asilimia sabini na moja (71%) ya watafitiwa wote katika kata zote za manispaa ya Kigoma ujiji walisikika wakitamka sauti [mu] badala ya [m] kwa mfano; *Rose ameweka chakula musufuria, Juma amekwendamumpira*. Wazungumzaji wa Kigoma walichanganya matamshi ya Kiha katika Kiswahili cha mazungumzo kwa sababu ya kuathiriwa na lugha yao ya asili. Kadhalika Mbaabu (1978, 1985, 1995) katika utafiti wake alichunguza Maingiliano ya lugha za kwanza na Kiswahili sanifu. Na aligundua kuwa lugha za asili zimechangia kwa kiasi kubwa kuathiri lugha ya Kiswahili sanifu. Anaendelea kusema kuwa athari hutokea katika makundi yote manne ambayo ni kundi la kimatamshi, kisarufi, kimaana na kimaandishi. Athari hizo huingiliana katika makundi yote manne, ambapo kosa la kimatamshi linaweza pia kuwa la kisarufi na linaweza kuathiri maana ya matamshi au maandishi. Ukweli huu umeowana na majibu ya kazi yetu ya utafiti. Maana jambo hilo ndilo lililowatokea watafitiwa katika lugha ya Kikurya.

Ukweli huu pia unakubaliwa na Nyanda (ameshatajwa) katika utafiti wake, ambapo alionesha kuwa lugha ya Kiswahili iliathiriwa na watumiaji wa kabila la Kinyamwezi kutokana na athari za lugha yao ya kwanza. Kwamba, baadhi ya misamiati ya lugha ya Kiswahili ilikosekana katika lugha ya Kinyamwezi na hivyo ilibidi watamke misamiati hiyo ndani ya lugha ya Kiswahili ambayo ilipelekea athari katika lugha ya Kiswahili. Kazi ya Otiende (ameshatajwa) nayo inakubaliana na utafiti wetu kuwa

athari za lugha mama huathiri lugha ya Kiswahili. Katika kazi yake alibainisha athari zinazodhihirika katika matumizi ya Kiswahili miongoni mwa watu ambao lugha yao ya kwanza ni Kiolusuba. Kadhalika, wanaisimu kama vile Nickel (1972) katika Lange (1974) na Corder (ameshatajwa) wanakubaliana kwamba makosa ya lugha ya kwanza huathiri lugha ya pili katika viwango vyote vya lugha yaani fonolojia, mofolojia na hata sintaksia. Mawazo haya pia yaliungwa mkono na Valdman (1975) aliyeorodhesha data ya lugha 246 zilizo na athari za lugha ya kwanza kwa lugha ya pili katika sintaksia, matamshi, tahajia na hata katika msamiati. Matokeo ya utafiti wetu pia unakubaliana na Massamba (ameshatajwa) ambaye kazi yake inakubaliana na ukweli wa utafiti huu kuwa lugha mama huathiri lugha ya Kiswahili. Aligundua kuwa lugha mama ambazo aliziita lugha za kienyeji zina athari kubwa kwenye lugha ya Kiswahili katika viwango mbalimbali kama vile fonolojia, msamiati na sarufi kwa ujumla. Anaeleza zaidi kwamba athari hizo yaweza kuwa udondoshaji wa baadhi ya sauti, uchopekaji katika matumizi ya maneno ya Kiswahili kutokana na athari ya lugha za kwanza, hali iliyosababisha makosa ya utamkaji na uandishi katika lugha ya Kiswahili. Hivyo basi, Kutokana na uchambuzi wa data katika utafiti huu zilizowasilishwa, mtafiti anakubaliana na tafiti zilizotangulia kuwa lugha mama yaani Kikurya ina athari kubwa katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili Sanifu.

4.3.2 Mitazamo Finyu Katika Jamii

Kwa upande wa mitazamo finyu katika jamii, watafitiwa wawili (2) kati ya watafitiwa ishirini na moja (21) ambao ni sawa na asilimia kumi (10%) walisema kuwa mitazamo finyu katika jamii haiwezi kusababisha lugha ya Kikurya kuathiri ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili Sanifu. Watafitiwa kumi na tisa (19) ambao ni sawa

na asilimia tisini (90%) wao walikubaliana na “Mitazamo finyu katika jamii”. Walisema kuwa mitazamo finyu katika jamii ni moja ya sababu inayoathiri ujifunzaji wa Kiswahili sanifu. Walieleza kuwa sababu kubwa hapa inatokana na tabia iliyojengeka katika jamii ambapo watu wanaoonekana kujifunza kuzungumza lugha ya Kiswahili na kutaka kuizungumza katika jamii wanaonekana kama watu wanaoringa na kujifanya kuwa bora kuliko wengine. Jambo hili limekuwa ni kikwazo kwa watu wa jamii ya wakurya wanaojaribu kuzungumuza lugha ya Kiswahili. Hoja hii ya utafiti wetu inakubaliana kabisa na tafiti mbalimbali zilizokwisha fanyika hapo awali. Kwa mfano, tukiangazia kazi ya Nyanda (ameshatajwa) na Lusesa (ameshatajwa) wote wanaeleza kuwa wakati mwingine wanaojaribu kuzungumza Kiswahili wamekuwa wakichekwa na watu waliowazunguka pindi wanapokosea utamkaji sahihi wa sauti fulani. Pia Mochwa (1979) naye anakubaliana na ukweli huo.

Katika maelezo yake akitolea mfano wakazi wa wilaya ya Handeni mkoani Tanga ambapo anasema, jamii ya watu wanaoishi maeneo ya vijijini sana mwitikio wao ni mdogo katika kujifunza lugha ya Kiswahili kwa sababu imezoeleka kwao kutumia lugha ya asili katika mawasiliano miongoni mwao na pia katika shughuli zao zote za kila siku. Hivyo huidharau lugha ya Kiswahili na kuona haina haja ya kujifunza wala kutumia lugha hiyo kwani mahitaji yao yote hujitosheleza kupitia lugha yao ya Kizigua. Matokeo ya utafiti wetu yanakubaliana pia na Rubanza (1979) ambaye katika kazi yake anaonesha namna wazungumzaji wa lugha ya Kihaya ambavyo hakuwa na utayari wa kutaka kujifunza lugha ya Kiswahili sanifu kwa sababu ya kuheshimu tamaduni na mila zao zilizoongozwa na wazee wao. Walitaka kudumisha

utamaduni wa kuzungumuza lugha yao ya asili hata kwa vizazi vijavyo. Maelezo haya yanashadadiwa na Msanjila (2009) aliyesema kila jamii huwa na mila, desturi na utamaduni wa aina moja ambao huzingatiwa na wanajamini na hivyo ni vigumu jamii kuacha mila walizoea. Hoja hii pia inapata mashiko kwa Massamba (1977) katika kazi yake alipokuwa akilinganisha lugha za pembe ya mashariki ya ziwa nyanza (Victoria) ambazo ni Kiruri, Kijita na Kikwaya na namna walivyokuwa wazito kujifunza lugha ya Kiswahili kwa sababu ya kuendekeza mila na tamaduni zao. Utafiti huu pia unakubaliana na Mhilu (2005), Rocha (2011) aliyenukuliwa na Wenceslaus (ameshatajwa) pamoja na Mekacha (2011) nao wanaungana na watafiti waliotangulia katika hoja hii kwenye kazi yake kwa kusema jamii nyingi huwa na mtazamo hasi na lugha ya pili katika kujifunza. Waliamini kuwa matumizi ya lugha zaidi ya moja husababisha utata katika jamii na hatimaye kudumaza maendeleo. Kutokana na mtazamo huo hawakuwa na utayari wa kujifunza lugha ya pili ambayo ni Kiswahili.

Katika kazi yake Athuman (ameshatajwa) anaunga mkono hoja hii kwa kueleza kuwa upekee wa jamii fulani katika makazi nayo hupelekea jamii kuwa na mtazamo hasi katika kujifunza lugha ya Kiswahili. Akitoa mfano kwa kurejea jamii ya wayao anaonesha namna ambavyo walithamini lugha ya kiyao na kushindwa kutoa mwanya wa kutaka kujifunza lugha ya Kiswahili. Udhaifu huu ulionekana pia katika jamii ya wangoni kama anavyoeleza Haule (2014) kwamba hawakuwa tayari kujifunza lugha ya Kiswahili kwa sababu ya upekee waliokuwa nao katika jamii yaani walikumbatia lugha yao na kuiona ni bora kuliko lugha ya Kiswahili. Kazi ya Ngonyani (ameshatajwa) nayo inathibitishwa na utafiti wetu kwa kueleza kwamba jamii

inapokuwa haina elimu ya kutosha kuhusiana na thamani ya lugha ya Kiswahili hasa maeneo ya vijijini ni rahisi kwao kupuuza kujifunza Kiswahili. Akitolea mfano Wangoni alionesha kuwa walionekana kutokuwa na utayari wa kutaka kujifunza lugha ya Kiswahili kwa kuwa hawakuona umuhimu wake. Ukweli huu unaowana na matokeo waliotoa Thomason (2001) na Besha (1994) katika kazi zao ambayo yanashabihiana kabisa na utafiti wetu. Kutokana na ukweli huu wa utafiti inaonekana kuwa wazungumzaji wengi wa lugha ya Kikurya wamekuwa wakiipa kipaumbele lugha ya Kikurya kuliko lugha ya Kiswahili. Matokeo yake ni kwamba wameshindwa kujifunza lugha ya Kiswahili sanifu na hivyo kujikuta wakikosea namna ya kuandika baadhi ya herufi, namna ya kutamka baadhi ya sauti na namna ya kupanga vipashio kwa ufasaha. Utafiti huu basi, unakubaliana kabisa na tafiti zilizotangulia ambazo zote zilionesha kwamba mitazamo finyu katika jamii iliyojikita katika lugha zao za asili huathiri ujifunzaji wa Kiswahili sanifu. Hii inadhihirishwa kutokana na matokeo ya utafiti huu ambapo asilimia (90%) ya watafiti walionesha kwamba lugha ya Kiswahili imekuwa ikiathiriwa zaidi na lugha ya Kikurya kwa sababu ya kutofuata sheria na kanuni zinazotawala mazungumzo na uandishi katika lugha ya Kiswahili.

4.3.3 Athari za Sarufi Matamshi katika Lugha ya Kikurya

Sarufi matamshi hushughulika na mfumo wa sauti katika lugha fulani. Hyman (1975) anaelezea tawi hili kama mtalaa wa mfumo wa sauti yaani linashughulikia jinsi sauti hupangwa pamoja na uamili wake katika lugha mahususi. Kwa hiyo athari zilizoshughulikiwa katika kipengele hiki ni zile zinazo athiri matamshi au sauti (fonimu) za lugha mahususi kama ilivyo kwa lugha ya Kikurya katika lugha ya

Kiswahili sanifu. Kwa mfano watumiaji wa lugha ya Kikurya walibadlisha sauti za lugha ya Kiswahili wakati wa utamkaji na kusababisha athari kubwa katika lugha kwani sauti hizi zinpotamkwa isivyo sahihi hubadilisha na kupotosha maana halisi ya neno. Katika kipengele hiki, jumla ya watafitiwa ishirini na moja (21) walihojiwa. Kati ya hao watafitiwa kumi na tano (15) sawa na asilimia sabini na moja (71%) walikubaliana na hoja hii kwa maelezo ya kwamba kuna baadhi ya sauti za Kikurya zinakosekana kwenye lugha ya Kiswahili Watafitiwa watano (5) ambao ni sawa na asilimia ishirini na tatu (23%) hawakukubaliana na sababu hii. Na mtafitiwa mmoja (1) sawa na asilima (4%) alisema haelewi chochote. Asilimia sabini na moja (71%) ya watafitiwa waliokubaliana na sababu hii walipohojiwa na mtafiti kwa nini walikubaliana hivyo walisema kuwa sauti wanazoshindwa kuzitamka pamoja na kuandika kwa usahihi ni zile ambazo hazipatikani kwenye lugha yao ya kwanza ambazo ndizo zinatakiwa kutamkwa katika maneno ya Kiswahili. Baadhi ya sauti ambazo zilionekana kuwa ni changamoto kwao kuzitamka ni pamoja na /li/, /ba/, /ja/ /zi/, /ga/ pamoja /fa/. Sababu ya kushindwa kutamka sauti hizi za lugha ya Kiswahili ni kutokana na lugha yao ya Kikurya kutokuwa na sauti hizo pia miundo tofauti ya baadhi ya maneo.

Mfano walisema:

Badala ya /li/ wanatumia /ri/

Badala ya /ba/ wanatumia /bha/

Badala ya /ja/ wanatumia /sha/

Badala ya /zi/ wanatumia /si/

Badala ya /ga/ wanatumia /gha/

Badala ya /va/ wanatumia /fa/

Matokeo haya ya utafiti wetu ambayo watafitiwa asilimia sabina moja (71%) wote walikubaliana na sababu ya kukosekana kwa baadhi ya sauti katika lugha ya Kikurya yanakubaliana kabisa na tafiti zilizotangulia. Mfano, utafiti wa Bagheri (2012), pia utafiti wa Otiende (ameshatajwa) ambaye alionesha jinsi athari za kimofonolojia za Kisoluba zinavyoathiri matumizi ya Kiswahili Sanifu kama lugha ya pili. Halikadhalika, Wencelaus (ameshatajwa) naye alieleza namna ambavyo lugha ya Kijita iliathiri Kiswahili Sanifu. Alisema sababu kubwa ya lugha ya Kiswahili kuathiriwa na lugha ya Kijita ni kutokana na kutumia lugha ya Kijita kwa asilimia kubwa kuliko kuhamasisha utumiaji wa lugha ya Kiswahili sanifu. Akitolea mfano wanafunzi ambao ndio sampuli yake, anasema walichanganya matumizi ya sauti katika Kiswahili kwa kuwa lugha ya Kijita haikuwa na hizo sauti. Anaeleza pia kulikuwa na athari katika matumizi ya /z/ badala ya /dh/, matumizi ya /s/ badala ya /dh/, kitu ambacho pia kimejitokeza katika watumiaji wa lugha ya Kikurya kwa baadhi ya sauti.

Sovu (ameshatajwa) anakungwa pia mkono na utafiti wetu katika utafiti wake uliosema matumizi ya Kiha katika Kiswahili cha mazungumzo ambapo alionesha watumiaji wa lugha ya Kiha walivyokosea kuzungumza lugha ya Kiswahili kwa ufasaha. Sababu iliyofanya kukosea ni kutokana na ukosefu wa baadhi ya sauti katika lugha yao ya asili na kusababisha kuiathiri lugha ya Kiswahili wakati wanapozungumza. Anasema wengi wao walisikika wakitamka sauti /bh/ badala ya /b/ kadhalika [bu] na [tu] badala ya [wa]. Pia Muthu (2005) pamoja Nyanda (ameshatajwa) wanaungwa mkono na utafiti wetu ya kuwa sauti zinazokosekana katika lugha za asili ni kikwazo kwa watumiaji wa lugha hizo pindi wanapojifunza/

kuzungumza lugha ya Kiswahili, kwa sababu huchanganya sauti za lugha mama katika Kiswahili sanifu na hivyo kuathiri lugha ya Kiswahili. Kadhalika matokeo ya utafiti huu hayatofautiani na yale ya Ng'ang'a (2000) ambapo alionesha lugha ya Kiingereza ilivyoathiriwa na watumiaji wa lugha ya Kikuyu ambayo ni lugha ya kwanza kwa upande wao. Anaeleza lugha ya Kiingereza iliathiriwa katika vipengere vya kisintaksia, kisementiki na kimofolojia. Makosa yaliyotokea katika nyanja hizo ni kutokana na ukosefu wa baadhi ya sauti katika lugha ya Kikuyu na kupelekea makosa ambayo yamekuwa yakiathiri lugha ya Kiingereza kwa sababu ya kuhamisha kanuni za lugha yao ya kwanza kwenye lugha ya pili. Kazi ya Were (ameshatajwa) nayo inaungwa mkono na matokeo ya utafiti wetu kuwa baadhi ya wazungumzaji huwa wanajumuisha sheria ambazo huathiri lugha ya Kiswahili. Kwenye maelezo yake alionesha wanafunzi walivyojumuisha sheria ambazo kimsingi hutoka lugha ya kwanza na kuzipeleka kwenye lugha ya pili (Kiswahili).

Matokeo ya ujumuishaji huo ni kuathiri lugha ya Kiswahili kwa kuongeza, kubadili ama kudondosha sauti. Maelezo haya yanashabiana kabisa na alivyoeleza Richards (1975) pamoja na Brown (ameshatajwa) kwamba athari katika lugha ya pili (Kiswahili) hutokana na watumiaji wa lugha za asili kukiuka kanuni zinazotawala lugha ya pili. Anaendelea kusema kuwa kumekuwa na mazoea ya kutumia sauti za lugha ya kwanza katika lugha ya pili ambayo hupelekea upotovu wa hiyo lugha. Ukweli huu pia uliungwa mkono na Lusesa (ameshatajwa) pamoja na Chomsky, (naye amekwishatajwa), ukweli ambao umedhihirishwa Dhahiri katika utafiti wetu kwa watafitiwa wa lugha ya Kikurya. Hivyo basi, kulingana na data zilizokusanywa na kuchambuliwa, utafiti huu unadhihirisha kwamba tafiti zilizotangulia zilikuwa

sahihi kuonyesha kwamba ukosekanaji wa baadhi ya sauti za lugha mbalimbali za makabila katika lugha ya Kiswahili zinasababisha athari kubwa katika kujifunza lugha ya Kiswahili Sanifu kama jedwali lifuatalo hapa chini linavyoonesha.

Jedwali 4.29: Sababu Zilizochangia Lugha Ya Kikurya Kuathiri Ujifunzaji wa Kiswahili Sanifu

| Na | Sababu zilizo hojiwa | Idadi ya wahojiwa | Waliokubaliana na sababu hii | % | Wasiokubaliana na sababu hii | % | Wasio upande wowote | % |
|----|---|-------------------|------------------------------|------|------------------------------|-----|---------------------|----|
| 1 | Athari ya lugha ya kwanza. | 21 | 21 | 100% | 0 | 0% | 0 | 0% |
| 2 | Mitazamo finyu katika jamii | 21 | 19 | 90% | 2 | 10% | ----- | 0% |
| 3 | Athari za sarufi matamshi katika lugha ya Kikurya | 21 | 15 | 71% | 5 | 23% | 1 | 4% |

Jedwali hili linaonyesha jinsi watafitiwa walivyojibu kulingana na sababu za lugha ya Kikurya zinavyoathiri ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili sanifu.

4.4 Hitimisho

Sura hii ilihusika na uwasilishaji, uchambuzi pamoja na mjadala wa data zilizokusanywa katika utafiti huu. Uwasilishaji wa uchambuzi wa data umefanyika kwa kuzingatia malengo mahususi ya utafiti huu. Ambapo tumeona jinsi maneno ya lugha ya Kikurya yanavyoathiri ujifunzaji wa Kiswahili sanifu pamoja na sababu zinazochangia lugha ya Kikurya kuathiri lugha ya Kiswahili. Hivyo basi, utafiti huu unadhihirisha kuwa lugha ya Kikurya ina athari katika lugha ya Kiswahili.

SURA YA TANO

5.0 HITIMISHO, MUHTASARI NA MAPENDEKEZO

5.1 Utangulizi

Sehemu hii ni hitimisho la zoezi zima la utafiti. Imeongelea muhtasari, mapendekezo na hitimisho la utafiti. Muhtasari kwa kawida huwa ni ufupisho kati ya mambo mengi yaliyoelezwa kuhusu jambo fulani. Muhtasari wa utafiti wetu umezungumzia kwa ufupi mambo yaliyojiri katika utafiti huu. Kadhalika, mapendekezo ni mawazo ambayo hutolewa kuhusu jambo fulani. Mapendekezo yaliyotolewa katika utafiti huu yana lengo la kuboresha na kujenga zaidi ili kuweza kupata mafanikio makubwa zaidi. Hitimisho huwa ni jambo linalosemwa au kuandikwa mwisho, yaani tamati. Mtafiti amehitimisha mambo aliyoyazungumza kulingana na utafiti alioufanya.

5.2 Muhtasari wa Utafiti

Utafiti huu umejengeka katika sehemu nne. Sehemu ya kwanza ilihusika na utangulizi, sehemu ya pili ilihusika na mapitio ya kazi tangulizi na mkabala wa kinadharia, sehemu ya tatu imeongelea mbinu za utafiti na sehemu ya nne ilihusika na uwasilishaji, uchambuzi na mjadala wa data. Sehemu zote zimefafanua na kueleza mambo kwa kina zaidi kuhusiana na utafiti wetu, lengo likiwa ni kuweka ukweli kuwa bayana. Mada kuu ya utafiti ilihusu “Athari za Kikurya katika ujifunzaji wa Kiswahili Sanifu miongoni mwa Wakurya”. Utafiti huu uliongozwa na malengo mawili. Lengo la kwanza lililenga kuonesha jinsi maneno ya lugha ya Kikurya yanavyoathiri ujifunzaji wa Kiswahili Sanifu. Lengo hili lilifanyiwa kazi na mtafiti na kubainisha wazi ukweli huu wa maneno ya lugha ya Kikurya yanavyoathiri

ujifunzaji wa Kiswahili Sanifu. Sehemu ya nne ya utafiti huu katika kipengele cha 4.2.1, 4.2.2 na 4.2.3 inaonyesha namna lengo hili lilivyoielezwa pamoja na kujadiliwa kwa kuzingatia data zilizokusanywa. Lengo la pili la utafiti lilikuwa ni kubainisha sababu zinazopelekea athari za Kikurya katika ujifunzaji wa Kiswahili. Kadhalika, lengo hili limefafanuliwa na kujadiliwa kwa kina na mtafiti kulingana na data zilizokusanywa kwa watafitiwa. Wazungumzaji walitoa sababu zinazo changia wao kuathiri lugha ya Kiswahili pindi wanapojifunza au kuzungumza pamoja na kuandika. Sehemu ya nne ya utafiti huu, kuanzia kipengele cha 4.3.1, 4.3.2, na 4.3.3 imefafanua vizuri.

Swali la kwanza lilisema, “Jinsi gani maneno ya lugha ya Kikurya yanaathiri ujifunzaji wa Kiswahili Sanifu?”, Swali la pili lilisema, “Ni sababu zipi zinachangia lugha ya Kikurya kuathiri ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili Sanifu?” maswali haya yamefanyiwa kazi na mtafiti. Sehemu ya nne ya utafiti huu imeeleza vizuri eneo hili na kulijadili kwa undani zaidi kulingana na data zilizokusanywa. Ili kuweza kutimiza lengo la utafiti ni lazima utafiti uwe na muongozo. Katika utafiti huu tuliongozwa na nadharia ya Fonolojia Zalishi Asilia. Nadharia hii ilikuwa na manufaa kwa mtafiti kwani ilikuwa muongozo kwake na pia ilimsaidia kupata mafanikio ya kile alicholenga katika utafiti wake. Utafiti huu ulifanyika katika mkoa wa Mara. Ulipangwa kufanyika wilaya za Tarime, Butiama na Serengeti. Wilaya ya Tarime ilichukuliwa kama sampuli ya Utafiti. Ulihusisha makundi rika ya vijana, watu wenye umri wa kati pamoja na wazee kwa kuzingatia jinsia zao. Mtafiti alitumia data za msingi katika utafiti huu ambapo alizipata kwa kutembela maskani ya watafitiwa. Aidha, utafiti huu ulihusisha mbinu ya hojaji pamoja na mahojiano

wakati wa ukusanyaji wa data. Utafiti huu ulibaini kuwa lugha za asili za makabila zilichangia sana kuathiri lugha ya Kiswahili katika nyanja tofauti tofauti. Ukweli huu ulithibitishwa na tafiti mbalimbali zilizotangulia ikiwemo ya Nyanda (ameshatajwa) aliyezungumza juu ya athari ya lugha ya Kinyamwezi katika kujifunza lugha ya Kiswahili. Mtafiti anakubaliana kuwa lugha za asili huchangia katika kuathiri lugha ya Kiswahili, hii ni kutokana na kujiridhisha nafsi yake baada ya utafiti alioufaya kuhusiana na lugha ya Kikurya ilivyoweza kuathiri lugha ya Kiswahili wakati wa ujifunzaji.

5.3 Mapendekezo ya Utafiti

Kama anavyoeleza Cann (1983) vikwazo vinavyotinga mawasiliano katika lugha ya Kiswahili ni vingi na vinazidi kupata nguvu. Hivyo ni muhimu basi kuweka mikakati itakayoimarisha lugha ya Kiswahili ili kuweza kukiweka katika hadhi inayostahili. Kutokana na matokeo ya utafiti huu, mtafiti amependekeza jamii ielimishwe kuhusu thamani ya lugha ya Kiswahili. Hii ni kutokana na watu mbalimbali hasa wakazi wa maeneo ya vijijini ambao wamekuwa wakidharau lugha ya Kiswahili na kuona haina thamani kwao. Pia wamekuwa wakiendekeza mitazamo finyu, tamaduni potofu, pamoja na mila na desturi ambazo zinawakosesha haki yao ya msingi ya kujifunza na kujua lugha yao ya taifa. Mtafiti amependekeza kuwa vyombo mbalimbali vyenye dhamana ya kukuza, kuimarisha, na kuendeleza lugha ya Kiswahili nchini Tanzania kama vile BAKITA, vihusishwe katika kubuni njia ya kusaidia wakazi walioko maeneo ya vijijini ili kuweza kukipenda Kiswahili na kukithamini. Kwa kufanya hivyo itasaidia lugha ya Kiswahili kukua na kuendelea kuwa katika hadhi yake.

Mtafiti anapendekeza pia kuwepo na makongamano mbalimbali kuhusiana na lugha ya Kiswahili na kuelekezwa hasa sehemu za vijijini. Hii itasaidia kuhamasisha matumizi ya lugha ya Kiswahili katika maeneo yao. Kwa kufanya hivyo kutasidia kuzuia Kiswahili kisiendeleo kuathiriwa na lugha za asili za makabila. Kwa sababu mwaikio ukiwa mkubwa wa watu kujifunza lugha ya Kiswahili kwa ufasaha ndivyo idadi inavyozidi kupungua ya watu wasiojua kuzungumza ama kuandika lugha ya Kiswahili kwa ufasaha.

Aidha mtafiti anapendekeza kuwa lugha ya Kiswahili ifanywe kuwa lugha kuu ya kufundishia katika ngazi zote za elimu toka elimu ya awali, msingi, sekondari hadi vyo vikuu. Kwa kufanya hivyo kutapungua ama kuepuka kabisa tatizo la kuathiriana na hasa lugha za asili kwa Kiswahili sanifu kwa sababu watu wengi watakuwa na mwamko wa kutumia lugha ya Kiswahili kuliko ambavyo ilivyo sasa katika jamii za watu wanaoishi hasa maeneo ya vijijini. Pamoja na hayo, mtafiti anapendekeza kuwa tafiti nyingi zifanyike ili kuweza kuibua maarifa mapya kuhusiana na lugha za asili za makabila zinavyoweza kuingiliana na hata kuathiri lugha ya Kiswahili. Hii itasaidia kujua ni namna gani tunaweza kuepuka na kukihifadhi Kiswahili kisiathiriwe na lugha mama za makabila mbalimbali.

5.4 Hitimisho

Utafiti huu ulikusudia kuchunguza athari ya lugha ya Kikurya katika ujifunzaji wa Kiswahili Sanifu miongoni mwa Wakurya. Aidha, ulilenga kubaini, kueleza na kufafanua sababu zinazopelekea lugha ya Kikurya kuathiri ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili sanifu. Utafiti umebaini kuwa lugha mama za makabila tofauti tofauti

ikiwemo lugha ya Kikurya zimekuwa zikiathiri lugha ya Kiswahili kwa kiasi kikubwa. Mtafiti alithibitisha kwa kuchunguza vipengele vya matamshi, mpangilo wa sentensi pamoja na tahajia. Matokeo ya utafiti wa vipengele hivi yameelezwa vizuri katika sehemu ya nne ya utafiti huu. Utafiti umefanikiwa kutambua chanzo cha tatizo la watumiaji wa lugha ya Kikurya katika kuathiri ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili Sanifu.

MAREJEO

- Adam, J. & Kauzora, F., (2008). *Research methods for bussines and social studies*. Morogoro: Mzumbe book project.
- Aruba, B. K., (2017). Makosa ya Semantiki katika Mawasiliano Andishi ya Kiswahili Miongoni mwa Wanafunzi wa Shule za Upili: Mfano wa Akaunti ya Kakamega. Tasnifu. Chuo cha Maasai Mara.
- Asiba, A., (1985, August 30). *Can Sheng' Stand the Test of Time*. Sunday Nation Nairobi
- Athuman, M. R., (2015). *Athari za kiisimu za lugha ya kiswahili katika lugha ya kiyao (Tasnifu)*. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Kitivo cha Sanaa na Sayansi ya Jamii.
- Babbie, E. (1999). *The Basics of Social Research*. Belmont: Wadsworth Publishing Company.
- Babbie, E. (1992). *The practice of social research* 6th edition. Publishing Company.
- Bagheri, M.S., (2012). *Error Analysis: Source of L2Learners' Errors*. Islamic Azad University. (Unipublished)
- Baljit, B., (1999). "Native Language Interference in Learning a Second Language: Exploratory Case Studies of Native Language Interference with Target Language Usage." *International Education Journal*, Vol. 1(1): 22-31.
- Bartoo, J. P., (2004). *Acquisition of English Syntax by Keiyo L1 Speakers*. Tasnifu ya M.A (Isiyochapishwa), Chuo Kikuu cha Egerton, Kenya.
- Berg, B. C., (2007). *Qualitative research methods for the social science (6th ed)*. California: Person Education Ally & Bacon.

- Besha, R.M., (1994). *Utangulizi wa Lugha na Isimu*. Dar es Salam: Dar es Salaam University Press.
- Bosha, I., (1993). *Taathira za Kiarabu katika Kiswahili pamoja na Kamusi Thulathiya*. Dar es Salaam: Dar es Salaam
- Cann, R., (1983). *Formal Semantic*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Chepkwony, L. C., (2011). *Uchunguzi wa Matatizo ya Kisarufi miongoni mwa Wanafunzi Wa Kikipsigis: Mfano Wilaya ya Bomet*. Tasnifu ya M. A. (Isiyochapishwa), Chuo Kikuu cha Kenyatta, Kenya
- Chiraghdin, S. & Munyampala, M., (1977). *Historia ya kiswahili*. Nairobi: Oxford University press
- Chomsky, N. & Halle, F. (1968). *Sound Patterns of English*. Cambridge: Cambridge University press
- Cohen, L., (2000). *Research methods in education(5th edition)*. London: Rutledge Farmer.
- Cooper, R. L., (1989). *Language planning and social change*. United Kingdom: Cambridge University Press.
- Corder, S. (1981). *Error Analysis*, London: Longman
- Corder, S. (1967). *Error analysis and interlanguage*. London: Oxford University Press.
- Cozby, P. C & Bates, S.C., (2012). *Method in behavioral science research (11th edition)*.New York: McGraw Hill.
- Cruse, D. A., (1986). *Lexical Semantic*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Ellis, R. (1994). *The study of Second Language acquisition*. London. Oxford University Press.

- Enon, C. J., (1998). *Education Research and Measurement*. Department of Distance Education, Makerere University. Uganda.
- Ewan, C.A& Calvert, D., (2000).*The Crisis of Scientific Researc*. In Garrick CAL Sage Publications.
- Faki, M. H., (2018). *Matumizi ya Lugha Tandawazi katika mitandao ya Kijamii, Changamoto katika lugha ya Kiswahili*. (Tasinifu). Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
- Goode and Hatt., (1952). *Methods in social research*. Tokyo: Mc Grow-Hill Book Company Inc.
- Gouala, P. M., (1991). *Problems of Learning English in the Congo due to Mother Tongue Interference*. Shahada ya P.G.D.E (Isiyochapishwa) University of Nairobi
- Guthrie, M., (1948). *Classification of bantu language*. London: Oxford University Press.
- Habwe, J. and Karanja, P., (2004).*Msingi wa sarufi ya Kiswahili*. Nairobi.Phoenix publisher University Press.
- Haroon, M., (1998). *Kuathirika kwa Kiswahili na Kigisu Nchini Uganda Kifonolojia, Kimofolojia, Sintaksia na Utamaduni*. Tasnifu ya M.A (Isiyochapishwa) Kampala University Press
- Haule, F., (2014). *Muundo wa Njeo za Lugha ya Kingoni*. (Tasnifu) Chuo Kikuu cha Kenyatta.
- Hooper, J. (1976). *Introdution to Generative Phonology*. Oxford: Oxford university press

- Hyman, L., (1975) *Phonology: Theory and Analysis*. New York: Holt Rinehart and Row
- Iribemwangi, Iribemwangi,P., (2010) *The Structure of Kiswahili Sounds, Sound changes and Words*. Saarbruken: Verlag
- James, C., (1998). *Errors in Language Learning and Use Exploring Error Analysis*. Harlow. Longman
- Kapinga, M.C. (1983). *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu*. (SAMIKISA). Dar es Salaam: TUKI.
- Kerlinger, F. N., (1979). *Behavioural research: A conceptual approach*. New York: Holt Rinehart & Winston Inc.
- King'ei, K., na Konbia, J., (2007). *Lugha kama kitambulisho: Changamoto ya sheng nchini Kenya*. Nordic Journal of African Studies 16 (3): 320 – 332.
- Kipacha, A., (2012). *Masters dissertation on Launi za Kiswahili Sanifu na Kiswahili Fasaha kwa Tanzania Bara na Zanzibar* (Haijachapishwa)
- Kisakwah, B. A., (2014) *Uchanganuzi Makosa na Muundo Sentensi: Ulinganisho wa Sentensi Sahili za Kiswahili Sanifu na za Kisuba*. (Tasnifu ya Uzamili). Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Kitsao, R.. (2015). *Uchanganuzi wa makosa ya Kisarufi katika insha za Wanafunzi wa Shule za Msingi yanayochangia matokeo mabaya ya mtihani, Kata ya Ganze, Kaunti ya Kifili*. (Tasinifu ya uzamili) Chuo Kikuu cha Pwani Kenya.
- Kiunga, M.T., (2016). *Maana ya Usemi na Mazungumzo katika Mitandao ya Kijamii hususani Facebook na Twitter*. (Tasinifu) Chuo Kikuu cha Kenyatta
- Kombo, D. K. and Tromp, D. L. A., (2006). *Proposal and thesis writing introduction*. Nairobi: Paulines publications Africa.

- Kothari, C. R. (1990). *Research methodology: Methods & techniques*. Wishwa
- Kothari, C. R. (2008). *Research methodology: Methods and technique*. New delhi:
New Age International Publishing LTD.
- Kress, T.M., (2008). *United state of Americage*
- Labov, W., (1972). *Language in the inner city: Studies in black english vernacular*.
Philadelphia: University of Pennsylvania press.
- Laufer, J., (1997). *Some Properties of the Language Learner's Lexicon as Evidenced by Lexcal Confusion*. IRAL, 29 (4), 317-330
- Lengo, P. E., (1995). *Contribution of Error Analysis to Foreign Language Teaching*.
- Lucius, M. T., (1978). *Misingi ya Kiswahili*. Mhenga publishing Consultants
Company Limited.
- Lusesa, J., (2013). *Athari ya lugha ya kisukuma katika kujifunza kiswahili (Tasnifu)*. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Kitivo cha Sanaa na Sayansi ya Jambii.
- Macharia, M., (2013). "The Phonological Basis of Misspellings in the Written english of Kikuyu Speakers". *Journal of Language, Technology & Entrepreneurship in Africa*, Vol. 4(2)
- Maganga, C., (1997) *Historia ya Kiswahili*. Dar es Salaam Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
- Mangwa, D. O., (2005). *Athari za Kikisii katika Kiswahili na Zinavyochangia Matokeo Mabaya ya Mtihani wa Kitaifa wa Kiswahili kwa Wanafunzi Wakisii Wilayani Kisii Kusini*. Tasnifu ya M.A (Isiyochapishwa), Chuo Kikuu cha Egerton, Kenya.

- Masamba, D. P.B. na Mlacha, S.A.K., (1988). *Kiswahili: Jarida la Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili*: Dar es salaam: TUKI
- Masebo, J. A. & Nyangwine, N. (2007). *Nadharia ya lugha: Kiswahili kidato cha 5 & 6*. Dar es salaam: Nyambari Nyangwine Publishers.
- Masebo, J. A. & Nyangwine, N. (2008). *Nadharia ya lugha: Kiswahili kidato cha 5 & 6*. Dar es Salaam: Nyambari Nyangwine Publishers.
- Massamba & wenzake., (2004). *Fonolojia ya kiswahili sanifu (FOKISA): Sekondari na vyuo*. Dar esSalaam: TUKI. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Massamba, D. P. B.,(1986). On the Influence of Local Languages on Kiswahili: The Case of Mara Region in Tanzania. *Kiswahili*, 53/1 na 53/2, 67-83
- Massamba, D.P.B.,(2011). *Maendeleo katika nadharia ya fonolojia*. Dar es Salaam: TUKI. Chuo kikuu cha Dar es Salaam.
- Matinde, R. S., (2012). *Dafina ya lugha isimu na nadharia: Kwa sekondari, vyuo vya kati na vyuo vikuu*. Mwanza: Serengeti Educational Publishers Ltd.
- Mbaabu, I. (1985). *Sarufi ya Kiswahili*. Nairobi. KLB
- Mbaabu, I. (1995). *Usahihishaji wa Makosa katika Kiswahili*. Nairobi. Longhorn Press
- Mbaabu, I. (2007). *Historia ya Usanifishaji wa Kiswahili*. Dar es Salaam. TUKI. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Mbaabu, I. (1978). *Kiswahili Lugha ya Taifa*. Nairobi. KLB.
- Mbwesa, K. J., (2006). *Introduction to Management Research. A study Handbook*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Mekacha, R. D. K., (2011). *Isimu jamii: Nadharia na mktadha wa kiswahili*. Dar es Salaam: TATAKI. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

- Mgullu, S. R., (1999). *Mtalaa wa Isimu: fonetiki, fonolojia na mfolojia ya Kiswahili*. Nairobi: Longhorn publishers.
- Mhilu, G.D., (2005). *Language It's Nature and Use*
- Mligo, E.S., (2012). *Jifunze utafiti mwongozo kuhusu utafiti na utamaduni wa ripoti yenye Mantiki*. Dar es Salaam. Ecumenical Gathering (EGY)
- Mochiwa, Z. M., (1979). *The Impact of Kiswahili Language on Ethnic Languages: A Case Study from Handeni District*. Tasnifu ya M. A. (Isiyochapishwa), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania.
- Mohamed, S., (1984) "Urban Versus Rural Swahili (A Study of Pemba Varieties)", Zanzibar. (Haijachapishwa).
- Msanjila, Y. P., (2009). *Isimu jamii. Sekondari na vyuo*. TUKI. Dar es Salaam
- Mtungu, B. N., (2001). *Makosa ya Kileksia katika Insha na cahanzo chake: Uchunguzi wa shule tano za upili wilayani Kiambu*. (Tasnifu). Chuo Kikuu cha Kenyatta.
- Muchome, H. S. S., (1998). *The Impact of English on Ethnic Community Language in Tanzania* *A case study of Cinamwanga*. Tasnifu ya PhD (Isiyochapishwa). University of Paris.
- Mukuthuria, M., (2004). *Kuathiriana kwa Kiswahili na Kimeru: Mfano kutokana na Wanafunzi wa Kitigania, Kenya*. Tasnifu ya PhD (Isiyochapishwa), Chuo Kikuu cha Egerton, Kenya.
- Munyua, J. G., (2002). *The Emerging Viswahili and Kiswahili Research*. Katika K. I. Simala (Mh.) *Jarida la Utafiti wa Kiswahili* (kur. 97 – 107). Eldoret: Moi University Press

- Muthu, K. F., (2005). *Uchanganuzi wa Makosa ya Kisintaksia katika Tafsihi za Magazeti (Taifa Leo)*. Tasnifu ya PhD (Isiyochapishwa), Chuo Kikuu cha Nairobi
- Ndungu, M., (1999). *A syntactic study of the interlanguage of kikuyu learners of english as second language (PhD Thesis)*. Department of Linguistic and African Languages. University of Nairobi
- Ng'ang'a., (2002). *Makosa ya Kisarufi Katika Insha za Wanafunzi na Jinsi Yanavyoshughulikiwa na Walimu Katika Tarafa ya Ndaragwa*.Tasnifu ya Uzamili (haijachapishwa) Chuo Kikuu cha Nairobi
- Ngonyani, D. S., (1988). *A comparative study of kindendeule, kingoni, and kimatengo (M.A Dissertation)*.University of Dar es Salaam. Unpublished.
- Ngugi, J. K., (2007). *Uchunguzi wa Taathari za Kifonolojia miongoni mwa Wanafunzi Wagikuyu: Mfano kutoka Tarafa ya Bahati, Nakuru*. Tasnifu ya M. A. (Isiyochapishwa). Chuo Kikuu cha Egerton, Kenya.
- Nyagah, S. K., (2016). *Uchanganuzi wa Makosa ya Kifonolojia na Kimofolojia yanayojitokeza katika kazi Andishi za Wanafunzi wa Shule za Upili, Tigania, Jimbo la Meru*. Tasnifu ya uzamili (Haijachapishwa) Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Nyanda, J., (2015). *Athari za lugha ya kinyamwezi katika kujifunza lugha ya Kiswahili*.Tasinifu ya uzamili (Haijachapishwa)Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Kitivo cha Sanaa na Sayansi ya jamii.
- Obara, J.M., (2014). *Uchanganuzi wa Makosa yanayofanyika na Wanafunzi wazungumzaji wa lugha ya Ekegusi*. Tasnifu ya uzamili (Haijachapishwa) Chuo Kikuu cha Nairobi

- Ontieri, J. O., (2010). *Uchanganuzi wa Makosa katika Insha za Wanafunzi wa Shule za Upili:Mfano wa Wilaya ya Nakuru, Kenya*. Tasnifu ya Uzamifu (Isiyochapishwa), Chuo Kikuu Cha Egerton, Kenya
- Onyango, J. O., (1997). *Uziada wa kisarafu katika kiswahili cha wanafunzi wa kinyala: Mtazamo wa uchanganuzi linganuzi. (Master thesis and Dissertation)*. Kenyatta University Institutional Repository. School of Humanities and Sciences. Department of Kiswahili and African languages.
- Orodho, J.A., (2009). *Elements of Education and Science Research Method*. 2ed. Maseno: Kanezja Publisher
- Otiende, M. A., (2013). *Athari za kimofonolojia za kisoluba katika matumizi ya Kiswahili sanifu kama lugha ya pili (Tasnifu)*. Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Patton, M. Q., (2001). *Qualitative Research Methods*. Thousands Oaks CA: Sage publication.
- Prakashan: New Delhin.
- Randolph, J. J., (2009). *Research and Evaluation. In practical Assessment. A Guide to writing the Dissertation Literature Review*. Walden University. Unpublished.
- Retrieved June 21, 2014 from <http://www.google.com>.
- Richard, J. C. (1972). Social factors, Interlanguage and Language Learning. *Language Learning* 22:159 – 188
- Richard, J. C. (1974). *Error analysis: Persepectives on second language acquisition*. London: Longman.
- Richard, J. C. (1975). *The Context for Analysis Error*. Singapore. Los Angeles.

- Roethlisberger, F. J., (1954). *Barriers to communication Between Men*: In Hayakawa S.I. (ed). USA: Language Meaning Maturity Romaine, S., (1994). *Language in Society: An Introduction to Socio – linguistic*. Oxford
- Rubanza, Y. I., (2003). SARUFI: Mtazamo wa Kimuundo. Dar es Salaam. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
- Selinker, L. (1972). Interlanguage. *International Review of Applied Linguistics in Language Teaching*, 10(3), 219-231.
- Sovu, A. Y., (2011). *Matumizi ya Kiha katika Kiswahili cha Mazungumzo*. Tsunifu. Chuo Kikuu cha Dar es salaam
- Trudgill, P., (1983). *Social linguistic: An introduction to language and society*. New York: Penguin.
University Press
- Walliman, N., (2011). *Research methods the basics*. New York: Routledge publisher.
- Wanyoike, E. N., (1978). Vikwazo katika Mafunzo ya Kiswahili Kenya katika Lugha Vol5 No3. Nairobi: *Kenya Language Association*.
- Wardhaugh, R., (1994). *Investigating language: Central problems in linguistic*. United Kingdom: Black well publishing
- Weiss, H. C., (1972). *Evaluation Research*. Edgewood Cliiffs, New Jersey: Prentice-Hall
- Wenceslaus, M., (2015). *Athari ya lugha ya kijita katika kujifunza kiswahili (Tasnifu)*. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Kitivo cha Sanaa na Sayansi ya Jamii.

VIAMBATISHO

KIAMBATANISHO NA: 1

MASWALI KWA WAZUNGUMZAJI WA KIKURYA KULINGANA NA

UFAHAMU WAO

Jina.....

Umri.....

Jinsia.....

Kiwango cha Elimu.....

1. Je, wewe ni mzawa halisi wa lugha ya Kikurya?

Ndiyo Hapana

Ndiyo Hapana

2. Je, unaweza kuzungumza kwa usahihi lugha zote mbili, Kikurya na Kiswahili?

Ndiyo Hapana

Ndiyo Hapana

3. Je, ni maneno yapi ya Kiswahili unafikiri wazungumzaji wa lugha ya Kikurya

hawawez kuyaandika kwa ufasaha?

a)

b)

c)

d)

e)

f)

g)

4. Unafikiri ni sababu zipi kwa ujumla zinachangia lugha ya Kikurya kuathiri

Kiswahili sanifu?

a)

b)

c)

d)

e)

KIAMBATANISHO NA: 2

MASWALI KWA WAZAWA WA KIKURYA WENYE UWEZO WA
KUANDIKA

Jina.....

Umuri.....

Jinsia.....

Kiwango cha elimu.....

1. Je, wewe ni mzawa wa kabila la Kikurya?

Ndiyo Hapana

Ndiyo Hapana

2. Je, unaweza kuzungumza kwa ufasaha lugha zote mbili, Kikurya na Kiswahili?

Ndiyo Hapana

Ndiyo Hapana

3. Je, kuna athari yoyote inayojitokeza katika mpangilio wa sentesi

iliyosababishwa na lugha ya Kikurya katika Kiswahili sanifu?

Ndiyo Hapana

Ndiyo Hapana

4. Iwapo jibu lako ni ndiyo, thibitisha kwa mifano kwa kutunga sentensi fupi fupi za Kiswahili.

a)

b)

c)

- d)
- e)
- f)
- g)

5. Je, kuna sababu zozote zinazochangia lugha ya Kikurya kuathiri Kiswahili Sanifu?

- a)
- b)
- c)

KIAMBATANISHO NA: 3**MASWALI KWA WAMILSI WA LUGHA YA KIKURYA**

Jina.....

Umuri.....

Jinsia.....

Kiwango cha elimu.....

1. Je, wewe asili yako ni mkurya?

Ndiyo Hapana

Ndiyo Hapana

2. Je, unapokuwa nyumbani unatumia lugha zote mbili Kikurya na Kiswahili katika mawasiliano?

Ndiyo Hapana

Ndiyo Hapana

3. Je, unaweza kutamka maneno haya ya Kiswahili kwa ufasaha?

Jamvi Chumvi

Kuoga Mboga

Suruali Msiba

Soksi Tafadhali

Uji Nibipu

Sketi Sketi